# Nipashe

Jumamosi Januari 18, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580131

www.ippmedia.com

The Guardian digital  nipasheTZ  nipasheTZ  nipasheTZ  0745 700710




## Lukuvi aibua tuhuma vigogo kuuza nyumba ya NHC kwa raia wa Ghana

UKURASA 3




UKURASA 13

# Wafanyabiashara wapaza sauti usajili laini za simu

**WAHOFU** uchumi kuporomoka, waitupia lawama Nida kusuasua kutoa vitambulisho...*Endelea ukurasa wa 2*

## YALIYOMO


**UKURASA WA 2**

**MO DEWJI AZIDI KUNG'ARA KWA UTAJIRI BARANI AFRIKA**

MFANYABIASHARA Mohammed Dewji, maarufu Mo Dewji, ameendelea...

**UKURASA WA 3**

**KUBENEA AIBUA UPYA SAKATA KUNG'OLEWA MEYA JIJI DAR**

MBUNGE wa Ubungo, Saeed Kubenea, ameibua upya sakata la kung'olewa kwa Meya...


## SHAHIDI AELEZA MKIMBIZI ALIVYOBAKA MWENZAKE

UKURASA 3



IGP Simon Sirro



Zitto Kabwe

# Polisi wazuia mkutano wa Zitto jimboni kwake

UKURASA 2




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play  App Store



**MICHEZO** UBABE WA MTIBWA WAISHIA KWA KMC UK. 31

MAONI, KATUNI UK.6

HABARI KITAIFA

# Wafanyabiashara wapaza sauti usajili laini za simu

**Na Waandishi Wetu**

ZIKIWA zimebaki siku mbili kuzimwa kwa laini za simu ambazo hazijasajiliwa kwa alama za vidole, baadhi ya wafanyabiashara wamepaza sauti na kuonya kuporomoka kiuchumi kwa kuwa hawajasajiliwa kwa kukosa vitambulisho vya taifa.

Juzi, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), ilisema watakaositishiwa huduma za laini zao zao ifikapo Januari 20, wanaweza pia kuendelea na utaratibu wa usajili kwa lengo ama kurudisha laini zao zitakazokuwa zimefungwa au kupata laini mpya na kwamba usajili ni endelevu.

Aidha, kilio kimesikika kwenye mikoa yote nchini kwa wananchi wengi kukosa namba za utaifa ili watimize sifa ya kuandikishwa na kuiomba serikali kuangalia suala hilo kwa jicho la pili.

Takwimu za Januari 7, mwaka huu, zilizotolewa na TCRA zilionyesha kuwa zaidi ya Watanzania milioni 22,796,472 sawa na asilimia 47.5 hawajasajiliwa.

Mkoani Shinyanga, wanafanyabiashara ambao bado hawajasajili laini zao, wamedai endapo zikizimwa watakosa mawasiliano katika biashara zao na hatimaye kushuka kiuchumi.

Wakizungumza na Nipashe kwenye ofisi za Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (Nida) mkoani humo, walisema kupata namba imekuwa tatizo kubwa na ndicho kinachowakwamisha kusajili laini zao.

Mmoja wa wafanyabiashara hao, Mabula Halfani, ambaye anafanya biashara ya kuuza nguo kutoka Kata ya Tinde, Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, alisema siku nne sasa anahangaikia kupata namba ya Nida ili akasajili laini yake ambayo ina namba nyingi za wateja na wafanyabiashara wenzake.

"Siku hizi mbili zilizosalia za kusajili laini za simu kwa alama ya vidole ni chache sana kutokana na changamoto zilizopo kwenye upataji wa namba ya Nida," alisema na kuongeza:

"Watu tuko wengi bado hawajasajili, hivyo tunamwomba Rais John Magufuli aongeze muda tena kwa sababu tukizimiwa laini zetu za simu, wafanyabiashara tutaathirika sana.

"Mfanyabiashara ambaye hana mawasiliano ya simu kamwe hawezi kuendesha biashara yake vizuri lazima atafeli na kushuka kiuchumi kwa sababu simu kwetu sisi ndio kila kitu unaweza kupigiwa simu na mteja ana hitaji umpelekee mzigo, au wenzako wanakutafuta kuna dili fulani sasa usipokuwapo hewani una kosa hela.

Naye Ngalu Joseph mkazi wa Shinyanga, alisema ana wiki ya tatu tangu alipojiandikisha kupata kitambulisho na alikwenda kwenye ofisi hizo, ili apate namba lakini hadi jana bado alikuwa anahangaika kupata namba za Nida ili akasajili laini yake ya simu huku, akiomba kasi iongezwe kwa watoaji wa namba hizo.

Ofisa Msajili wa Nida mkoani Shinyanga, Nathanael Njau, alisema utoaji wa namba za vitambulisho unaendelea vizuri na kubainisha idadi kubwa ya watu ambao wamesalia kupata namba ni ambao wamejiandikisha hivi karibuni.

INAENDELEA UK 8



Baadhi ya wakazi wa Jiji la Dodoma, wakiwa kwenye foleni kutafuta vitambulisho vya Taifa nje ya Ofisi za Mamlaka ya Vitambulisho (NIDA), jijini humo, jana, kwa ajili ya kusajili laini zao za simu, kabla ya kufungwa kwa zoezi hilo, Jumatatu ijayo. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Polisi wazuia mkutano wa Zitto

**Na Mwandishi Wetu**

JESHI la Polisi Wilaya ya Kigoma, limezuia mkutano wa hadhara wa Mbunge wa Kigoma Mjini, Zitto Kabwe, kwa kile kilichoelezwa ni sababu za kiintelijensia.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa kwa vyombo vya habari na Chama cha ACT-Wazalendo, mkutano huo ulikuwa ufanyike viwanja vya Mwanga Center, Manispaa ya Kigoma.

Chama hicho kilieleza kutoridhishwa kwake na sababu zilizotolewa na jeshi hilo, kwa kuwa zinamnyima mbunge huyo kutekeleza shughuli zake halali za kuwatumikia wananchi wa jimbo lake.

Kwa mujibu wa barua ya Jeshi la Polisi, yenye kumbukumbu KIG/A.24/60/VOL.I/114 yenye kichwa cha habari 'Taarifa ya Kuzuia Mkutano wa Hadhara wa Mbunge, Jeshi hilo lilikiri kupokea barua ya mbunge huyo ya Januari 14, mwaka huu, yenye kumbukumbu namba MB/OCD/KGMJN/13/2020.

"Napenda kukujulisha kuwa mkutano huo umezuiliwa kwa tarehe uliyoomba kwa sababu za kiusalama. Kutokana na taarifa za kiintelijensia zilizopo, huruhusiwi kufanya mkutano au kuendelea na maandalizi ya mkutano," ilieleza sehemu ya barua hiyo.

Taarifa zilizoifikia Nipashe baadaye jioni, zilieleza kuwa mbunge huyo ambaye ni Kiongozi Mkuu wa ACT-Wazalendo, aliamua kufanya mkutano wa ndani na viongozi wa chama hicho.

Hata hivyo, ilielezwa kuwa polisi wakiwa na sare na wengine wakiwa wamevaa kiraia, walivamia mkutano huo.

## Mo Dewji azidi kung'ara Afrika

**NA Mwandishi Wetu**

MFANYABIASHARA Mohammed Dewji, maarufu Mo Dewji, ameendelea kung'ara katika orodha ya matajiri barani Afrika.

Katika orodha iliyotolewa na jarida la Forbes, Mo Dewji ameendelea kushika nafasi ya kwanza katika kundi la 'Mfanyabiashara Tajiri Mdogo Kuliko Wote Afrika' kwa mwaka wa sita mfululizo.

Jarida hilo limebainisha kuwa Mo Dewji, ambaye ni Ofisa Mtendaji Mkuu wa Kundi la Kampuni za MeTL, anakadiriwa kuwa na utajiri wenye thamani ya Dola za Marekani bilioni 1.6.

"Licha ya kupoteza Dola za Kimarekani milioni 300 kulinganisha na tathmini yake iliyofanyika mwaka jana, pengine kwa sababu ya kupotea kwa fedha za kigeni, Dewji amekuwa akisema wazi juu ya mipango yake ya kujipanua kibiashara ndani ya Afrika.

"Akionekana katika mazungumzo mazito na wakuu wa nchi za Afrika hasa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, Afrika Kusini, Zambia, Uganda, Madagascar na Comoros, anaonekana dhahiri kukuza biashara na kuongeza utajiri wake kwa mwaka 2020 na miaka ijayo katika uzalishaji kupitia viwanda ambavyo anavimiliki," lilisema jarida hilo.

Forbes ilikaririwa ikisema katika mahojiano ya hivi karibuni, Dewji aliweka wazi kuwekeza Sh. bilioni 500 nchini Tanzania na kuzalisha ajira 100,000 miaka mitano ijayo.

Dewji ambaye ni mkereketwa na mpenzi mkubwa wa michezo, pia anajulikana kimataifa kutokana na uwekezaji alioufanya katika klabu ya soka ya Simba na sasa akiwa mwenyekiti wa bodi.

Mfanyabiashara huyo hajaficha kiu yake katika uwekezaji kwenye michezo hasa baada ya kuahidi kuwekeza mamilioni ya shilingi katika maendeleo ya soka kwa kushirikiana na Ubalozi wa Sweden kwa ajili ya kujenga uwezo.

Kati ya mataifa 54 ya Afrika, ni nchi nane tu zenye mabilionea, Tanzania ikiwamo kwa kuwa na matajiri kadhaa akiwamo Dewji.

# HABARI KITAIFA

## Shahidi aeleza mkimbizi alivyombaka mwenzake

**Na Joctan Ngelly, KIGOMA**

SHAHIDI wa pili katika kesi inayomkabili mkimbizi wa kambi ya Nyarugusu, raia wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Ramadhani Salum (44), jana aliieleza Mahakama ya Wilaya Kigoma mshtakiwa huyo alivyombaka mwanamke mwenye umri wa miaka 39, raia wa Burundi, mkimbizi wa kambi ya Nduta wilayani Kibondo.

Salumu anakabiliwa na shtaka moja la kumbaka mkimbizi huyo mwanamke bila ridhaa yake kitendo ambacho ni kinyume cha sheria. Mshtakiwa huyo alipandishwa kizimbani jana mbele ya Hakimu Mkazi Katoki Mwakitalu.

Akiongozwa na Wakili wa Serikali Raymond Kimbe, shahidi huyo, Ntibaganyigwa Fides, raia wa Burundi, ambaye pia ni mkimbizi wa kambi ya Nduta, alidai kuwa Oktoba 4, mwaka jana, alikuwa kwenye kambi ya NMC, Kibirizi Manispaa ya Kigoma/Ujiji.

Wakati anatoka ofisi za IRC, alidai kuwa alisikia mtu akilia chumbani na alipoingia ndani, aliwakuta watu watatu. Ntabaganyigwa aliwataja watu aliyowakuta chumbani ni Salimu ambaye ni mshtakiwa, mwathirika wa ubakaji (jina linahifadhiwa) Niyokuru Yudes.

Kwa mujibu wa shahidi huyo, wakati anaingia katika chumba hicho, alimkuta mwathirika wa kitendo hicho akilia na mshtakiwa akiwa anatokwa na jasho jingi na ndipo alipomuuliza kwa nini analia.

Alidai kuwa kabla hajamjibu, Salum alijibu kuwa: "Analia kwa sababu tumemaliza kufanya mapenzi lakini amenigeuka."

"Mwathirika alipotaka kutoka nje, mshtakiwa alimshika mkono kumzuia huku akituambia sisi tumwambie kama anataka fedha ampatie inawezekana hawakuelewana na kwa lugha kati yao," alidai shahidi huyo.

Shahidi huyo aliendelea kudai kuwa mshtakiwa pia aliwaambia wamwombee msamaha kwa mwathirika ili asiende kusema kwa sababu akisema atafungwa.

Kwa mujibu wa shahidi huyo, baada ya mshtakiwa kusema hivyo, mwathirika alikataa na kusema: "Unaona amenichania gauni yangu kifuani na nguo yangu ya ndani. Mimi nilikuja kwa ajili ya matibabu, sikuja kwa ajili ya wanamume."

Shahidi huyo aliendelea kudai kuwa mshtakiwa alimbembeleza mwathirika asiende nje kwa manesi kusema kwa sababu yuko tayari kumpa chochote anachotaka kwa kuwa akienda kusema atafungwa.

Baada ya shahidi huyo kumaliza kutoa ushahidi wake, upande wa mashtaka ulidai kuwa jana walikuwa na shahidi mmoja na kuomba tarehe nyingine kwa ajili ya kuendelea kusikiliza mashahidi wengine waliobaki.

## Kubenea aibua upya sakata la Meya Dar

**Na Enock Charles**

HALI ya mambo katika Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam bado si shwari. Ndivyo mtu anavyoweza kusema kwa sasa baada ya baadhi ya wajumbe wa Baraza la Jiji hilo kuendelea kushikilia msimamo wao wa kupinga hoja za kumvua madaraka Meya Isaya Mwita.

Aidha, baadhi ya wajumbe wamesema wataendelea kumtambua Mwita kama Meya halali wa jiji hilo na watahudhuria vikao atakavyoitisha na si vinginevyo.

Mbunge wa Ubungo, Saeed Kubenea, akiwa ameambatana na Diwani wa Tabata, Patrick Asenga, aliwaambia waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana kuwa wataendelea kumpa ushirikiano Mwita na kuonya matumizi ya nguvu katika kumzuia kutekeleza majukumu yake.

"Tutahakikisha haki za wananchi wa Dar es Salaam zinalindwa, Mwita bado ataendelea kuwa Meya kwa sababu ya takwa la kikatiba na kikanuni la mbili ya tatu limeshindwa kutimizwa," alisema Kubenea.

Mbunge huyo alionya kuwa iwapo wajumbe kutoka Chama Cha Mapinduzi (CCM) wataendelea kushinikiza kuondolewa kwa Meya huyo kwa kile alichodai kinyume cha utaratibu, vikao vya Baraza la Madiwani wa Jiji la Dar es Salaam vitalazimika kuendeshwa kwa usimamizi wa vyombo vya ulinzi na usalama likiwamo Jeshi la Polisi kwa kuwa wajumbe kutoka vyama vya upinzani hususani Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), hawatakubali kuendeshwa pasipo Meya huyo.

Juzi, kikao cha Kamati ya Fedha na Uongozi ya Halmashauri hiyo, kilifanyika chini ya ulinzi wa polisi baada ya kuwapo

mvutano ulioashiria vurugu baada ya wajumbe wanaomtambua Mwita kama Meya halali kuendelea kutaka aongoze kikao hicho huku wale wasiomuunga mkono wakitaka Naibu wake, Abdala Mtinita, aongoze.

Awali, ilidaiwa kuwa Mwita ndiye aliyekuwa akiongoza kikao lakini baadaye polisi walipoitwa walimtoa kikaoni kwa mazungumzo na kikao kikaendeshwa na Mtinika chini ya ulinzi wa polisi na wajumbe kutoka upinzani walipohoji alikopelekwa, walijibiwa na

Mkurugenzi wa Jiji kuwa polisi wamemchukua na hawajui walikompeleka.

Mwita alikwenda kuhudhuria kikao hicho cha juzi licha ya kutopewa mwaliko na Mkurugenzi wa Jiji na badala yake alipewa Naibu Meya kwa lengo la kuendesha kikao hicho kilicholenga kujadili ajenda kadhaa ikiwamo kusoma na kuthibitisha muhtasari wa kikao cha Kamati ya Fedha na Uongozi kilichofanyika Desemba 23, mwaka jana, na taarifa ya mapato na matumizi ya mwezi huo.



Mkurugenzi wa Huduma za Matibabu wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Mwananyamala, Dk. Isdory Kiwale (kulia), akionyesha kwa waandishi wa habari, mtambo wa kuzalisha mifuko ya kuhifadhia taka kwa kutumia chupa na mifuko ya plastiki hospitalini hapo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MARY GEOFREY**

## Lukuvi aibua tuhuma uuzwaji nyumba NHC

**Na Romana Mallya**

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, ameibua tuhuma juu ya uuzaji wa nyumba ya Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) kwa raia wa Ghana, akihusisha majina ya watu wakubwa kushiriki na kutaka kufanyika uchunguzi.

Kutokana na awali kuiagiza NHC ifuatilie jambo hilo na kuchelewa, jana Lukuvi alilikabidhi suala hilo ofisi ya Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai (DCI) ili ianze uchunguzi mara moja utakaowezesha nyumba hiyo kurudi serikalini.

Maagizo hayo aliyatoa baada ya kufanya ziara kwenye nyumba mbili zilizouzwa ikiwamo nyingine ya Shirika la Bima la Taifa (NIC).

"DCI kuanzia leo (jana) ufanye uchunguzi kwa nini hii nyumba imehama kutoka Shirika la Nyumba mpaka kumilikiwa na mtu binafsi na mtu huyo ni mgeni," alisema Lukuvi.

Alisema amekwenda hapo makusudi kwa ajili ya kukabidhi suala hilo ili polisi waanze uchunguzi wa jambo hilo.

"Yeyote aliyehusika awe wa NHC au serikalini au wa wizarani kwangu, shughulikeni naye kwa mujibu wa taratibu zenu," alisema.

Pia alitaka taarifa zote za hapo zikabidhiwe kwa DCI ili waanze uchunguzi huo kwa sababu tangu mwezi uliopita alitoa maagizo hayo, lakini nyumba hiyo haijarudi serikalini.

"Yaelekea Shirika la Nyumba mmeshindwa. Wakabidhini wenye kazi yao wafanye hii kazi. Nataka hii nyumba irudi serikalini," alisema.

Waziri Lukuvi alisema raia huyo wa kigeni kutoka Ghana alikuja Tanzania kufanya kazi kwenye kampuni ya ujenzi (hakuitaja) na kampuni hiyo ilipanga na baadaye akawa mpangaji.

"Mikataba ipo, ukiendelea hadi sasa yeye ameinunua hii nyumba kampuni hiyo yeye ni mwakilishi wake, ameinunua haiwezekani nyumba ya shirika ihame mikono kutoka NHC halafu ikaja kwake na shirika wameachia kwamba si nyumba yao.

"Hata yeye nilipoagiza alete nyaraka hana uhakika hii nyumba aliipataje ndiyo maana nimekabidhi kwenye ofisi ya upelelezi ya polisi ili waanze uchunguzi."

Waziri Lukuvi alisema mpaka sasa hati ya nyumba hiyo imeshabadilishwa imewekwa jina la raia huyo wa kigeni.

"Leo (jana) nimewaita polisi

INAENDELEA UK 8


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Baruapepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaawa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA
Tarehe 17-01-2020

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Alhamisi tarehe **23-01-2020** kampuni ya **Mainline Carriers Ltd** itasafirisha Mzigo wenye vipimo vikubwa kutoka **Dar es salaam kuelekea Mafinga,** magari hayo yenye namba za usajili:

**T 622 DFA / T 837 DJB**
**T 653 DFA / T 887 DJB**

2. Magari hayo yana vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Urefu** | - | **mita** | **31** |
| **Upana** | - | **mita** | **4.30** |
| **Kimo** | - | **mita** | **5.20** |

3. Njia itakayotumika: **Dar es salaam hadi Mafinga kupitia Iringa,** Magari yatasafiri muda wa mchana tu ***(kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12.00 jioni)***

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

115589902

# Profesa aona shida vigezo utoaji mikopo elimu ya juu

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

MAKAMU Mkuu wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, Prof. Elifas Bisanda, ameishauri Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB), kubadili falsafa ya utoaji wa mikopo inayolenga kuwakopesha wasiokuwa na uwezo wa kifedha, badala yake iwakopeshe wenye uwezo.

Prof. Bisanda alitoa ushauri huo juzi jijini Mbeya wakati wa mkutano wa viongozi wa serikali ya wanafunzi wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUTSO) kutoka nchi nzima, akieleza kuwa falsafa ya sasa ya kuwakopesha wasiokuwa na uwezo ni kuwaongezea mzigo wa maisha.

Alisema kwa sasa mfumo wa ajira ni mgumu, hivyo endapo wanafunzi hao wasiokuwa na uwezo wa kifedha wataendelea kukopeshwa, itakuwa ngumu kwao kurejesha mikopo hiyo ikiwa hawatapata ajira ikizingatiwa riba ya mikopo hiyo itaendelea kuongezeka kila mwaka.

Alisema endapo watasomeshwa bure na bodi, watakuwa wamepunguziwa mzigo wa deni na hivyo hata wasipopata ajira na wakaamua kujiajiri, itakuwa rahisi kwao kuendesha maisha yao na kuwasomesha wengine.

Alisema watoto wa matajiri wakikopeshwa, ni rahisi kurejesha mikopo hiyo hata kama hawataajiriwa baada ya kumaliza masomo yao ya elimu ya juu na kwamba wakisharejesha fedha hizo zinarudi tena kwenye mzunguko wa mkopo.

"Tunaishukuru serikali kwa kuanzisha mfumo huu wa utoaji wa mikopo kwa wanafunzi, ni kweli wanasaidia hata watoto wa maskini kusoma elimu ya vyuo vikuu, lakini mtazamo wangu ni kwamba utaratibu huo hausaidii sana," Prof. Bisanda alisema na kufafanua:

"Mtazamo wangu ni kwamba serikali ingetenga fungu fulani la fedha kwa ajili ya kuwakopesha watoto wa matajiri ambao watakuwa na uwezo wa kurejesha mapema pamoja na riba na hiyo riba irudi kusaidia watoto wa maskini kwa kusoma bure."

Alisema utaratibu huo wa kuwasaidia watoto wa maskini unatakiwa uendane na viwango vya ufaulu kwa maelezo kuwa kinatakiwa kiwekwe kiwango cha ufaulu wa mwanafunzi anayestahili kusomeshwa bure.

Hata hivyo, aliwataka wanafunzi hasa wa Chuo Kikuu Huria (OUT), ambao wengi ni watumishi, kutopenda kusoma kwa kutegemea mkopo kwa maelezo kuwa mkopo ni utumwa wa maisha ya baadaye kwao.

"Unapokopa ujue kwamba leo unakula maisha yako ya baadaye, maana utalazimika kulipa mkopo huo na riba juu, lakini ukipambana ukajisomesha mwenyewe utakuwa huru sana," alibainisha.

Vilevile, alisema utaratibu wa Bodi ya Mikopo kutaka vyuo vikuu kuwasilisha saini za wanafunzi waliopokea mikopo yao ndani ya siku 30 ni mwiba kwa chuo hicho kwa maelezo kuwa wanafunzi wa chuo hicho wamesambaa nchi nzima na hivyo ni vigumu kuwapata wote kwa muda huo.

Alisema baadhi ya wanafunzi wanaishi vijijini na hivyo akaomba angalau bodi hiyo iwape siku 90 za kuwasilisha saini hizo kwa maelezo kuwa muda huo ndiyo utatosha kuwafikia wanafunzi wa matawi yote ya Tanzania Bara na Visiwani.

Awali, Rais wa Serikali ya Wanafunzi wa Chuo hicho, Felix Lugeiyamu, alisema chuo kina mfumo mzuri wa uongozi ambao unawashirikisha pia wanafunzi kwenye majukumu ya utawala.

Alisema serikali ya menejimenti ya uongozi wa serikali ya wanafunzi wa chuo hicho wameandaa mradi maalum wa kufundisha Watanzania kuhusu uzalendo kwa taifa lao, utakaowafikia wananchi wote.

"Mradi huu utagharimu zaidi ya Sh. milioni 300 na tunaamini zitapatikana, lakini sisi kama menejimenti, tumesaidia mambo mbalimbali kwenye chuo ikiwa ni pamoja na kununua jenereta kwa ajili ya kituo cha Lindi na viti kwa kituo cha Morogoro," alisema.

Alisema wanaamini uzalendo ni imani kama ilivyo kwa imani zingine na hivyo watahakikisha wanasambaza imani hiyo mpaka ngazi ya familia ili kuchochea maendeleo ya taifa.



Mwenyekiti wa Taasisi ya IMED, Dk. Donath Olomi, akitoa mada kwa wadau wa nishati mbadala, wakati wa uzinduzi wa awamu ya pili ya huduma ya kiatamishi cha biashara zinazohusika na nishati jadilifu (TAREBI), inayotolewa na taasisi hiyo, kwa ushirikiano na Taasisi ya SELCO ya India kwa ufadhili wa Taasisi ya CS Mott. **PICHA: JOHN BADI**

# Waziri aonya takwimu feki utafiti

**Na Paul Mabeja, DODOMA**

NAIBU Waziri wa Viwanda na Biashara, Mhandisi Stella Manyanya, ameyaonya mashirika na taasisi ambazo zimekuwa zikitoa takwimu zisizo sahihi na kusisitiza kuwa serikali haitazivumilia.

Manyanya aliyasema hayo juzi wakati wa uzinduzi wa programu ya miezi 18 ya kuzijengea uwezo bidhaa zinazozalishwa nchini kuingia katika soko la nje inayoratibiwa na Taasisi ya Utafiti wa kuondoa Umaskini (REPOA) kwa kushirikiana na Umoja wa Ulaya (EU).

Alisema serikali itaendelea kuzifanyia kazi taarifa za utafiti ambazo zinatolewa na wadau mbalimbali wa maendeleo zenye ukweli katika kuhakikisha inafikia uchumi wa kati 2025 na siyo za kupikwa.

"Nitumie fursa hii kusema kuwa wote wanaopika takwimu ambazo zinachonganisha hatutaendelea kuwafumbia macho, lakini wale ambao wanatoa takwimu sahihi ambazo zinaweza kulisaidia taifa letu kupiga hatua tutaendelea kuzifanyia kazi," alisema Manyanya.

Aliyashukuru mashirika na taasisi ambazo zimekuwa zinaandaa utafiti kwa usahihi na serikali imeutumia katika kuboresha mambo mbalimbali ikiwamo sera pamoja na sheria zake.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Repoa, Dk. Donald Mmari, alisema katika programu hiyo wataanza na maeneo matano ambayo ni pamoja na kilimo cha mbogamboga na matunda.

"Tumeona katika kilimo hicho kunasoko kubwa sana nje ya nchi ambalo kama tutaboresha tutaweza kuuza mbogambaga na matunda kwa kiwango kikubwa nje ya nchi hivyo kuongeza ajira kwa vijana na kinamama kwani hadi hivi sasa Tanzania inauza tani 3,000 za maparachichi nje ya nchi," alisema Dk. Mmari.

Alisema eneo la pili ni kilimo cha mpunga ambacho pia mchele wa Tanzania unahitajika sana katika soko la nje, hivyo wakiboresha mazingira ya kilimo hicho, kutasaidia kupata soko la uhakika.

"Eneo la tatu ambalo tunataka kuliboresha ni katika bidhaa za ngozi pamoja na kuwa nchi yetu inaelezwa kuwa ya pili katika bara hili sekta hii bado haijatumika vizuri ili wafugaji wetu waweze kunufaika na mifugo yao na kuchangia katika ukuaji wa pato la taifa," alisema.

Eneo lingine watakalolifanyika kazi katika programu hiyo, alisema ni katika bidhaa za baharini ambazo hivi sasa zinahitajika sana katika soko la nje lakini bado hazijaboreshwa.

"Lakini katika eneo la tano ambalo ni la mwisho tutahakikisha kuwa tunafanyia kazi miundombinu ya usafirishaji na uchukuzi ili bidhaa zivunwe na kusafirishwa kwa wakati na kufika kwa mlaji katika ubora uleule," aliongeza Dk. Mmari.

## Mshtakiwa mauaji aangua kilio kortini

**Na Hellen Mwango**

UKUMBI namba moja katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, ulitawala vilio wakati mshtakiwa wa nne, Nduimana Zebedayo, maarufu kama mchungaji, kulalamika huku akilia kwa sauti kwamba wamenyimwa chakula kwa kuwa ni raia wa nje kwa siku tano katika Gereza la Keko.

Mchungaji wakati anatoa malalamiko hayo, raia mwenzake wa Burundi, Habonimana Nyandwi, alipoteza fahamu baada ya kuanguka chini wakati akipanda kizimbani kusikiliza kesi yao ya mauaji ya mwanaharakati Wayner Lotter (52).

Hatua hiyo ilisababisha askari polisi wawili kumnyoosha miguu, kumvua viatu na kumfungua mkanda wa kaptula aliyokuwa ameivaa.

Mahakama hiyo iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Mwandamizi Mfawidhi, Godfrey Isaya, ilianza shughuli zake saa 4:15 asubuhi kesi hiyo iliitwa na washtakiwa kupanda kizimbani.

Wakili wa Serikali Ester Martin alidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo bado haujakamilika aliomba tarehe nyingine ya kutajwa.

Baada ya maelezo hayo, Mchungaji alinyoosha mkono kuomba ruhusa ya kuzungumza na alianza kupangua kilio kwamba yeye na mwenzake aliyeanguka ni raia wa kigeni hawana ndugu hapa nchini wa kuwapelekea chakula, wamenyimwa haki ya kupata chakula kama wageni.

"Mheshimiwa (huku akilia kwa sauti) tunaomba huruma yako tupate haki yetu kama raia wa kigeni. Siku ya tano leo hatujapata chakula, tumedhoofu afya zetu," alidai Mchungaji huku akilia kwa sauti na kububujikwa machozi hali iliyosababisha ukumbi mzima kusikika miguno.

Upande wa Jamhuri ulipohojiwa na hakimu kuhusu malalamiko hayo, Wakili Martin alidai kuwa huduma zote wanatakiwa kupata wakiwa mahabusu ikiwamo malazi na chakula.

Alidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo uko katika hatua ya mwisho kukamilika na kwamba Ofisa wa Magereza ana majibu kuhusu malalamiko hayo.

Ifuatayo ni sehemu ya mahojiano kati ya Hakimu na Ofisa wa Magereza Inspekta Shabani:

ENDELEA UK 8

## HABARI KITAIFA

# Naibu Waziri aamuru kuachiwa ng'ombe waliokamatwa hifadhini

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu, ameiagiza Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA) kuiachia na kuirudisha mifugo, wakiwamo ng'ombe 179 waliokamatwa ndani ya Pori la Akiba la Mkungunero.

Ng'ombe hao ni mali ya Mathayo Marao, mkazi wa kijiji cha Kimotorok kilichopo ndani ya pori hilo katika Wilaya ya Simanjiro mkoani Manyara kwa makubaliano ya kutoingiza tena mifugo hiyo.

Uamuzi huo umechukuliwa kutokana na utata uliopo eneo ilipokamatiwa mifugo hiyo kwa vile Kimotorok ni miongoni mwa vijiji na vitongoji 366 vilivyo ndani hifadhi na vinavyosubiri uamuzi ya Rais John Magufuli na moja kati ya maagizo aliyoyatoa kwamba wananchi wa vijiji hivyo wasibughudhiwe hadi uamuzi wa mwisho utakapotolewa.

Kwa mujibu wa wahifadhi, mifugo hiyo iliyokamatwa mwishoni mwa mwaka jana, inadaiwa kukutwa mita 450 ndani ya pori hilo huku wananchi wakidai kuwa ilikutwa nje ya mita 450 kutoka kwenye mpaka mahali ambako wamekuwa wakiishi.

Mvutano huo baina ya wahifadhi na wananchi umesababisha Kanyasu kutumia busara na kufikia uamuzi huo kwa kuzingatia kuwa kijiji hicho kiko ndani ya hifadhi. Kutokana na majadiliano ya pande hizo mbili, Naibu Waziri alitoa uamuzi wa kuachiwa mifugo hiyo kwa makubaliano ya wananchi wa kijiji hicho kuheshimu sheria za uhifadhi kwa kutoingiza mifugo ndani ya hifadhi hadi pale uamuzi wa mwisho utakapotolewa na Rais Magufuli.

Akizungumza jana katika mkutano huo uliofanyika kwenye kijiji hicho, Naibu Waziri alisema uamuzi huo umefanyika kwa busara kwa vile mifugo hiyo ilibidi ipelekwe mahakamani.

Alisema kitendo cha kuacha kupeleka kesi hiyo mahakamani kinasaidia kupunguza idadi kubwa ya mifugo kufa kwa kuwa hadi sasa zaidi ya ndama 10 wameshakufa. Kanyasu aliwataka wananchi hao kuacha kutumia vibaya kauli ya Rais Magufuli kwa kuvamia maeneo mapya ya hifadhi bali wanatakiwa kubaki na mifugo yao mahali walipo.

**Kwa mujibu wa wahifadhi, mifugo hiyo iliyokamatwa mwishoni mwa mwaka jana, inadaiwa kukutwa mita 450 ndani ya pori hilo huku wananchi wakidai kuwa ilikutwa nje ya mita 450 kutoka kwenye mpaka mahali ambako wamekuwa wakiishi.**



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akibonyeza kitufe kuzindua huduma ya Ultra Sound, baada ya kuzindua huduma ya afya ya kijiji, katika Halmashauri ya Wilaya ya Kusini, Kizimkazi Dimbani, mjini Zanzibar jana, akiwa kwenye ziara ya kikazi ya siku tatu. **PICHA: OWM**

# Katibu mkuu ataka usalama mahala pa kazi

**Na Gwamaka Alipipi**

KATIBU Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na wenye Ulemavu, Andrew Massawe, amesema ujenzi wa uchumi wa viwanda hauna budi kwenda sambamba na uzingatiaji wa viwango vya usalama na afya mahali pa kazi ili kuepuka madhara yanayoweza kutokea.

Aidha, ameitaka Mamlaka ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi (Osha) kuongeza jitihada katika kuwaelimisha wananchi kuhusu utekelezaji wa Sheria ya Afya na Usalama Mahali pa Kazi ya mwaka 2003 pamoja na kuimarisha mifumo ya utoaji huduma kwa njia ya mtandao.

Aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam alipotembelea ofisi za Osha zilizoko Kinondoni jijini Dar es Salaam na kufanya kikao na menejimenti ili kupata mrejesho wa utekelezaji wa maelekezo na miongozo mbalimbali ambayo ofisi yake imekuwa ikiyatoa katika kuboresha huduma kwa wananchi.

"Katika kipindi hiki ambacho serikali inaweka msukumo mkubwa katika ujenzi wa uchumi wa viwanda, tunataka mageuzi haya ya viwanda yaende sambamba na uzingatiaji wa viwango vya usalama na afya mahali pa kazi ili kuepuka madhara yanayoweza kutokea endapo suala hili muhimu halitazingatiwa," alisema.

"Mmezungumzia pia kuhusu kupanua wigo wa kazi zenu hizi katika maeneo mengi ya nchi; hilo nalo ni jambo la msingi japokuwa tunataka kuweka msisitizo katika utoaji wa huduma kwa njia ya mtandao," aliongeza.

Pia alisema: Tunahitaji kuwa na ofisi walau katika maeneo yote muhimu, tunatakiwa kujenga ushirikiano mzuri na taasisi nyingine katika wizara ili tuweze kutumia majengo yaliyopo kwa pamoja kwa sababu hatuhitaji kujenga au kukodisha majengo kila mahali."

Naye Kaimu Mtendaji Mkuu wa Osha, Khadija Mwenda, alisema wanatarajia kufungua ofisi za Kanda ya Magharibi mkoani Tabora itakayohudumia mikoa ya Tabora, Kigoma, Rukwa na Katavi.

Pia alielezea namna taasisi yake imefanikiwa katika matumizi ya mifumo mbalimbali ya serikali ikiwamo mifumo ya malipo serikalini ya GePG, Muse na mfumo wa Ununuzi na Ugavi Serikalini (TANePS).


KUMBUKUMBU



SIMON IVAMBI

115589402

Leo tarehe **18/01/2020** baba yetu **Simon Ivambi** umetimiza Miaka 19 tangu umeitwa na Muumba Wetu.

Baba tunakukumbuka kwa mengi Upendo, Huruma, Busara na ushauri kwa familia ni miongoni mwa tunayokumbuka.

***Baba hakuna wa kuziba pengo lako,***

Unakumbukwa siku zote na Wanao:-**Sebastian,Veronica, Oliva, Janeth & Frida**

**Wajukuu:** Loide, Hans, Nancyse, Diana, Simon Senior, Agatha, Martin, Marcela, Simon Jr, Nancy Jr, Benard na Stevie. Wakwe zako na wanafamilia wote wa Mathias Ninga daima tunakuombea Baba upumzike kwa amani Bwana alitoa ,

***Bwana ametwaa jina lake lihimidiwe.***



MASETO AUCTIONEER & DEBT COLLECTOR LTD

**TANGAZO LA MNADA WA MAGARI (SALVAGE)**

KWA NIAMBA YA KAMPUNI YA BIMA (UAP INSURANCE TANZANIA COMPANY LTD), MASETO AUCTIONEER AND DEBT COLLECTOR LTD TUNAWATANGAZIA WANANCHI KUWA TUTAUZA KWA MNADA WA HADHA MAGARI (SALVAGE) YALIYOKO KWENYE YARD YA UAP MBEZI BEACH MAKONDE MAARUFU OFISI ZA MINARA YA SIMU BUNGE ROAD. MNADA UTAFANYIKA SIKU YA JUMAMOSI TAREHE 25/01/2020 KUANZIA SAA TANO (05:00) ASUBUHI, UKAGUZI WA MAGARI NI TAREHE 22/01/2020 KUANZIA SAA NNE ASUBUHI HADI SAA KUMI JIONI.

| S/N | NAMBA YA USAJIRI | AINA YA GARI | TOLEO LA GARI |
|---|---|---|---|
| 01 | T 739 BHB | TOYOTA | CRESTA |
| 02 | T 723 DRN | FAW | |
| 03 | T 479 CNC | TOYOTA | NOAH |
| 04 | T 253 DJF | NISSAN | SALON |
| 05 | T 596 DJY | TOYOTA | KLUGER |
| 06 | T 996 DFQ | TOYOTA | HARRIER |
| 07 | T 663 DBW | TOYOTA | CROWN |
| 08 | T 433 DMV | TOYOTA | IST |
| 09 | T 469 BBQ | MITSUBISH | MIN |
| 10 | T 161 AWX | JEEP | |
| 11 | T 186 CDD | V/WAGEN | POLO |
| 12 | T 273 CQQ | V/WAGEN | POLO |
| 13 | T 966 CHL | NISSAN | ELGRAND |
| 14 | T 868 BCL | TOYOTA | CHASER |
| 15 | T 628 CVW | TOYOTA | BRAVIS |
| 16 | T 788 DJE | AUD | |
| 17 | T 921 DQL | M/BENZ | |
| 18 | T 946 BHK | TOYOTA | HIACE |
| 19 | T 307 ASV | HYUNDAI | SANTAFEE |
| 20 | T 584 CMC | JEEP | |
| 21 | MC 156 BZC | MOTOR CYCLE | |

**MASHARITI YA MNADA**

1. MNUNUZI ATATAKIWA KULIPA NUSU YA BEI ILIYOFIKIWA MARA BAADA KUDONDOSHEWA NYUNDO YA MWISHO
2. NUSU INAYOBAKIA INATAKIWA KULIPWA NDANI YA SIKU TANO, KAMA HAITALIPWA BASI NUSU ILIYOLIPWA MWANZO HAITARUDISHWA NA MNADA UTARUDIWA

**KWA MAELEZO ZAIDI WASILIANA NASI KUPITIA NAMBA HIZI +255 765 999 000 OR +255 784 622 019 OR +255 715 622 019**

115590102

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# *Simba, Yanga na Azam kwa hili, sasa badilikeni*

TAYARI hata kabla raundi ya kwanza ya Ligi Kuu Tanzania Bara haijamalizika, tumeshuhudia miamba ya soka nchini, klabu za Yanga, Simba na Azam zikivunja mabenchi yao ya ufundi, kama si kuachana na makocha wakuu, kwa sababu mbalimbali.

Yanga ilianza msimu ikiwa na Kocha Mkuu, Mkongomani Mwinyi Zahera akisaidiwa na Mzambia Noel Mwandila kabla ya Novemba mwaka jana benchi nzima la ufundi kuvunjwa na makocha hao kutimuliwa.

Makocha hao walitimuliwa baada ya kushindwa kuiwezezesha timu hiyo kutinga hatua ya makundi ya michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika na kile kilichoelezwa kuwa ni kutounda timu ya ushindani kutokana na kushindwa kukiunganisha kikosi.

Kwa upande wa Simba, nayo ilianza msimu na aliyekuwa kocha wao, Mbelgiji Patrick Aussems akisaidiwa na Mrundi Masoud Juma kabla ya kumkataa msaidizi huyo na kisha kuletewa Dennis Kitambi.

Hata hivyo, licha ya kutolewa mapema kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika, kushindwa kuunda timu ya ushindani na kudhibiti nidhamu ya wachezaji kilielezwa ni sababu tosha ya uongozi wa Simba kuamua kumtimua Mbelgiji huyo na kisha kufikia makubaliano ya kuachana na msaidizi wake, Kitambi.

Azam FC, yenyewe ilianza msimu na Mrundi Etienne Ndayiragije akisaidiwa na Iddi Cheche, lakini ilifikia makubaliano ya kuachana naye baada ya Shirikisho la Soka nchini (TFF), kuhitaji huduma yake timu ya Taifa, Taifa Stars.

Kwa sasa Yanga, iliyokuwa ikinolewa na Kaimu Kocha Mkuu, Boniface Mkwasa, imemuajiri Mbelgiji Luc Eymael kuwa kocha mkuu, huku ikiwa katika mazungumzo na Kocha Mkuu wa Kagera Sugar, Mecky Maxime ikimtaka akawe kocha msaidizi.

Na Simba inanolewa na Mbelgiji mwingine, Sven Vandenbroeck akisaidiwa na Selemani Matola ambaye aliajiriwa baada ya Aussems kutimuliwa. Azam FC, baada ya kuachana na Ndayiragije iliamua kumrejesha aliyekuwa kocha wake wa zamani, Mromania Aristica Cioaba, ambaye ameendelea kusaidiwa na Cheche.

Kwa mtiririko huo, inaonyesha wazi uamuzi wa nani awe kocha msaidizi bado ni jukumu la uongozi wa klabu hizi tatu na kocha mkuu hana nafasi ya kupendekeza nani awe msaidizi wake kama ambavyo tumekuwa tukishuhudia kwa klabu na timu za taifa za wenzetu walioipiga hatua kisoka.

Ikumbukwe Maxime, alianza kuhusishwa na Yanga kabla hata ya Eymael kutua katika klabu hiyo, hivyo, pendekezo hilo ni wazi hayo ni matakwa ya uongozi wa klabu kumwajiri na si chaguo la kocha mkuu kumtaka awe msaidizi wake.

Nipashe tunatambua, uongozi wa klabu hizi tatu, umekuwa msatari wa mbele katika kuajiri makocha na kuwatimua kwa sababu ya kutopata matokeo wanayoyataka, lakini tunashangazwa na namna makocha hao wasivyopewa nafasi ya kufanya maamuzi hayo muhimu kwao. Tunatambua kocha mkuu wa klabu ya soka, ni lazima apendekeze msaidizi wake ambaye anaamini anaweza kufanya naye kazi pamoja wote wakiamini katika falsafa moja ili kutotofautiana katika ufundishaji.

Lakini kwa utaratibu ambao, klabu hizi tatu zinautumia kwa uongozi kuajiri kocha mkuu na kisha kumchagulia msaidizi wake, hakuna ubishi kwamba wanaweza kutofautiana katika falsafa ya ufundishaji, hivyo kocha msaidizi kushindwa kutekeleza majukumu ya bosi wake ipasavyo. Tulishuhudia, Aussems akimkataa msaidizi wake, Masoud kwa kile kilichoelezwa kuwa ni kutofuata maelekezo yake anayompangia jambo ambalo lilizua mvutano mkubwa kabla ya uongozi wa Simba kuamua kuachana na Mrundi huyo na kumuajiri Kitambi.

Kwa mantiki hiyo, tunaona umefika wakati sasa kwa klabu hizo kubadili utaratibu huo kwani tunaamini wapo baadhi ya wasaidizi ambao lengo lao ni kuhakikisha wanawapindua makocha wakuu na wengine wamekuwa vikwazo katika klabu kupiga hatua kimaendeleo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Tamba uone kama hukutamba...



Na Barnabas Maro

**NAAM,** "Tamba uone kama hukutamba huna uonacho." Maana yake zunguka ulimwenguni ujionee mambo usiyoyajua. Hutumiwa kuwahimiza watu wetembee na kujikusanyia maarifa wasiishie kudhani wanayajua yote kumbe hawana wajualo.

Aidha, wahenga walisema: "Gogo la m-buyu si la mvule." Maana yake pande la m-buyu ambao ni mti mnene si sawa na la mvule ambao ni mgumu na hauliwi na mchwa."

Methali hii yaweza kupigiwa mfano wa watu wawili tofauti; mmoja mkubwa, lakini asiyeitumia akili; na mdogo ambaye anaitumia akili yake.

Kabla ya mechi ya Simba na Yanga ambayo sasa yaitwa 'timu ya wananchi', (kwani Simba ni timu ya wakimbizi?) mchezaji Said Ndemla wa Simba alisema siku chache kabla ya mechi hiyo kwamba: "Yanga hawana ubavu wa kupata pointi tatu katika mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara utakaochezwa keshokutwa kwenye Uwanja wa Taifa, Dar es Salaam."

Akihojiwa na moja ya magazeti ya michezo nchini, mchezaji huyo alisema hawakosi usingizi kwa mchezo huo kwani wamejipanga kuondoka na ushindi.

Akaendelea: "Kwa ujumla kila mchezaji wa kikosi chetu hana hofu na Yanga hata kidogo na matumaini yetu ni ushindi. Tunajiandaa kuifunga Yanga kwa mbinu za kocha wetu Mbelgiji, Sven Vandenbroeck," Ndemla alinukuliwa kusema hivyo bila kujua kabumbu mara nyingine huwa mchezo wa bahati.

Haieleweki Ndemla alijisikiaje wakati Simba ikiwa mbele ya Yanga kwa mabao mawili bila; lakini Yanga ikasawazisha yote kipindi cha pili na mchezo kumalizika kwa sare ya 2-2.

Haikuwa mara ya kwanza kwa timu hizo kushangazana. Mara ya kwanza Yanga iliifunga Simba mabao 3-0 ya kipindi cha kwanza, lakini Simba ilirejesha yote kipindi cha pili kuwa 3-3 hata kuufanya uso wa Abdallah Kibadeni aliyekuwa kocha wao ukunjuke baada ya kuwa umetuna kwa wasiwasi!

Mwandishi mwingine wa gazeti ninalolijadili akaandika: "Kwa jeshi hili, wengi watazimia. Kazi ipo Jumamosi kwenye Uwanja wa Taifa, Dar es Salaam kwani benchi la ufundi la Yanga limepanga kufanya 'surprise' ya aina yake kwa kupanga jeshi la mauaji litakaloivaa Simba katika mchezo wa Ligi Kuu Tanzania."

Sikumbuki kusikia kuna watu waliozimia Uwanja wa Taifa wakati na baada ya mechi ya Simba na Yanga. Ingekuwa hivyo baada ya Simba kuongoza kwa mabao mawili mpaka kipindi cha pili. Kwa hiyo mashabiki wa Yanga wangezimia kwa kutoamini macho yao!

Kadhalika, ingekuwa hivyo kwa mashabiki wa Simba baada ya Yanga kusawazisha mabao yote mawili kwa muda mfupi na mchezo kumalizika kwa kufungana 2-2. Pengine mwandishi alipatia alipoandika " ... benchi la ufundi la Yanga limepanga kufanya 'surprise' (mshangao) ya aina yake ..."

Wakati Simba ikiwafunga Yanga mabao mawili, moja katika kila kipindi, Yanga ilifaulu kusawazisha mabao yote mawili kwa muda usiozidi dakika saba kipindi cha pili.

Tumeona au kusikia timu ngumu na maarufu duniani zikifungwa na timu dhaifu na kuwaacha wapenzi wao kwenye mshangao mkubwa. Timu kama Manchester United, Manchester City, Barcelona, Real Madrid n.k. hufungwa na timu zisizotarajiwa na kuwashangaza wengi! Ndio maana husemwa 'mpira hudunda.'

Naye Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba, Senzo Mazingiza, aliwaambia waandishi wa habari siku mbili kabla ya kupambana na Yanga kuwa mchezo huo utatoa sura ya ubingwa kwao kwani watacheza na timu kubwa ambayo ndio wapinzani wao katika mbio za ubingwa.

Akasema: "Mwaka 2020 tunaanza na Yanga. Ni mchezo mgumu, lakini tunahitaji matokeo mazuri ili tuendelee kupambana kutwaa ubingwa wa msimu wa 2019/2020. Tukishinda tutakuwa na asilimia kubwa ya kutwaa kombe."

Kabla ya mechi baina ya Simba na Mtibwa Sugar kugombea Kombe la Mapinduzi kwenye Uwanja wa Amaan mjini Zanzibar, Kocha msaidizi wa Simba, Selemani Matola alisema:

"Tuna historia nzuri ya kupata ushindi tunapokutana na Mtibwa, ni timu yenye ushindani, lakini na sisi tunajipanga kukabiliana nayo na kuishinda. Tutapambana kuhakikisha ubingwa unakuwa wetu, hii itatusaidia pia kwenye ligi kuendeleza moto wa mapambano."

Kichwa cha habari hiyo kiliandikwa: "Matola: Simba ni baba kwa Mtibwa" lakini habari ya paragrafu 10 chini ya kichwa hicho sikusoma popote palipoandikwa Matola kasema 'Simba ni baba kwa Mtibwa!"

Hata hivyo, Mtibwa Sugar ilipopambana na Yanga jijini Dar es Salaam kwenye mechi ya Ligi Kuu, Mtibwa ilicheza soka la kufundishwa wakiambaa uwanja mzima kwa pasi za hapa na pale huku wenzao wakitafuta gozi la ng'ombe kwa 'taa!'

Hakika Mtibwa walikuwa wazuri kimchezo kuliko Yanga hata kuibuka na ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Yanga. Baadhi ya mashabiki wa Yanga wasiokuwa na uvumilivu waliondoka kabla ya mchezo kufikia ukomo huku waliobaki wakijishika matama.

Hii yathibitisha kuwa kila timu iingiapo uwanjani huwa na lengo la ushindi, si kushindwa. Kwa kuwa Ligi Kuu ina timu 20, kila moja inacheza ili kutwaa kombe na kucheza na timu za nje ya nchi.

Pia kila moja inajitahidi kubaki kwenye Ligi Kuu kwani msimu ujao timu zitapunguzwa. Nani asiyetaka kujua nchi mbalimbali za Afrika badala ya kuzisikia tu?

Kabla ya kupambana usitoe maneno ya dharau dhidi ya mwenzako. Ilisemwa "mwenye kelele hana neno." Maana yake aghalabu mtu anayepiga kelele huwa hana madhara yoyote.

Hutumiwa kutukumbusha kuwa hatupaswi kumwogopa mtu mwenye kelele au fujo kwa kuwa kwa kawaida hana neno.

*marobarnabas@yahoo.com*
*0784 334 096*

# Mbaroni tuhuma kuhujumu mizani

**Na Mwandishi Wetu**

WATU 11 wanashikiliwa katika vituo mbalimbali vya polisi kwa mahojiano baada ya kubainika kuhujumu mizani.

Katibu Mkuu Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Elius Mwakalinga, alibainisha hayo jana wakati wa ufunguzi wa mkutano wa baraza la sekta hiyo, uliofanyika mkoani Iringa.

Alisema wizara itaendelea kuchukua hatua kali za kisheria kwa wasafirishaji ambao watakiuka sheria ya uthibiti wa uzito wa magari ya mwaka 2016.

"Toka tuanze mfumo tumeshawakamata watu 11 na bado tunaendelea kufuatilia ili tuwashike zaidi na hatua kali zitachukuliwa ili kukomesha vitendo vya uhujumu katika mizani," alisisitiza Mwakalinga.

Kwa mujibu wa Mwakalinga, hatua hiyo imetokana baada ya sekta hiyo kuanzisha utaratibu wa kufuatilia utendaji kazi wa mizani kwa saa 24 kwa kutumia mfumo wa kielektroniki na kamera za CCTV kwa ajili ya kuongeza uwazi na uwajibikaji na kudhibiti vitendo vya rushwa.

Aidha, alisema serikali imeanza mchakato wa ununuzi wa gari kwa ajili ya mfumo wa kusimamia miundombinu ya barabara kwa ufanisi, weledi na kwa gharama nafuu ikiwa na lengo la kuhakikisha kazi za ukaguzi wa barabara zinafanywa kwa ufanisi.

"Gari hilo litakuwa la kisasa na lenye mionzi itakayowezesha kukagua mtandao wote wa barabara hapa nchini ndani ya mwezi mmoja na kutoa majibu ya ubora na upungufu wa barabara kuanzia hatua za awali za ujenzi hadi mradi utakapokamilika," alisema Katibu Mkuu huyo.

Alibainisha kuwa katika kuhakikisha Tanzania inapata makandarasi wazawa na wenye uwezo wa kujenga na kusimamia miradi mikubwa nchini kwa lengo la kuchangia maendeleo ya Taifa pia sekta hiyo imekwisha peleka wataalamu 33 kwenye miradi mbalimbali nchini, ili kuleta mapinduzi katika sekta ya ujenzi.

Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Ally Hapi, aliipongeza sekta hiyo kwa kuandaa baraza hilo na mikakati mbalimbali ya kimaendeleo ambayo ina lengo la kukuza uchumi wa nchi.

# PAC yazipongeza Ewura, NHC

**Mwandishi Wetu, DODOMA**

MAKAMU Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC), Aeshi Hilal, amezimwagia sifa Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) na Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji (Ewura) kwa ushirikiano mzuri uliowezesha kujengwa jengo la kisasa la makao makuu ya mamlaka hiyo jijini Dodoma.

Aeshi aliyasema hayo juzi wakati kamati yake ilipotembelea jengo la makao makuu ya Ewura linalojengwa na NHC katika eneo la Medeli.

Alisema ushirikiano unaoonyeshwa na mashirika hayo mawili ya serikali katika kufanikisha ujenzi wa jengo hilo si tu unaleta faraja bali unaonyesha ni kwa jinsi gani mashirika hayo yanavyoweza kushirikiana na kufanikisha kazi iliyokusudiwa.

Kutokana na mafanikio hayo, Aeshi alizitaka taasisi za serikali kuiga mfano wa Ewura kwa kuitumia NHC katika kujenga majengo na kubainisha shirika hilo lina sifa na viwango vyote vinavyotakiwa katika ujenzi.

Baadhi ya wajumbe wa PAC, walieleza kuwa wameridhishwa na kasi ya ujenzi wa jengo la Ewura na kuipongeza NHC kwa kasi hiyo na kumaliza ujenzi kwa wakati.

Awali, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Ewura, Nzinyangwa Mchany, alisema mamlaka inatarajia kuhamia kwenye jengo hilo katika mwaka wa fedha ujao, ili kupunguza gharama za kukodi ofisi alizozieleza kuwa huwagharimu zaidi ya Sh. bilioni moja kwa mwaka.

"Tunamshukuru mkandarasi (NHC) kwa kazi nzuri yenye viwango na gharama nafuu," alisema Mchany na kuongeza kuwa jengo hilo litakapokamilika litagharimu zaidi ya Sh. bilioni 10 likiwa na huduma zote muhimu.

NHC kwa sasa imeaminiwa na serikali kwa kupewa miradi mbalimbali kama vile mkandarasi na miradi hiyo inatekelezwa kwenye maeneo mbalimbali nchini ikiwa ni pamoja na majengo ya Halmashauri za Wanging'mbe na Malinyi, miradi 17 ya ofisi za Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Hai na Hospitali ya Rufani Kanda ya Kusini.



Mbunge wa Jimbo la Ubungo, Saed Kubenea, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu kumtambua Isaya Mwita Meya wa Jiji hilo. Kulia ni Diwani wa Tabata, Patrick Asenga na Mwenyekiti wa Madiwani Kanda ya Pwani, Mustafa Muro. **PICHA: MIRAJI**

# Mkandarasi adaiwa kutoweka na mamilioni fedha za barabara

**Na Juster Prudence**

MKANDARASI wa ujenzi wa barabara katika Manispaa ya Morogoro, amedaiwa kukimbia na Sh. milioni 108 za kazi hiyo.

Kutokana na madai hayo, Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, Regina Chonjo, aliagiza Jeshi la Polisi kumsaka mahali popote ili achukuliwe hatua za kisheria.

Chonjo aliyasema hayo jana mjini Morogoro alipotembelea mradi huo kabla ya kikao cha kutoa uamuzi wa kumwondoa mkandarasi huyo.

Aidha, aligiza kufuatwa kwa taratibu za kisheria kukabidhi mradi ukabidhiwe kwa mkandarasi mwingine.

Mradi huo, alisema ulitakiwa kukamilika Januari kesho, lakini mpaka sasa hakuna kilichofanyika kutokana na mkandarasi huyo kwenda kusikojulikana na fedha ambazo zilipangwa kutumika kwa ajili ya mradi.

Meneja wa Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (Tarura) Manispaa ya Morogoro, James Mnene, alisema tangu kuanza kwa mradi ni asilimia 15 tu zilizokamilika.

Aidha, alisema muda uliotumika ni asilimia 96 na kwamba kwa siku mbili zilizobaki hakuna njia inayoweza kutumika kukamilisha mradi huo.

Naye Meya wa Manispaa ya Morogoro, Paschal Kihanga, alisema wana mpango wa kutafuta mkandarasi mwingine ambaye ataweza kuendana na muda uliopangwa na kuongeza kuwa fedha walizonazo kama manispaa haziwezi kukamilisha ujenzi wa mradi huo.


**MAJEMBE AUCTION MART LTD (VIJANA WA KAZI)**

215586002

**MNADA WA HADHARA**

KWA NIABA YA SHIRIKA LA NYUMBA LA TAIFA (NHC) S.L.P 391 DODOMA TUTAUZA MALI ZA WADAIWA ZILIZOCHUKULIWA WAKATI WANAONDOLEWA KWENYE MAJENGO YA SHIRIKA LA NYUMBA BAADA YA KUSHINDWA KULIPA KODI YA PANGO.

MNADA UTAFANYIKA SIKU YA IJUMAA TAREHE 31/1/2020 SAA 5.00 ASUBUHI KWENYE ENEO LA CCM MKOA KARIBU NA SHULE YA SEKONDARI VIWANDANI.

| NA. | JINA LA MDAIWA | AINA YA MALI |
|---|---|---|
| 1. | GEOFREY A. MKOLONGO | SOFA, FRIDGE, MEZA, KITANDA, GODORO, DISH |
| 2. | LUCY MICHAEL MWITA | KOCHI ZA MBAO, KING'AMUZI, VITANDA/GODORO, TV, KABATI ZA MBAO |
| 3. | CHRISTOPHER MKANDE | TV, DECL, FRIDGE, TV, MITO YA MAKOCHI NA KADHALIKA |

**MASHARTI YA MNADA:**
MALIPO NI TASLIMU NA MALI ITAONDOLEWA SIKU HIYO HIYO. KWA MAELEZO ZAIDI WASILIANA NASI KWA NAMBA **0754 301930, 0715 868000, NA 0752 959595, 0715 311057, 0783 533819**

## Wafanyabiashara wapaza sauti usajili laini za simu

INATOKA UK 2

Alisema watu ambao wamejiandikisha tangu mwaka juzi na mwaka jana wengi wameshapewa namba zao za vitambulisho isipokuwa kuna baadhi ya watu ambao wana siku moja au mbili.

Ofisa huyo alisema mfumo wa kupata namba unachukua kuanzia muda wa wiki mbili, na kubainisha itakuwa ngumu kwao kupata namba kwa siku hizo mbili zilizosalia.

Awali, TCRA ilitangaza kuwa mwisho wa usajili ungekuwa Desemba 31, mwaka jana, lakini Rais aliongeza hadi Januari 20, mwaka huu.

**HALI DODOMA**

Jijini Dodoma, watu wengi wamejikuta kwenye foleni muda mrefu kusubiri kupata namba za vitambulisho.

Nipashe ilitembelea Ofisi za Nida jijini humo kuona uandikishaji unavyoendelea na kukuta foleni ndefu zisizoisha za watu wakisubiri huduma hiyo.

Mmoja wa wakazi wa jijini humo, Juma Adamu, alisema ana siku tatu ambazo amekuwa akifika kila siku akipanga foleni kutafuta huduma ya kitambulisho hicho bila mafanikio.

"Ni kweli tulichelewa kupata vitambulisho hivi kwa sababu kubwa moja ni utaratibu wa kushinda siku nzima bila kukamilika, tumekuwa tukifika kwenye kituo hiki kutafuta vitambulisho, lakini hatufanikiwi mpaka laini zetu zitafungiwa," alisema.

Adamu aliyataja maeneo yenye usumbufu mkubwa kuwa ni Nida kwa sababu ya uchukuaji wa taarifa na upigaji picha unachukua muda mrefu kumhudumia mtu mmoja.

Nipashe ilishuhudia wananchi wakiwa kwenye foleni ya mistari mirefu katika kituo cha kuandikisha cha Nyerere Square, ofisi za Nida zilizopo jengo la bima jijini hapo.

***Imeandikwa na Marco Maduhu, SHINYANGA na Ibrahim Joseph, DODOMA***



## Maalim Seif, Bimani waachiwa kwa dhamana

**Na Mwandishi Wetu**

MSHAURI Mkuu wa Chama cha ACT-Wazalendo, Maalim Seif Sharif Hamad na Mwenyekiti wa Kamati wa Itikadi, Uenezi na Mawasiliano ya Umma, Salim Bimani, wameachiwa kwa dhamana.

Viongozi hao waliitikia wito wa Mkuu wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai mkoa wa Kaskazini Pemba.

Aidha, baada ya kuachiwa kwa dhamana Maalim Seif alipokewa na mamia ya wanachama na wananchi waliokuwa nje ya kituo cha polisi wakati akifanyiwa mahojiano.

Viongozi hao walitakiwa kuripoti polisi kwa madai ya kufanya mkutano bila kibali cha polisi Desemba 9, mwaka jana katika Jimbo la Micheweni mkoani humo.

Kwa mujibu wa taarifa ya ACT-Wazalendo, iliyotolewa na Katibu wa Itikadi, Uenezi na Mawasiliano na Umma, Ado Shaibu, viongozi hao hawakufanya mkutano wa hadhara bali kikao cha ndani kupitia ziara ya kukusanya maoni ya wananchi kwa ajili ya kuandaa ilani ya uchaguzi mkuu 2020.

Aidha, aliliasa jeshi hilo kuacha kutumika kisiasa kutokana na bugudha za mara kwa mara wanazopata wanapofanya vikao vya ndani na mikutano.

Alisema wakati wao wakizuiwa na kubughudhiwa vijana wa CCM waliruhusiwa kufanya maandamano ikiwamo kushusha bendera za matawi la ACT-Wazalendo bila kuchukuliwa hatua zozote.

"Tunalikumbusha Jeshi la Polisi kuwa shughuli za vyama vya siasa zipo kwa mujibu wa sheria. Ni muhimu wajiendeshe kwa weledi na haki badala ya kutumika kisiasa kuhujumu shughuli za vyama vya upinzani na kubariki shughuli za CCM pekee," alisema.

## Mshtakiwa mauaji aangua kilio kortini

INATOKA UK 4

**Hakimu:** Washtakiwa wanalalamika wananyimwa chakula. Ni kweli?

**Inspekta Shabani:** Mheshimiwa Hakimu sina taarifa.

**Hakimu:** Unaweza kueleza?

Inspekta Shabani: Kwa kifupi najua mahabusi wote wanapata chakula. Sina taarifa nyingine mheshimiwa Hakimu.

Hata hivyo, mshtakiwa wa 13, Ayubu Selemani aliomba kuzungumza na aliporuhusiwa alidai kuwa wao ni wa mahabusu ya Keko na kwamba wako raia wa kigeni wengi kutoka mataifa mbalimbali.

"Siku tano zilizopita washtakiwa hawa wenzetu katika kesi hii, raia wa Burundi waliitwa na ofisa usalama wa Magereza na kuwaeleza kwamba kuanzia sasa hawatapewa chakula kama raia wa kigeni kitu ambacho wengine wanaendelea kupata huduma hiyo. Wapo Wapakistani, Wacongo na wa Kenya, kwa nini hawa wawakatie huduma?" Alidai Selemani.

Hakimu alisema anaiahirisha kesi hiyo kwa siku saba badala ya 14, kwa ajili ya kupata taarifa kamili kuhusu malalamiko ya washtakiwa.

Alisema kesi hiyo itatajwa Januari 24, mwaka huu na washtakiwa wapelekwe mahabusu.

Mbali na Mchungaji (40), Nyandwi na Selemani, washtakiwa wengine ni, Godfrey Salamba (42) mkazi wa Kinondoni Msisiri A, Inocent Kimaro (23) mkazi wa Temeke Mikoroshini, Chambie Ally (32) mkazi wa Kia/Boma na Ofisa wa NBC, Robert Mwaipyana (31).

Wengine ni Meneja wa Benki ya Backlays, Khalid Mwinyi (33) mkazi wa Mikocheni B, Rahma Almas (37) mkazi wa Mbagala na Mohammed Maganga (61) mchimba makaburi (alifariki dunia mwaka jana). Allan Mafue, Ismail Mohammed, Leornad Makoye, Amino Sham, Ayoub Selemani, Joseph Lukoa, Gaudence Matemu na Abuu Mkingie,

Katika shtaka la kwanza, washtakiwa kwa pamoja wanadaiwa kuwa kati ya Julai Mosi na Agosti 16, 2017 walikula njama ya kufanya mauaji ya Lotter.

Katika shtaka la pili, washtakiwa hao wanadaiwa Agosti 16, 2017 katika makutano ya barabara za Chole na Haile Selasie iliyopo Wilaya ya Kinondoni Dar es Salaam, wanadaiwa kumuua Lotter.



Mwenyekiti wa Shirikisho la Wakuu wa Polisi Ukanda wa Mashariki mwa Afrika (EAPCCO), IGP Simon Sirro, akikabidhi zawadi kwa kiongozi wa ujumbe kutoka Umoja wa Nchi za Ulaya, Ignasi Mundane, baada ya kufanya mazungumzo, jijini Dodoma jana, kuhusu mradi wanaoufadhili wa mafunzo ya kuwajengea uwezo wasimamizi wa sheria katika nchi zilizopo pembe ya Afrika, hususani kwenye masuala ya upelelezi. **PICHA: JESHI LA POLISI**

## Lukuvi aibua tuhuma uuzwaji nyumba NHC

INATOKA UK 3

hapa ofisi ya DCI ili niwakabidhi hii nyumba kwa sababu jambo hili nililibaini miezi miwili iliyopita na nikawakabidhi NHC lakini hadi leo hawajatoa taarifa hata polisi, wao peke yao hawawezi kuchunguza.

"Jambo hili hawawezi kuchunguza kwa sababu linawahusu wao na siyo uongozi wa sasa, lakini siku za nyuma lazima wanajua kilichotokea, sasa Jeshi la Polisi litatusaidia mali hii kurudi serikalini.

"Na wote waliohusika kutoka ofisi za wanasheria wa nje ambao kwenye mikataba nimewaona na wengine baadaye wakaja kuwa viongozi waliohusika hata ubadilishaji wa nyaraka ofisini kwangu, wale walioandika barua za kuhamisha na kumtambulisha sasa hii nyumba ni mali yako waliopo ofisi yangu na NHC tutapata taarifa," alisema.

Lukuvi alisema alitarajia tangu alivyokabidhi suala hilo kwa NHC, wangekuwa wamelikabidhi kwa DCI lakini hawajafanya hivyo.

Kuhusu nyumba ya NIC iliyopo Kitalu 459 mtaa wa Charambe, Upanga jijini Dar es Salaam, Lukuvi aliagiza uchunguzi wake ulenge kuangalia kwa nini licha ya kuwa na zuio la mahakama iliuzwa.

HABARI ARUSHA

# Apongeza wadau kumuenzi Gambo

**Na Cynthia Mwilolezi, ARUSHA**

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako, amewapongeza wadau wa elimu mkoani Arusha kumuenzi Mkuu wa Mkoa huo, Mrisho Gambo, kwa kuipa jina lake shule ya sekondari mpya ya mchepuo wa sayansi aliyoifungua juzi katika Kata ya Olasiti.

Akitoa pongezi hizo juzi wakati wa kuweka jiwe la msingi katika shule hiyo, Prof. Ndalichako alisema mkoa wa Arusha umepata mkuu wa mkoa jembe anayependa maendeleo hasa katika nyanja ya elimu.

"Wewe Gambo ni jembe pamoja na kuwa ni kijana. Unafanya mambo makubwa hasa katika elimu ambayo katika mkoa wako shule nyingi zinafanya vizuri," alisema.

Prof. Ndalichako alisema ni wazo zuri la uanzishwaji wa shule hiyo mkoani humo hasa ya mchepuo wa sayansi ambayo itazalisha wataalamu wanaohitajika katika nyanja mbalimbali kwa sasa.

"Lakini shule hii kwa kuwa inamiundombinu mizuri na maabara za kutosha za masomo ya Baiolojia na Kemia mbele na baadaye itaongezwa na kuwa hadi kidato cha tano na sita ili watoto wapate fursa ya kuendelea na masomo yao ngazi hiyo, baada ya kumaliza kidato cha nne," alisema.

Kwa upande wake, Gambo alishukuru kwa pongezi hizo na kuahidi kuisimamia shule hiyo ili iwe mfano.

"Lakini pongezi hizi zilizotolewa kwangu si zangu peke yangu kwani kazi hii imefanywa na viongozi wote wa Kata ya Olasiti na Jiji la Arusha ambao ni wasaidizi wangu na mimi mtendaji mkuu," alisema.

Gambo alisema ameamua kuwekeza katika elimu ili kusaidia watoto wa familia maskini kupata elimu bure ya serikali inayotolewa sasa.

"Mimi ni zao la familia maskini nilisoma kwa fedha za mauzo ya uji na nilisoma masomo ya sayansi, sasa na mimi naona njia pekee ya kusaidia wenzangu walio katika familiya kama yangu ni kujenga shule ya sayansi yenye miundombinu imara ya kupata elimu hiyo," alisema.

Kwa mujibu wa Gambo, kuiendeleza shule hiyo kuwa hadi kidato cha sita watasaidiana na Jiji hilo pamoja na wadau wengine kutafuta eneo la ujenzi wa madarasa hayo.

**"Lakini pongezi hizi zilizotolewa kwangu si zangu peke yangu kwani kazi hii imefanywa na viongozi wote wa Kata ya Olasiti na Jiji la Arusha ambao ni wasaidizi wangu na mimi mtendaji mkuu," alisema.**

# Butiku aeleza gharama upatikanaji haki, uhuru

**Na Allan Isack, ARUSHA**

MKURUGENZI Mtendaji wa Taasisi ya Mwalimu Nyerere (MNF), Joseph Butiku, amesema haki, demokrasia na uhuru wa vyombo vya habari nchini, haipatikani kirahisi bali inatafutwa kwa gharama kubwa.

Hayo aliyasema jana jijini Arusha, wakati wa hafla fupi ya ujenzi wa nchi ya amani kuelekea uchaguzi mkuu Oktoba, mwaka huu, iliyofanyika katika ukumbi wa Mkuu wa Mkoa Arusha.

Hafla hiyo iliwakutanisha waandishi wa habari na wadau wa vyombo vya habari mkoani hapa.

Kutokana na hali hiyo, Butiku aliwataka waandishi wa habari nchini kuendelea kutafuta haki zao, kwa kufanya mazungumzo ambayo yanatakiwa kuwa na busara na unyenyekevu kwa pande zote.

"Haki siku zote haipatikani kirahisi bali hupatikana kwa njia ya mazungumzo yenye busara, hekima na kusikilizana. Naomba mjaribu kuzungumza kwa maelewano kwa pande zote mbili," alisema Butiku.

Hata hivyo, aliwataka waandishi wa habari kutokukata tamaa katika harakati za kupigania haki zao na uhuru wa vyombo vya habari.

"Msife moyo na msichoke kutafuta haki kwa kuwa haki haifi bali inachelewa tu, lakini sisi binadamu tunakufa," alisema na kuongeza:

"Nina miaka 81 kama nikifa nitasikitika sana kusikia kuwa mmekata tamaa na mmeshindwa kupigania haki zenu."

Aidha, alisema binadamu wote ni sawa, hivyo kila mtu anastahili kuheshimiwa na kupewa haki yake na asili ya uongozi ni watu na haki.



Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Mrisho Gambo (kulia), akiwa na Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako (wa pili kulia), wakishuhudia wakati Balozi wa China hapa nchini, Wang Ke, akizindua Shule mpya ya Sekondari ya Mrisho Gambo ya mchepuo wa Kiingereza, katika Kata ya Olasiti, jijini Arusha juzi. **PICHA: CYNTHIA MWILOLEZI**

# Watakaotafuna fedha za ushirika kukiona

**Na Jaliwason Jasson, BABATI**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) mkoani Manyara, imeapa kuwashughulikia watu wote watakaobainika kutafuna fedha za vyama vya ushirika.

Mkuu wa Takukuru mkoani hapa, Fidelis Kalungula, alisema juzi wakati akitoa taarifa kwa waandishi wa habari juu ya utekelezaji kazi ya mkoa kwa kipindi cha miezi mitatu kuanzia Oktoba hadi Desemba, mwaka jana.

"Tutaendelea kufuatilia vyama vya ushirika na waliohujumu tutahakikisha mali zilizohujumiwa zinarejeshwa na waliohujumu kufilisiwa," alisema Kalungula.

Aidha, alisema watachambua taarifa za ukaguzi wa hesabu ili kuona kila chama chenye udhaifu na kuufanyia kazi.

Kalungula alisema watachambua kila chama ikiwamo kurejesha fedha na kuwafikisha mahakamani wahusika.

"Kwa kipindi cha miezi mitatu iliyopita Takukuru tulipokea malalamiko tisa juu ya vyama vya ushirika, hivyo inaonyesha katika vyama hivi kumekithiri ubadhirifu," alisema.

Alisema baada ya kupokea taarifa hizo, walifanya uchunguzi na kuokoa Sh. milioni 13.4 na kati ya hizo Sh. milioni 5 ziliokolewa na kurejeshwa katika akaunti ya Chama Kikuu cha Ushirika (Rivacu).

Kwa mujibu wa Fidelis, katika kuhakikisha vyama vya ushirika vinakuwa kwenye mstari miezi mitatu ijayo watayafanyia kazi malalamiko yote na kuwachukulia hatua wanaovihujumu vyama hivyo.

Mkuu wa Dawati la Elimu kwa Umma, Sultan Ng'alanzi, aliwatahadharisha wenye tuhuma kwenye vyama hivyo kuwa makini na baadhi ya watu wanaowalaghai kuwapa msaada wa kumaliza kesi zao.

"Watu hao wanajiita maofisa wa Takukuru na kuwataka wakutane nao ili wawasaidie, msikubali kurubuniwa na muwaulize kama wana vitambulisho na mvione, lakini mkiwaona mje ofisi za Takukuru kutoa taarifa zao," alisema.

# Norway yaipa tano serikali mikakati ya kuinua uchumi

**Na Godfrey Mushi, HAI**

MKURUGENZI Mkazi wa Shirika la Misaada la Makanisa ya Norway (NCA), Gwen Bwerge, amesema nchi yake inaunga mkono juhudi za Serikali ya Tanzania katika kupigania maendeleo ya wananchi wake na hatua inazochukua kuinua uchumi.

Amesema nishati jadidifu ni dawa ya mabadiliko ya tabianchi na Watanzania wataendelea kuona umuhimu wa kutumia umeme unaotokana na nishati hiyo hasa maeneo ya vijijini.

Bwerge aliyasema hayo juzi alipozungumza na Nipashe kuhusu uwekezaji wa Serikali ya Tanzania katika kituo kipya cha mafunzo ya utafiti juu ya nishati jadidifu cha Kikuletwa kilichoko wilayani Hai.

"Tanzania inafanya vizuri zaidi katika sekta mbalimbali kwa sasa, nimefurahi kusikia kwamba inazindua kituo cha mafunzo ya utafiti juu ya nishati jadidifu.

"Ni hatua nzuri na sisi wadau wa maendeleo tunaiunga mkono kwa sababu ni moja ya njia za kuhamasisha matumizi ya nishati hiyo muhimu kwa sasa ulimwenguni," alisifu.

Jana, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako, alizindua rasmi kituo hicho cha utafiti wa nishati jadidifu ambayo huzalishwa na vyanzo asili kama jua, maji, upepo, mvua, mawimbi na jotoridi.

Kituo hicho cha mafunzo na utafiti juu ya nishati jadidifu (renewable energy) cha Kikuletwa ni sehemu ya Chuo cha Ufundi Arusha (ATC).

Kituo cha mafunzo na utafiti juu ya nishati jadidifu cha Kikuletwa kimeanzishwa kwa lengo kutoa mafunzo na utafiti katika nyanja za nishati jadidifu.

Kaimu Mkuu wa Chuo cha Ufundi Arusha, Dk. Masudi Senzia, akizungumzia kituo hicho, alisema mafunzo yatakayotolewa katika Kampasi ya Kikuletwa ni pamoja na uzalishaji wa umeme kwa nguvu za maji, upepo, jua na nishati itokanayo na viumbe hai (biomass).

**"Ni hatua nzuri na sisi wadau wa maendeleo tunaiunga mkono kwa sababu ni moja ya njia za kuhamasisha matumizi ya nishati hiyo muhimu kwa sasa ulimwenguni," alisifu.**

# RC akosoa mikataba inayozuia watoto kufanya kazi mikono

**Na Godfrey Mushi, MOSHI**

MKUU wa Mkoa wa Kilimanjaro, Dk. Anna Mghwira, amekosoa mikataba inayozuia watoto kufundishwa kazi za mikono na haki hiyo kutafsiriwa vibaya kwamba ni 'ajira za watoto', akieleza kuwa ni fikra hasi inayojengwa katika jamii.

Amesema kupinga ajira kwa watoto ni kutomfundisha mtoto kufanya kazi, jambo ambalo ni fikra potofu inayopaswa kukemewa isiote mizizi zaidi.

Dk. Mghwira aliyasema hayo wakati akizungumza na wakuu wa shule na maofisa elimu ngazi ya kata wilayani Moshi waliokuwa katika mafunzo maalum ya kimkakati.

"Kumejengeka fikra hasi katika jamii, kupinga ajira kwa watoto ni kutomfundisha mtoto kufanya kazi, jambo hili ni fikra potofu kabisa. Mtoto anaweza kupewa kazi kwa mujibu wa umri wake kama sehemu ya malezi ili awe na fikra za kujitegemea katika maisha yake.

"Hebu tusaidieni sasa kutoa elimu ya maarifa itakayowasaidia wanafunzi kuwa na uwezo wa kufanya kazi za mikono. Walimu hakikisheni kwamba elimu mnayoitoa kwa watoto isiwe ya darasani pekee, bali toeni mafunzo ya vitendo ambayo yatahusu stadi za kazi," aliagiza.

Alisema mfano mzuri wa kumfunda mtoto kufanya kazi za mikono ni pamoja na shughuli za utunzaji wa mazingira.

"Si makosa kumfundisha mtoto kupanda na kutunza miti ya matunda, kwa sababu faida ya kufanya hivyo ataiona mapema akiwa shuleni.

"Huyu atanufaika kwa kivuli na matunda na hatimaye atakapohitimu masomo yake, atakuwa ameshanufaika na elimu hiyo kwa vitendo," alifafanua.

Mkuu wa Mkoa huyo alisema umuhimu wa utoaji elimu ya kumjengea mtoto fikra na uwezo wa kujitegemea uliasisiwa na Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere, ili kujenga taifa lenye watu wasio na fikra za utegemezi.

"Wakati tulipokuwa watoto, Mwalimu Nyerere alikuwa akituhimiza kuotesha miti hata katika maeneo haya ambayo mnapanda maua," alisema.

Awali, akitoa taarifa ya mafunzo hayo kwa Dk. Mghwira, Katibu Tawala Msaidizi, Sekretarieti ya Mkoa wa Kilimanjaro, anayesimamia elimu, Paulina Mkwama, alisema mafunzo hayo ya kimkakati kwa ajili ya kujiimarisha katika ufaulu, yanahusisha walimu 460 na maofisa elimu kata 168 na wakuu wa shule 338.



Mwakilishi wa Balozi wa Norway hapa nchini, Britt Hilde Kjolas, akizungumzia ushirikiano wa nchi yake na Tanzania, kwenye maadhimisho ya Miaka 64 ya Hospitali ya Rufani ya Haydom, mkoani Manyara juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Wanufaika wa mikopo ya halmashauri wapewa neno

**Na Godfrey Mushi, ROMBO**

WANUFAIKA wa mikopo isiyo na riba inayotolewa na Halmashauri ya Wilaya ya Rombo mkoani Kilimanjaro, wametakiwa 'kujiongeza' katika uwekezaji wa kibiashara na kufikiria wazo la kuanzisha viwanda vidogo.

Mkuu wa Wilaya hiyo, Agness Hokororo, alitoa somo hilo jana kwa makundi maalum yanayonufaika na asilimia 10 ya fedha za mapato ya ndani zinazotengwa kwa ajili ya uwezeshaji kiuchumi makundi ya wanawake, vijana na walemavu.

"Inabidi mjifunze sana kutunza akiba zenu, kwa sababu zitawasaidia kufanya uzalishaji mkubwa zaidi; na kwa kweli nia njema ya serikali ni kutaka kuona wananchi wake wanainuka kiuchumi na kutoka hapo walipo," alisema.

Ili kufikia malengo ya kuanzisha viwanda vidogo kutokana na mikopo hiyo, Hokororo aliyataka makundi hayo maalum kujiepusha na biashara za magendo.

Alisisitiza kuwa iwapo vikundi hivyo vitajihusisha na biashara za magendo, serikali itawakamata na fedha yote ya kikundi itapotea na hivyo watapata hasara na kushindwa kufanya marejesho, jambo ambalo litaisukuma halmashauri kuwashtaki mahakamani.

Kabla ya makabidhiano ya fedha hizo kiasi cha Sh. milioni 61.5 zilizotolewa kwa vikundi 20 vya wanawake, vijana na walemavu, Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Wilaya hiyo, Patricia Kinyange, alisema walionufaika ni vikundi 12 vya wanawake, saba za vijana na kimoja cha watu wenye ulemavu.

Kwa mujibu wa ofisa huyo, vikundi vilivyokuwa vimeomba mkopo huo vilikuwa 55 vilivyohitaji Sh. milioni 275, lakini kutokana na mapato madogo ya halmashauri, kamati ilikaa na kuchuja na kila kata ilipata kikundi kimoja.

Fedha hizo zilizotolewa na serikali ni kwa ajili ya kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2019/2020.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Rombo, Godwin Chacha, akizungumza katika hafla hiyo alisema: "Natamani vikundi hivi viendelee kiuchumi na baadaye hata kuungana na kuwa na mtaji mkubwa zaidi ili kuanzisha viwanda vitakavyokuwa vinatengeneza bidhaa zilizoongezwa thamani na bidhaa za uzalishaji ambazo zitakuwa zinatoka Rombo."

Kabla ya kupewa mikopo hiyo, vikundi hivyo vilipata mafunzo ya siku mbili juu ya uandaaji wa vitabu vya fedha vinavyotunza kumbukumbu, elimu ya ujasiriamali, usimamizi wa akaunti, hatua za kuchukua kabla ya kuchukua mkopo, namna ya kufanya marejesho na jinsi ya kujisajili katika Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA).

HABARI DODOMA

## Watakiwa kutoa maoni kuboresha sera ya wazee

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

SERIKALI imewataka wadau wa utoaji huduma kwa wazee kutoa maoni ya kuboresha Sera ya Taifa ya Wazee ya mwaka 2003 ili kukidhi mahitaji ya wazee kwa sasa.

Wito huo ulitolewa juzi na Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. John Jingu, alipokuwa akifungua kikao cha wadau kilichokuwa kikilenga kuhuisha Sera ya Taifa ya Wazee ya mwaka 2003, jijini hapa.

Dk. Jingu alisema wameandaa rasimu ya awali ya sera hiyo ambayo itatumika kuchochea fikra za wadau ili kupata maoni chanya yatakayojumuishwa katika sera iliyoboreshwa kwa kuwa itazingatia mazingira halisi ya afya, ulinzi, usalama, hifadhi ya kijamii, matunzo na ushirikishwaji katika masuala ya kijamii.

Alibainisha kuwa serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuhudumia wazee ikiwa ni pamoja na kusimamia makao ya wazee 17 ya yanayomilikiwa na hivi sasa yamepunguzwa manne na kubaki 13 kwa ajili ya kuboresha huduma kwa wazee wasiojiweza wanaoishi katika makazi hayo.

"Serikali inachukua jukumu la kuwalea wazee baada ya kuthibitika kuwa familia husika haina uwezo au haikujitokeza kutoa huduma," alisisitiza.

Kadhalika, alisema mpango wa utambuzi wa wazee katika halmashauri hadi kufikia Desemba, 2019 wazee 1,837,162 wametambuliwa, kati yao wasio na uwezo 684,383 wamepatiwa vitambulisho vya matibabu bila malipo.

Naye Kamishna wa Ustawi wa Jamii, Dk. Naftali Ng'ondi, alisema kuna umuhimu kuboresha sera ya wazee ili kuakisi mahitaji na kero zinazowakabili wazee.

**"Serikali inachukua jukumu la kuwalea wazee baada ya kuthibitika kuwa familia husika haina uwezo au haikujitokeza kutoa huduma," alisisitiza.**

# Kamati ya Bunge yatoa neno kilimo hifadhi

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

KAMATI ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, imeishauri serikali kuweka kipaumbele kwenye kilimo hifadhi kisera na kisheria ili kulinda ardhi na kuwa na kilimo chenye tija.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Mahamoud Mgimwa, alisema hayo jana katika kikao cha kamati na wadau wa kilimo kilichohusu mipango na mikakati ya kuendeleza kilimo hifadhi na matumizi ya zana bora za kilimo katika kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi.

Katika kikao hicho, kamati hiyo ilikutana na Shirika la Kilimo Hifadhi Tanzania (CFU) na Mtandao wa Kilimo Hifadhi Barani Afrika (ACTN), ambao wanashauri wakulima kutumia mbinu stahiki za kilimo hifadhi na matumizi sahihi ya pembejeo.

Mgimwa pia alitaka kujua namna serikali ilivyowekeza katika kilimo hifadhi.

"Kilimo hifadhi kina tija na si ndogo kwanza mkulima anapata mazao ya kutosha lakini pia kubana matumizi kwa kuwa matumizi ya mbolea hayatakuwapo kwa kiasi kikubwa, kwa hiyo kuna tija na hata vyakula vitakavyopatikana vitakuwa vya asili," alisema.

Alieleza hali hiyo itamwezesha mkulima kuuza mazao yake bila kikwazo chochote.

"Kamati itahakikisha serikali wanalipa uzito suala la kilimo hifadhi kwa kuweka sera na sheria, hatuna sababu ya kulikwepa tuliweke watu walijadili," alisema.

Akichangia katika kikao hicho, Mbunge wa Hanang, Mary Nagu, alisema kilimo ndiyo sekta itakayowainua wakulima na awali wakulima wa jimbo lake waliamini kuhusu kilimo hifadhi lakini baadaye walihamasishwa kutumia mbolea za kisasa, hivyo wataalam wana wajibu wa kutoa elimu kwa kina kuhusu hilo.

"Tutawatoaje kwenye matumizi ya mbolea ya kisasa, ili waendelee kuwa na imani, kama mliwaambia mbolea ya kisasa ikitumika kwa muda mrefu inaharibu ardhi kabisa, leo tunawezaje kurudisha hili la kilimo hifadhi kwa wakulima ambapo awali walikuwa wanaamini," alisema.

Nagu alisema suala la kilimo hicho linapaswa kuwa endelevu ili kuwasaidia wakulima na kuwataka wataalamu watoe elimu ya kutosha ili kunusuru ardhi ya Tanzania.

Naye Mbunge wa Musoma Vijijini, Prof. Sospeter Muhongo, alisema uharibifu mkubwa wa ardhi unafanywa na mbolea na mwamko wa kutumia mbolea ni mkubwa na kuwaomba wataalam kutoa elimu namna ya kurutubisha ardhi kupitia kilimo hicho.

Mbunge wa Singida Kaskazini, Justine Monko, alisema wataalamu wanashauri mahindi yalimwe na maharage yasiyoliwa ili kuchangia ardhi kupata rutuba lakini elimu zaidi inahitajika kwa wakulima imekuwa ni vigumu kuweka mchanganyiko huo.

Awali, akiwasilisha kwa kamati mada ya uzoefu wa kilimo hifadhi barani Afrika, Mtendaji Mkuu wa ACTN), Mhandisi Saidi Mkomwa, alisema kuna haja ya kubadili kilimo cha sasa kuwa kilimo hifadhi yatakayoendana na matumizi sahihi ya zana za kilimo.

Alisema kuna tatizo kubwa la kilimo cha Tanzania kuchakaza udongo na hivyo kuna haja ya kulinda mazingira kwa manufaa ya taifa na vizazi vijavyo.

Alibainisha kuwa kuna fursa nyingi zinazojitokeza kwa Tanzania kutokana na mabadiliko yaliyoanza kujitokeza ikiwamo watanzania wengi kuhamia mijini na kwamba ifikapo mwaka 2030 kutakuwa na watu milioni 35 mijini ambao watategemea kununua chakula.



Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji, Mitaji ya Umma (PIC), Dk. Raphael Chegeni (kulia), akiongoza kikao cha kamati hiyo, walipokutana Bungeni, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Operesheni maalum maeneo machafu yaja

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

SERIKALI imeiagiza kuendesha operesheni maalum za ukaguzi wa sehemu za kuuzia chakula, nyumba za kulala wageni, mabucha, masoko kwa mikoa yote nchini ili kudhibiti uchafu wa mazingira kwenye maeneo hayo.

Agizo hilo lilitolewa jana jijini hapa na Mkurugenzi wa Huduma za Kinga, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Leonard Subi, alipokuwa akizungumzia uboreshaji hali ya usafi wa mazingira nchini.

Dk. Subi alisema huo ufanyike kwa kuzingatia sheria ya afya ya jamii ya mwaka 2009 ili hatua stahiki zichukuliwe kwa wanaokiuka sheria hiyo.

Mkurugenzi huyo alisema maofisa afya nchini wana wajibu wa kusimamia, kuratibu na kutekeleza mikakati yote ya uboreshaji usafi wa miji na usalama wa maji na chakula.

"Pia naagiza vyombo vya usafiri (mabasi, meli, majahazi, bajaji) vikaguliwe ili kubaini uzingatiaji wa usafi wa vyombo hivyo na upuliziaji dawa ya kuua wadudu ufanyike na cheti maalum cha kuthibitisha kitolewe," alisema.

Hata hivyo, alisema vyombo ambavyo vitabainika kuwa na uchafu uliokithiri viruhusiwe kutoa huduma na vitozwe faini kwa mujibu wa sheria hiyo.

"Ukaguzi pia ufanyike kaya kwa kaya maeneo yote nchini na hatua stahiki zichukuliwe kwa watakaobainika kwenda kinyume cha kanuni za afya ikiwemo matumizi ya vyoo bora, udhibiti wa taka ngumu, majitaka na usafi wa mazingira wanayoishi kwa ujumla," alisisitiza.

Pamoja na hayo, aliagiza kufanyika ukaguzi maalum katika taasisi zote za umma na binafsi na zitakazobainika kutozingatia usafi zichukuliwe hatua kali za kisheria.

"Kuna tabia ya kutiririsha majitaka imekuwa sugu katika baadhi ya maeneo hapa nchini hususan Jiji la Dar es Salaam ambapo kila kona ya jiji kuna harufu mbaya ambayo ni kero kwa wakazi, viongozi wa mitaa wanawajibu wa kusimamia usafi wa kuondokana na tatizo hili," alisema.

Alizitaka halmashauri kuongeza mikakati zaidi na ufuatiliaji wa magonjwa yanayoenezwa kwa njia ya chakula.

# Hospitali zafungiwa huduma ya mionzi

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

VITUO viwili vya afya vinavyotumia vifaa vya mionzi katika kutoa huduma za afya Zanzibar vimefungiwa kutoa huduma hiyo kutokana na kutokidhi matakwa ya kisheria na kiusalama.

Hayo yalielezwa jana na mtafiti mwandamizi wa Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania, Dk. Suleima Amour Suleiman, wakati akizungumza na waandishi wa habari katika maonyesho ya biashara ya Miaka 56 ya Mapinduzi katika viwanja vya Maisara mjini hapa.

Alisema Desemba, mwaka jana, tume hiyo imekagua vituo 23 vya afya ambavyo vinatoa huduma za mionzi na vituo 21 vimekidhi matakwa ya kiusalama ya utoaji wa huduma hiyo na vituo viwili havikukidhi matakwa ya kiusalama na kuvifungia.

Dk. Suleiman alisema vituo hivyo vilivyofungiwa ni Hospitali ya Wete Pemba ambayo inamilikiwa na Wizara ya Afya Zanzibar na Alkhamis Camp inayomilikiwa na Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) iliyoko Chakechake, Pemba.

Alisema hospitali hizo vifaa tiba vyake vilikuwa vikivujisha mionzi jambo ambalo ni hatari kwa afya za wananchi wanaokwenda kupata huduma katika hospitali hizo.

Naye Mkuu wa Mawasiliano wa Tume hiyo, Peter Ngamilo, alisema athari ambazo zinaweza kupatikana ambapo mgonjwa atapigwa mionzi ambayo haijakidhi vigezo ni kupata majeraha makubwa na kusababisha kifo. Pia alisema mionzi huharibu mfumo wa mwili na kupata saratani.

Alisema serikali katika kuhakikisha inajali wananchi wake, imeanzisha tume hiyo ili kuwalinda wananchi wasipate madhara yanayosababishwa na mionzi.

"Mionzi haina mipaka, utaigundua kwa vifaa maalum na serikali imewekeza kweli kweli katika hili ndiyo maana serikali ina maabara ya kisasa ya kupima mionzi na kuhakiki vifaa vinavyotumia mionzi katika sehemu mbalimbali nchini," alisema.

Ngamilo alisema lazima mionzi itumike kwa ajili ya maendeleo na endapo itatumika vibaya, inaweza kusababisha madhara ikiwamo saratani.

Mkuu wa Tume hiyo Ofisi ya Zanzibar, Ali Othman Masoud, aliwataka wananchi kuacha kufanya vipimo vya mara kwa mara vinavyotumia mionzi ikiwemo X-Ray ili kulinda afya na usalama wao.

"Tusiwe na utamaduni wa kurejea kupiga X-Ray mara kwa mara zisizo na ulazima kwa sababu mionzi ni hatari kwa binadamu," alisema.

Mkuu huyo alisema tume hiyo hufanya ufuatiliaji wa mara kwa mara wa viashiria vya mionzi katika vyakula vinavyoingizwa ndani ya nchi ili kuhakikisha kuwa ni salama kwa matumizi ya binadamu.




Mtafiti Mwandamizi wa Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania, Dk. Suleiman Amour Suleiman, akionyesha jarida linaloeleza kazi ya tume hiyo, wakati akizungumza na waandishi wa habari katika Maonyesho ya Biashara ya Miaka 56 ya Mapinduzi katika viwanja vya Maisara, mjini Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## Boti Zanzibar One kuanza leo

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

KAMPUNI ya Zanzibar Fast Ferries inatarajia kuzindua boti yake mpya ya Zanzibar One leo ambayo boti itakuwa inafanya safari zake kati ya Zanzibar na Dar es Salaam.

Akizungumza jana na waandishi wa habari, Makamu Mwenyekiti wa Kampuni hiyo, Salim Hassan Turkey, alisema boti hiyo iliyotengenezwa na kampuni ya Uholanzi yenye tawi lake nchini China, itasaidia kuondosha usumbufu kwa wananchi.

Alisema boti hiyo itakuwa na uwezo wa kubeba abiria 500 na imezingatia mahitaji ya watu wenye ulemavu.

Kwa mujbu wa Turkey, boti hiyo itakuwa na viwango tofauti vya nauli na watu wa chini watakuwa na daraja lao na itakuwa inafanya safari nne kwa siku kati ya Zanzibar na Dar es Salaam.

Alisema boti nyingine ya kampuni hiyo ya Zanzibar Two, inatarajia kuwasili Zanzibar Machi, mwaka huu, na itafanya safari kati ya Unguja na Pemba.

Kwa upande wao wananchi wa Zanzibar wamewaomba wamili wa boti za abiria kupunguza gharama za nauli ili kuweza kumudu gharama.

Amina Makame, mkazi wa mjini Zanzibar alisema ujio wa boti hiyo utapunguza usumbufu wa usafiri na ulaghai kwa baadhi ya mawakala wanaouza tiketi za boti ambao si waaminifu.

"Wakati mwingine unaenda kununua tiketi ya boti kwa mawakala wanapandisha bei holela au utaambiwa tiketi za kawaida zimeisha zilizobaki ni za daraja la juu wakati sisi wengine nauli yake hatuimudu," alisema.

Aidha, alisema kila boti za usafiri zinapoongezeka zinapunguza msongamano wa foleni wakati wa kununua tiketi.

**"Wakati mwingine unaenda kununua tiketi ya boti kwa mawakala wanapandisha bei holela au utaambiwa tiketi za kawaida zimeisha zilizobaki ni za daraja la juu wakati sisi wengine nauli yake hatuimudu," alisema.**

# Shein aelezea manufaa mipango ya UN

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, amesema utekelezaji wa mipango inayowekwa na Umoja wa Mataifa (UN) na taasisi zake umekuwa na faida nyingi kwa mataifa wanachama wa umoja huo.

Alisema Zanzibar ikiwa ni sehemu ya Tanzania, nayo haikuachwa nyuma katika mafanikio hayo kutokana na ushirikiano wake na taasisi na mashirika ya UN katika utekelezaji wa mipango yake ya maendeleo kwenye sekta zote muhimu za kiuchumi na kijamii.

Dk. Shein alisema hayo juzi katika hotuba yake iliyosomwa kwa niaba yake na Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi, katika sherehe za maadhimisho ya Siku ya Umoja wa Mataifa kutimiza miaka 74 zilizofanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa Sheikh Idriss Abdulwakil, Kikwajuni, mjini hapa.

Alisema Zanzibar imekuwa ikiendelea kufanya kazi na taasisi za UN katika kuendeleza na kukuza elimu, afya, mazingira, uvuvi, kilimo, kuimarisha demokrasia na utawala bora, kulinda na kuimarisha haki za binaadamu, mapambano dhidi ya ukatili wa kijinsia na watoto na masuala mengine ya maendeleo.

"Miradi iliyotekelezwa hapa Zanzibar kwa ushirikiano na Umoja wa Mataifa ni mingi katika awamu zote saba za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar tangu Mapinduzi ya mwaka 1964, hivyo tunahitaji muda mwingi zaidi kuitaja," alisema.

Alisema mfumo mpya unaotumiwa na mashirika ya Umoja wa Mataifa wa kuwashirikisha moja kwa moja wananchi wa kawaida ni utaratibu mpya na wenye mafanikio ambao umeonyesha wazi utekelezaji kwa vitendo wa dhamira ya umoja huo.

Dk. Shein alisema wananchi hasa wakulima wengi nchini wamefurahia na kuzipongeza juhudi zilizochukuliwa hadi wakapatiwa msaada wa vihori 100 vya kubebea mwani, kila kimoja kikiwa na uwezo wa kubeba zaidi ya kilo 400.

Kwa mujibu wa Dk. Shein, hatua hiyo imesaidia kupunguza usumbufu wa ubebaji wa mwani waliokuwa wakiupata wakulima wa zao hilo jambo lililowasababishia hivi sasa kuwa na uwezo mkubwa wa kuusarifu mwani katika kutengeneza bidhaa mbalimbali.

Alisema serikali itaendelea na jitihada ya kuwashirikisha wanawake katika vyombo vya utoaji wa uamuzi katika ngazi zote kwa kuwapa nafasi mbalimbali za uongozi.

Aidha, aliupongeza uamuzi wa Umoja wa Mataifa kwa kukitumia Kiswahili katika shughuli zake ikiwamo sherehe na maadhimisho ya kuzaliwa kwa umoja huo.

Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT
BURUDANI TELE
JUMAMOSI JANUARI 18, 2020



**OPRAH AWAPA NENO HARRY, MEGHAN** Soma UK.20



# KONDE BOY

# Kagusa kipele, atakayejikuna anahusika

## BASI SAWA

# Jors awaambia 'I Don't Care'

MAYARISHAJI na mwanamuziki chipukizi wa Bongo fleva, Jors, ameanza mwaka kwa kuitambulisha singo yake mpya inayoitwa "I Don't Care".

Wimbo huo umetayarishwa nchini Uholanzi na Menno Beck na yeye mwenyewe alifanya kazi za kuhariri na kuongeza vionjo.

'Naamini wimbo huu utawapa mashabiki wa muziki mtazamo mpya, naomba watarajie vitu vizuri zaidi," amesema Jors



# Loh! Wapenzi wakiumbuana, wewe kaa chini

MWANAMUZIKI wa Kenya, ametoa mpya baada ya kueleza kamwe hakuvutiwa na mwili wa mrembo Vera Sindika na kwamba alianza kumtongoza mwenyewe.

Otile alikuwa akijibu madai kuwa alitoka kimapenzi na mlimbwende ili kujipatia umaarufu ambao ameupata hivi sasa.

Wawili hao penzi lao lilivunjika 2018 ambapo Vera alijitosa kumlipua Otile kuwa kitandani alikuwa bure kabisa hakuwa akimridhisha, pia Vera alidai Otile alikuwa kapigika kipesa hivyo alikuwa tegemezi kwake.





# Tessy hataki kuzushiwa uongo

MAMA mtoto wa Aslay, anayefahamika kwa jina la Tessy, ameibuka na kukanusha kwamba hatoki kimapenzi na Diamond Platnumz.

Hivi karibuni kumesambaa taarifa kwenye mitandao ya kijamii kwamba mrembo huyo alionekana katika safari mbalimbali zinazoandaliwa na Diamond.

"Taarifa si za kweli na hakuna mwanadamu asiyekosa cha kuzungumza ama kuzusha unajua instagram ukiandikwa vibaya unaweza kupaniki na kuwajibu ila mimi nakaa kimya," alisema Tessy.



E

K

MAS

Buhe

msa

Aj

bara

kuto

likip

"A

sasa

tume

kupi

## INSTA-TWITTER





**Wanaume** wanaojitambua hawawezi kumpiga mwanamke! Tunapokaa kimya tunaendeleza vitendo hivi **- Mo Dewji.**



**Kuna** watu wanachukia wew kuwa na cheo ulichonacho, n kushangaza hata ukikiacha w hawawezi kukipata. Kuna watu wana chukia kwa sababu ya vitu unavyoen lea kununua na hata hawataki kujiuli umevipataje. Kuna watu watakusema vibaya kwa maneno ya uongo ili wak ibie sifa na kuchafua jina lako, hata wewe huna ugomvi nao. Kuna watu ja kuwa karibu na wewe ili tu wakuf vizuri na kutumia kila udhaifu watak ta kukushusha chini **-Madebe Lidai.**



# sha jua Mungu akunusuru

HABIKI wa mwigizaji nyota wa Bongo Muvi, Esha eti, wameguswa na ajali mbaya ya gari aliyopata nii huyo wakati akiwa safarini.
ali hiyo iliyosababishwa na ng'ombe aliyekatiza barani ilimuacha Esha akiwa na maumivu ya mwili kana na kujipigiza mara kadhaa wakati gari hilo induka.
Asanteni kwa message na simu nyingi sana ila kwa kichwa kinauma sana ni kweli tumepata ajali ila etoka salama Alhamdulillah" Ameandika Esha Buheti tia Instagram baada ya ajali hiyo.




>>> Usikose Jarida hili la Burudani Tele (BT) ndani ya Gazeti lako la Nipashe kila Jumamosi, pia lipo kwenye mtandao wa kijamii Twitter, tu' follow

## UNASEMAAA...

# Shilole ni mipasho tu kwa mashabiki

MSANII wa muziki, Shilole, amewabwatukia mashabiki zake kuacha tabia ya kumpanda kichwani kwa kumuuliza swali kwanini hapati mtoto na mumewe.

"Tutapata mtoto tu, halafu hayo sio mafungu ya nyanya kwamba yanawekwa tu pale, ni baraka kutoka kwa Mungu, bado siku haijafika hata mimi natamani sana kupata mtoto, naamini ataleta kheri kuhusu mashabiki zangu siwajali kwa sababu wao hawalali na mimi," amesema Shilole.

Alizidi kutoa dozi kwa kueleza "Wanajua kama nina matatizo gani au walishanipeleka hospitali wakajua kama nina shida gani, kwa hiyo wawe wavumilivu wasijaji maisha yangu, waangalie muziki wangu na biashara zangu mambo ya ndoa yangu na kutozaa hayawahusu nikipata waseme Inshaalah, nikikosa waseme Hewala".



## INSTA-TWITTER

e
a cha
vao
a-
nde-
za
a
kuhar-
wakati
wataku-
ahamu
aoupa-



Tuffolow/ Tu-tag
@burudanitele



**Vikwazo** huwa tunavitengeneza wenyewe vichwani mwetu, halafu tunaanza kuviamini kama kweli vipo, tuanze wiki kwa kuikataa imani hii - **Nikki wa Pilli.**



**Hakuna** urafiki ambao hauna matatizo wala misukumo. Ukitaka rafiki asiye na matatizo utakuwa mpweke daima - **Nandy.**



**Mwanamke** mapishi babu wee. Hakuna kitu kizuri kwa mumeo kama ujue kucheza na jiko! Yaani mume akienda kula nje anaona takataka anawaza nyumbani tu - **Juma Lokole**

Kuumbe!



KONDE BOY

# Kagusa kipele, atakayejikuna anahusika

MWANAMUZIKI anayeleta ushindani wa kipekee katika muziki wa kizazi kiya, Harmonize, ameamua kugusa kipele cha siku nyingi kinachosababisha muziki wa Bongofleva kukosa ushindani wa haki.

Akizungumza hivi karibuni, Harmonize ambaye amejitenga na lebo yake ya zamani ya WCB, amesema Bongo fleva imejaa watu wenye chuki na choyo, kiasi ambacho hata mtu akipata mafanikio inakuwa ni kama bahati.

Amesema nchi pekee katika Afrika ambayo wasanii wake wa muziki wanashirikiana na kupata mafanikio ya kweli ni Nigeria.

Harmonize amesema hayo wakati atambulisha ujio wa Album yake mpya ambayo ndani yake amewashirikisha mastaa mbalimbali wa ndani na nje ya Tanzania.

Amesema baadhi ya wanamuziki waliopata mafanikio kwa hapa nchini inatokana na kuwa na bahati na si vinginevyo.

"Hapa kwetu Tanzania msanii akiwa na mafanikio basi jua ni ana bahati, vinginevyo ni vigumu kutokana na kukosa ushirikiano kama wenzetu wa Nigeria," amesema.

Akitolea mfano nchi hiyo, Konde Boy. amesema wao kila mwaka msanii mmoja anakuwa juu na wengine wanampa usaidizi kwani wanajua wanafanya hayo kwa ajili ya nchi yao.

"Kwa upande wangu natamani jambo hilo, na ndio maana kwenye Albam yangu mpya nimewashirikisha nyota wengi kutoka Nigeria, Tanzania na Jamaica ili kutoa ladha na funzo muhimu kwetu," ameongeza kusema.

Harmonize amesema moja ya msanii ambaye atakuwepo kwenye Album hiyo, ni Burna Boy ambaye tayari amesharekodi nyimbo nne na ambazo hivi karibuni zitaanza kuchukuliwa picha za video.

Pia aligusia kufanya kazi na msanii Alikiba kwa kusema " "Mimi ni msanii naweza kufanya kolabo na msanii yoyote ndio maana nasema Konde boy for everybody, (Konde Boy wa kila mtu) nina amini muziki wa Afrika Magharibi unafika mbali sana kwa sababu ya ushirikiano."

Amesema kuwapa ushirikiano wasanii wengine kufanikisha Albam hiyo ni ndoto aliyokuwa nayo siku nyingi na sasa anafurahi kuitimiza.

"Sio kama siwezi kufanya albamu peke yangu, naweza lakini nataka kuwashirikisha familia yangu, hii ni maalum kila mtu awepo," amesisitiza.



# Waliojilipua kama Stamina



**Na Adam Fungamwango**

HABARI ya mjini kwa sasa ni ngoma ya msanii Stamina iiitwayo 'Asiwaze'. Ngoma hii hadi Ijumaa, ilikuwa imeshazamwa na watu 1,378,134 tangu ilipotolewa rasmi Januari 9 mwaka huu.

Idadi kubwa ya mashabiki kuupenda wimbo huo na kuwa na watazamaji wengi kwa muda mfupi nimaudhui ya wimbo wenyewe, pamoja na msanii mwenyewe kukubali ukweli kuwa amemuimba aliyekuwa mkewe.

Maudhui ya ngoma hiyo ni kwamba Stamina analalamika kuhusu ndoa yake ambayo imevunjika kwa sababu ambazo ni za kusalitiwa.

Ni kwamba mkewe alikuwa na uhusiano na aliyekuwa mchezaji wa Simba, kitu hicho kilisababisha ndoa yake kuyumba na hatimaye kuvunjika kabisa.

Imemuuma sana na kufikiri sana kuhusu kitu ndoa, akifikiria maandalizi na sherehe za harusi, gharama zilizotumika na muda, lakini vyote ni kazi bure.

Pamoja na kulalamika sana, lakini anawashauri watu, wanaotaka kuoa au kuolewa wasiogope kwa sababu ya yaliyomkuta, bali hayo ni maisha tu.

Wengi wametoa maoni tofauti kuhusu kitendo cha Stamina kuamua 'kujilipua' kuweka mambo yake ya ndoa, au mambo yanayumhusu yeye na familia yake hadharani. Wegine wamemsifu na kusema kuwa kitendo cha kuandika mistari hiyo na kuipeleka studio kutoa ngoma hiyo, kimeondoa kinyongo chote cha moyoni na sasa hatokuwa na mawazo yoyote mabaya, badala yake atataka maisha yaendelee.

Lakini wapo waliomlaumu na kusema kuwa hakupeswa mambo ya ndani kuyaweka hadharani. Hata hivyo, tangu miaka ya nyuma, wanamuziki walikuwa wakitumia muziki wao kutunga nyimbo ya mambo ambayo yamewakera au kuwakuta kwenye ndoa zao, wazazi wao au jamaa zao.

Leo tunawaletea wanamuziki ambao walipatwa na matatizo kama Stamina na wakatunga nyimbo.

**NENDA UKAISHI SALAMA - MIKIDADI SEIF**

Mzee Mikidadi Seif, aliyekuwa mwanamuziki wa bendi ya Uda Jazz, miaka ya '80 alitunga wimbo unaouitwa 'Nenda Ukaishi Salama', ambao uliondokea kupendwa mno.

Hivi majuzi tu akihojiwa na vitu vya redio alisema kuwa wimbo huo aliutunga kutokana na kumfumania mkewe Suzana laivu na mwanaume ambaye ni rafiki yake mkubwa.

Mzee Mikidadi anasema baada ya tukio hilo alimpa talaka mkewe na kwa dukuduku alilokuwa nalo alitunga wimbo huo.

**MICKY-MIKIDADI SEIF**

Mwanamuziki huyo wa Uda Jazz, Mikidadi Seif anayeonekana kupatwa na matatizo mara kwa mara kwenye ndoa zake, alitunga wimbo mmoja usemao 'Micky' jina ambalo ni kifupi cha jina lake Mikidadi.

Akihojiwa kwenye redio, alisema kuwa gari lililowarudisha majumbani kutoka kwenda dansi lilipata ajali na yeye kulazwa Muhimbili. Lakini kuna baadhi ya mashabiki wa kike walikwenda nyumbani kwake kumpa pole na kumkuta mkewe mwingine aliyemuoa, siyo yule Suzana tena.

Hawakumkuta, lakini maneno waliyokuwa wakiongea, yalionyesha kama vile na wana uhusiano naye.

Mkewe alikasirika na kuongea maneno makali juu yake, kumuonya na kutahadharisha kuwa akiendelea basi anaondoka. Mikidadi aliyechukua maneno ya mkewe na kuyatungia wimbo huo.

**SUNIASA-MBARAKA MWINSHEHE**

"Suniasa unipoze moyo mama kwa nini usinirudie, ingawa mimi ndiyo mwenye kosa nakuoma unisamehe." Ni maneno yaliyomo kwenye wimbo wa 'Suniasa' uliotungwa na marehemu Mbaraka Mwinshehe.

Kwa mujibu wa mkewe Amne Mbaraka ni kwamba alikorofishana na Mbaraka na kurejea kwao.

Kutokana na hali hiyo Mbaraka alitunga wimbo huo kwa ajili ya kumuomba radhi na kuurekodi.

Alipousikia mwenyewe alilainika na kurejea nyumbani, ugomvi ukaisha.

**BARUA KUTOKA WA MAMA-COSMAS CHIDUMULE**

Hapa mtunzi Cosmas Thobias Chidumule akiwa na Mlimani Park Orchestra alitunga wimbo huu kutokana na ugomvi wa wazazi wake. Kwa mujibu wake mwenyewe ni kwamba ni kweli wazazi wake alikuwa na ugomvi na yeye ndiye aliyekuwa akitakiwa kuwasuluhisha, lakini alikuwa akikwepa lawama, hivyo kutafuta ndugu, majirani na wazee wa kusuluhisha.

Alichofanya akachukua kalamu na kuandika wimbo kuwa ugomvi wa baba na mama yake hawezi kuingilia ili asije kosa radhi ya mmoja wao. Kwa sasa Chidumule anaimba nyimbo za Injili.

**KAZA MOYO-TX MOSHI WILLIAM**

Wakati wa uhai wake, TX Moshi William alitunga wimbo ulitwao 'Kaza Moyo'.

Aliuelezea mwenyewe wimbo huu kuwa ulitokana na watu kwenda kumueleza mkewe maneno ya uongo, kiasi cha kusababisha ugomvi mkubwa na kuiweka ndoa yake matatani, ingawa baadaye ukweli ulibainika. Baada ya zogo kwisha alitunga wimbo huo kuwa atakaza moyo hapa duniani ili awashinde wafitini.

IMETOKEA

# Warembo wanaotaka kwenda mwezini kazi kwenu

BILIONEA wa Japan Yusaku Maezawa, anamtafuta mwanamke atakayekuwa mpenzi wake wa maisha ili aandamane naye kutalii anga za mbali hadi mwezini.

Mwanamitindo huyo wa miaka 44, anajiandaa kuwa abiria wa kwanza kwenda mwezini kwa kutumia roketi maalumu inayofahamika kama 'Starship'.

Safari hiyo iliyopangiwa kufanyika mwaka 2023, itakuwa ya kwanza kwa binadamu kwenda mwezini tangu mwaka 1972.

Katika ombi lake alilochapisha kwenye mtandao Maezawa anasema anataka kufurahia safari hiyo na mwanamke wa kipekee.

Mfanyabiashara huyo ambaye hivi karibuni aliachana na mpenzi wake, muigizaji Ayame Goriki, mwenye umri wa miaka 27, ametoa wito kwa wanawake kuwasilisha maombi yao kuhusu safari hiyo ya kipekee kupitia tuvuti yake.

"Japo hisia ya upweke imeanza kunizonga, nafikiria kitu kimoja, kuendelea kumpenda mpenzi wangu," Maezawa aliandika katika tovuti yake.

"Nataka kumpata mpenzi wa maisha," alisema na kuongeza 'Nikiwa na mpenzi wangu mtarajiwa wa maisha, nataka kuutangazia ulimwengu penzi letu nikiwa mwezini."

Tovuti hiyo imeweka masharti pamoja na maelezo kuhusu jinsi ya kuwasilisha maombi katika mchakato huo utakaochukua miezi mitatu.

Masharti ya kushiriki lazima uwe bila mpenzi, uwe na miaka zaidi ya 20, uwe na mtazamo mzuri wa maisha na ufurahie kuzuru anga za mbali.

Muda wa mwisho wa kuwasilisha maombi ni Januari 17 ambapo uamuzi wa mwisho kuhusu mpenzi wa Maezawa utatolewa mwisho wa mwezi Machi.

Bilionea huyo ambaye amejizolea sifa kwa kuwa mpiga ngoma katika bendi ya punk, anajulikana kwa kujihusisha na visa ambavyo huzua gumzo na kuwaacha watu midomo wazi.

Mapema mwezi huu, aliahidi kupeana yenye Sh. milioni 100 sawa na dola 925,000, kwa watu 100 watakaoshiriki ujumbe wake wa twitter .

"Unachotakiwa kufanya ili kushiriki ni kunifuatilia kwa kutweet tena," alisema.

Mwanzilishi wa biashara ya kuuza nguo mtandaoni nchini Japan Zozo Inc, Maezawa alijizolea utajiri mkubwa katika ulimwengu wa uanamitindo.

Anaaminiwa kuwa na utajiri wa karibu dola bilioni, sehemu kubwa ya pesa hizo anatumia katika sanaa.





# Mwajuma N'chokonoe: Kunguru hafugiki

**Na Adam Fungamwango**

SI unakumbuka kuwa wasanii Roma Mkatoliki na Stamina, ambao walijiunga pamoja na kujiita 'Rostam', walipotoa ngoma kali inayoitwa 'Mwajuma N'chokonoe?'

Ilikuwa ni ngoma inayomhusu dada mmoja ambaye alikuwa kicheche na majirani walidhani kuwa hatoolewa. Matokeo yake akapata wa kumstiri akaolewa, kila mmoja wakabaki mdomo wazi, wakawa wanasutana wenyewe kwa wenyewe.

Sasa imetoka filamu ambayo nayo inaitwa jina hilo hilo la Mwajuma N'chokonoe. Hii haijachezwa na wasanii maarufu, bali wengi ni chipukizi, lakini wenye uwezo mkubwa na vipaji.

Tofauti kidogo na ile ngoma ya kina Rostam. Duniani una ndege ambao wanafugika. Unaweza kuwatia kwenye tundu na kuwapa chakula, wakaishi maisha yake yote.

Ndige wengine jamii kama bata, kuku khanga, unaweza hata ukawaachia asubuhi na kwenda kujitafutia chakula wenyewe, lakini jua linapoanza kuzama tu, wanarejea tunduni au kwenye banda ambalo mfugaji amewajengea, hadi watakapouzwa au kuchinjwa kwa ajili ya kutoweo.

Lakini kunguru ni mmoja kati ya ndege ambaye hafugiki. Fanya ufanyavyo. Mpe chakula anachokitaka, maji na kila aina ya kitu anachokitaka. Lakini akipata upenyo wa kuondoka, harejei tena kwenye tundu, tofauti na njiwa. Ndivyo ilivyo kwenye maisha wakati mwingine ndani ya jamii.

Mussa ni kijana aliyetokea kumpenda sana msichana Mwajuma. Lakini msichana huyo kila mmoja hapo mtaani anajua kuwa hajatulia. Ni kama samaki tu, hapishi chambo. Kila mwanaume wake. Vijana, watu wa makamo, wazee, walevi, ili mradi tu yeye anachokata ni pesa. Kwa tabia hiyo, mtaaji akabatizwa jina la 'Mwajuma N'chokonoe.'

Inafikia wakati sasa Mussa anaamua kutaka kumuoa. Taarifa anazifikisha kwa mama yake mzazi.

Mama Mussa anamkatalia na kumwambia kuwa kama mchumba mwenyewe ni Mwajuma basi yeye hamtaki na kama atamuoa bila ridhaa yake, basi asimshirikishe.

Kauli hiyo haimfanyi Mussa kutelekeza azma yake. Mwajuma anafumaniwa na mume wa mtu wakiwa nyuma ya wageni.

Mke wa mume huyo anatinga nyumbani kwa mama yake Mwajuma kufanya timbwili la nguvu na kumuacha mtoto ili amlee na yeye anaondoka, hataki tena ndoa.Mwajuma na mama yake wanaamua kumpeleka mtoto huyo kwa mjumbe wa nyumba kumi.

Taarifa hizo zinamfikia mama yake Mussa ambaye anazidi kumchukia Mwajuma, akijua kabisa atakuja kumsumbua tu mtoto wake. Hakuna mke hapo.

Mussa yeye hasikii wala haambiwi, mipango yake ya ndoa inakamilika bila kuwashirikisha ndugu zake ambao waliamua kujiweka pembeni.

Ugomvi wa Mwajuma na Kidawa ambaye ni mke wa Bocha aliyefumaniwa na Mwajuma unakuwa mkubwa mtaani kiasi cha kuunda makundi mawili. Moja ni 'timu Mwajuma N'chokomoe', lingine ni 'timu Kidawa.'

Wanawake wa upande huu wakikutana na wa timu nyingine hata njiani tu ugomvi wake usipime. Ngumi zinafumuka.

Matayarisho ya harusi yanaanza. Mwajuma na mama yake wanaanza kutembeza sare, tena kwa 'kigoma cha uruguay.'

Kigoma hicho kikafika hadi nyumbani kwa mama Mussa, nia ni kwenda kumsuta kwa kitendo chake cha kupinga mwanaye asimuoe Mwajuma.



DRAKE HUYOOO AFRIKA

# Kutumbiza Nigeria, Ghana, Afrika Kusini

RAPA kutoka Canada ambaye ana makazi yake nchini Marekani, Drake, ametangaza kufanya ziara ya kimuziki katika nchi tatu za Afrika.

Drake anaungana na wanamuziki wengine wa Marekani kuzuru Bara la Afrika kutumbuiza, wasanii hao ni Card B na Future.

Wanamuziki hao walifanya shoo zao mwezi Desemba mwaka jana.

Katika tangazo lake amelitoa kupitia ukurasa wake wa Instagram, ataanzia ziara yake nchini Nigeria Machi mwaka huu, kisha anaelekea Afrika Kusini na Ghana kabla ya kurudi tena Nigeria.

Mshindi huyo wa tuzo za Grammy katika ziara hiyo ya kikazi atatumbuzia katika miji sita tofauti na anatarajia kuwapagawisha mashabiki wake. Kulingana na maofisa wake, mkali hiyo wa Hip hop, atafanya shoo zake katika miji mitatu akiwa Afrika Kusini, mbili Nigeria na moja nchini Ghana.

Ratiba yake inaonesha kwamba Machi 18, atatumbuiza ndani ya Jiji la Johannesburg. Afrika Kusini na siku inayofuata atakwenda Durban na kumalizia Cape Town Machi 22, mwajka huu.

Machi 27 ataangusha shoo ya aina yake katika Jiji la Accra nchini Ghana.

Nchini Nigeria atapanda jukwaani katika Jiji la Lagos, Machi 29 na siku ya pili ataivamia Abuja na kufanya mambo yake.




# Davido aamua kuingia kanisani

WAKATI tuhuma za kula bata na mwanamke wake wa zamani zinapoa, mwanamuziki Davido, ameamua kujifariji kwa kwenda kanisani kumuomba Mungu.

Davido ambaye anajulikana kwa tabia yake ya kukesha katika klabu mbalimbali akila raha, aliwashangaza wengi baada ya kuweka video fupi kwenye akaunti yake ya Instagram akionekana akiingia kanisani na familia yake.

Mwanamuziki huyo, alijumuika na dada yake Sharon Ademefun, B-Red katika kanisa hilo lililopo katika kisiwa kimoja kwenye jiji la Lagos.



## Card B wenzio wamechoka fiksi

RAPA nyota wa Marekani, Card B, ameibua mjadala baada ya kuonyesha zawadi aliyopewa na rafiki yake wa karibu Beyonce.

Mwanamuziki huyo aliposti video fupi ikionesha sanduku lililojaa zawadi mbalimbali za nguo na viatu kutoka kampuni ya Adidas x Ivy Park Collections.

Cardi B anajulikana kwa kujipa sapraizi mwenyewe na kwamba zawadi hiyo haikuwashtua mashabiki wake kama alivyotarajia.

## Stella pole sana, yote ni Mungu

MWIGIZAJI mkongwe wa Nollywood, Stella Damasus, amempoteza mama yake mlezi ambaye alikuwa akimtambulisha kama rafiki yake kipenzi.

Nyota huyo wa filamu alitoa tangazo la kufiwa na mama yake kupitia akaunti ya Instagram, na kuelezea jinsi alivyohuzunika kutokana na kifo hicho.

"Nimempoteza rafiki yangu kipenzi, shujaa wangu wa ibada, malaika wangu na mama yangu mlezi. Mwanamke huyu alikuwa karibu yangu na mambo mengi ya kunishangaza," aliandika Stella.





## Tacha sasa kuibukia kwenye muziki

ALIYEKUWA mshiriki wa shindano la Big Brother Nigeria 2019, Tacha, ataachia singo yake ya kwanza baada ya kuamua kuingia kwenye muziki.

Natacha Akide maarufu kama Tacha amejizolea wafuasi wengi baada ya kufanya vizuri katika shindano hilo.

Kulingana na mrembo huyo, amepanga kuzindua brandi yake mapema iwezekanavyo katika muziki kabla ya kuangalia suala la uigizaji.

## Oprah awapa neno Harry, Meghan

MTANGAZAJI wa vipindi vya maisha, Oprah Winfrey, amewatakia mkono wa baraka Prince Harry na Meghan Marklem kujiondoa katika shughuli za kifalme.

Oprah amewashauri wanandoa hao kuangalia nyuma maamuzi hayo kama wanataka kujiondoa katika maisha ya kifalme.

"Meghan na Harry hamuitaji usaidizi wangu kuhusu nini kizuri juu yenu, Niwatunza wote na kuunga mkono nini maamuzi yenu kwa familia," alisema Oprah.



**SAFU**



**MIONZI YA SHERIA**

Na John Juma
0716217615

# Je, umezaa nje ya ndoa? Rekebisha hivi mirathi

UNAWEZA kuwa na watoto wa namna mbalimbali. Unao uliowazaa ndani ya ndoa na wale uliowazaa nje ya ndoa.

Unawapenda sana wote kwa usawa kwasababu wote ni watoto wako. Kuna suala la kifo na ungependa baada ya kifo chako watoto wako wote wafaidi kidogo ulichochuma. Lakini, je, hilo umelijengea mazingira?

Ni muhimu sana ujue kuwa suala la watoto wako kufaidi ulicho nacho halitokani na matakwa yako, la hasha, bali linatokana na matakwa ya sheria.

Wewe waweza kuamua watoto wako wote wa nje ya ndoa na wale wa ndani ya ndoa wapate mali, lakini baadhi wakakosa kutokana na msimamo wa sheria.

Ni hapo unapotakiwa kuandaa mazingira yanayoendana na matakwa ya sheria, ili watoto wako wote wafaidi manufaa yako.

Sasa unapaswa kufanya yafuatayo ili kuwaezesha watoto wa nje kuwawezesha watoto.

• Kwa Waislamu: Kama wewe ni Muislam na una mtoto/watoto nje ya ndoa, na unataka kuwahusisha katika mirathi unaandika wosia ambao utampatia mali hata huyo mtoto wa nje ya ndoa. Lakini lazima ujue kuwa mali yako yote uliyo nayo ni 1/3 = (100%) (theluthi moja). Hivyo theluthi mbili ya mali yote, ni lazima iende kwa warithi halali na mtoto wa nje ya ndoa hataingia kabisa.

Katika mali hiyo ya theluthi mbili, haihitaji wosia kwa kuwa tayari sheria ya Kiislam, imeeleza vipi hiyo mali igawanywe.

Uhuru wako wa kugawa mali kwa wosia upo katika theluthi moja na si vinginevyo. Ni kusema kuwa mtoto au watoto wa nje ya ndoa, haki yao ipo katika theluthi tu.

Ikiwa utampatia mali zaidi ya theluthi, basi anaweza kunyanganywa. Kwa hiyo uelewe kuwa wosia utakaoandika unahusu theluthi ya mali pekee.

Zingatia kuwa, usipoandika wosia kugawa theluthi yote au sehemu yake kwa mtoto/watoto uliowazaa nje ya ndoa, basi hawatapata mali kabisa baada ya kifo chako. Hii ni kwa sababu watoto hao hawaruhusiwi kurithi kisheria.

Kwa hiyo utaona kuwa unachotakiwa kufanya ili hao watoto wasikose, ni
kupiga hesabu ili kupata 1/3 ya mali yako na kuwapa yote au sehemu yake.

b. Wanaoishi kimila; Karibu taratibu za kimila zote haziruhusu watoto wa nje ya ndoa kurithi. Hiyo maana yake, ikiwa unaishi maisha hayo na unakufa hawatarithi. Unachotakiwa kufanya waweze kurithi hata baada ya kifo chako ni kuwahalalisha watoto hao kabla hujafa.

Utaratibu wa kuwahalalisha watoto wa nje ya ndoa hutofautiana katika mila na mila. Utakachofanya ni kufuata utaratibu wa mila yako kama ulivyo na kuwahalalisha watoto hao. Usiseme nitaandika wosia niwape mali hapana.

Hii ni kwa sababu wosia wataupinga kuwa ni wosia uliokiuka taratibu kwa kuwarithisha wasiostahili. Kinachotakiwa ni kuwahalalisha kwa mujibu wa mila yako.

c. Kwa wasio Waislamu; Hawa mara nyingi ni Wakristo. Sheria inayotumika kwao ni Sheria ya Urithi ya Mwaka 1865. Nayo inakataza mtoto wa nje ya ndoa kurithi. Hivyo basi, ili kumwezesha kurithi, unatakiwa kuwa umeandika wosia ambao utawapatia mali.

Ikiwa utakufa bila kuacha wosia hata kama ulikuwa unaishi, nao hawataruhusiwa kurithi. Kinachotakiwa ni uandike wosia na wao uwajumuishe humo.

Pia, hii ni ziada na vyema kuwa umewatambulisha kwa ndugu zako, wana ukoo na hata mke kama unaye.

Kwa jumla ifahamike kuwa ni muhimu kuweka maandalizi ya kisheria katika suala la mirathi.

Usipofanya hivyo, usitegemee watoto au mtoto wa nje ya ndoa kurithi mali zako, lakini pia ujue utakuwa umekufa huku umeanzisha mgogoro mkubwa katika familia.



**KALAMU YA MWALIMU**

Na Reubeni Lumbagala
0764-666349.

# Wanafunzi wakorofi badilikeni, mmesikia agizo la Waziri Jafo?

ILIPOFIKA Januari mwaka huu, shule za msingi na sekondari nchini zilifunguliwa, kuanza mwaka mpya wa masomo, 2020. Hiyo ni baada ya likizo ya mwezi mzima, walimu na wanafunzi walipata wasaa kupumzika, baada ya kazi kubwa ya kusoma na kufundisha shuleni.

Tukiwa tupo mwanzoni kabisa mwa kufunguliwa kwa shule zetu za msingi na sekondari, napenda kuwakumbusha wanafunzi, mwaka huu unaweza kuwa mzuri au mbaya kwa mustakabali wa elimu zao.

Hiyo ni kutegemea namna mwanafunzi atakavyoamua kuishi na kuheshimu sheria na kanuni za shule au kuzivunja sheria hizo zinazomwongoza shuleni kwake. Ni uamuzi wa mwanafunzi kusuka au kunyoa, nitafafanua.

Mwishoni mwa mwaka jana, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, alitoa agizo ambalo wanafunzi wote wanapaswa kulitii, waweze kuendelea vyema na masomo yao pasi kukumbana na mkono wa sheria, unaoweza kusababisha kufukuzwa shule na hatimaye kufikishwa katika vyombo vya sheria kwa hatua zaidi.

Iko hivi, mwaka jana kulitokea matukio mawili katika Shule za Sekondari ya Liwanja iliyopo wilayani Chunya, Mkoa wa Mbeya na Sekondari ya Mji Mpya ya Manispaa ya Morogoro, ambako baadhi ya wanafunzi wasio na nidhamu, waliharibu miundombinu na samani za shule hizo na kusababisha hasara kwa Taifa.

Wanafunzi wa shule hao walichoma mabweni, kuharibu samani za shule na kuchora vibonzo na majina yao katika majengo ya shule, jambo ambalo ni kinyume na sheria na kanuni za shule.

Kimsingi, kilichofanywa na wanafunzi hawa ni jambo linalopaswa kukemewa na kila mpenda maendeleo ya sekta ya elimu na nchi.

Ni kwa sababu, mwanafunzi hapaswi kushiriki katika uharibifu wa miundombinu ya shule, kwani wanayotumia leo, ilishawahi kutumiwa na wenzao waliotunza hadi kufikia hatua wao kuikuta katika kusaka stadi, maarifa na ujuzi shuleni.

Aidha, sheria na kanuni za shule ziko wazi katika makosa yanayoweza kumfukuzisha mwanafunzi shule. Mojawapo ni kuharibu mali ya shule kwa makusudi.

Hivyo, napenda kuwashauri wanafunzi wote kuwa wabadili tabia zao, waheshimu sheria na kanuni ili kuepuka kukatisha masomo kwa kufukuzwa shule kwa makosa yanayoepukika.

Kutokana na uharibifu wa miundombinu uliojitokeza katika shule hizi mbili, serikali iliamua kuwalipisha wazazi wa watoto wao fedha ili kufidia hasara kwa kukarabati upya miundombinu ya shule.

Baadhi ya wanafunzi katika Shule ya Sekondari Kiwanja walifukuzwa moja kwa moja. Hayo ni madhara ambayo wazazi na watoto wameyapata, kutokana na utovu wa nidhamu shuleni.

Waziri Jafo alitamka: "Serikali haiwezi kuvumilia kuendelea kuwa na wanafunzi waharibifu na wasio na maadili mema katika shule za umma."

Kila mwanafunzi afahamu kwamba, kuharibu miundombinu shuleni kwa makusudi, tena wakati mwingine kufuata mkumbo wa kuiga wengine wanachofanya, anajiweka hatarini kukumbana na kilichowapata wenzao wa Kiwanja na Mji Mpya.

Waziri Jafo aliagiza kuwa wazazi na walezi watawajibika kutengeneza kifaa au mali kuirejesha katika hali yake ya awali na mzazi au mlezi wa mwanafunzi atakayekaidi agizo hili, mwanaye atasimamishwa masomo au kufukuzwa shule.

Kuna haja gani ya mwanafunzi kumwingiza mzazi au mlezi wake katika hasara ya kulipa mali au kufukuzwa shule kwa kuharibu mali ya shule ambayo haijafanya kosa au dhambi yeyote?

Kama wanafunzi wanakabiliwa na tatizo lolote, zipo njia nzuri za kuwasilisha malalamiko yao kwa viongozi wa serikali ya wanafunzi bila kuharibu miundombinu ya shule ambayo imegharimu fedha nyingi hadi kukamilika kwake.

Serikali inatumia fedha nyingi katika ununuzi wa vitabu, kukarabati na kujenga shule mpya, kujenga nyumba za walimu, maabara, vyoo, ofisi za walimu, mabwalo, maktaba nk ili kuwawezesha wanafunzi kuwa na mazingira mazuri ya ufundishaji na ujifunzaji ili kupata elimu bora itakayowasaidia katika maisha yao ya sasa na ya baadaye.

Katika kuungana na Waziri Jafo kukemea uharibifu wa miundombinu ya shule, Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Mlali 'B' wilayani Kongwa, Diego Mshana, ana msisitizo wake:


"Miundombinu tuliyonayo shuleni ni kwa sababu waliotutangulia waliitunza vinginevyo tungekuwa na mazingira magumu ya kujifunzia na kufundishia, kuiharibu ni ubinafsi kwa vizazi vijavyo."

Kwahiyo, wanafunzi shuleni wahakikishe hawawi chanzo cha kuitia hasara serikali kwa kuharibu miundombinu, kwani imegharimu fedha nyingi za walipa kodi. Ni vyema mwaka 2020, mwanafunzi akapanga kupiga kitabu na si kuharibu miundombinu ya shule.

Tafakari chukua hatua!

• ***Reubeni Lumbagala ni Mwalimu wa Shule ya Sekondari Mlali, wilayani Kongwa, Mkoa wa Dodoma.***
***Maoni: (+255) 0764 666349.***

# MKAKATI KUINUSURU SAHEL WAKAMILIKA



Viongozi wa nchi za Sahel wakiwa na Rais wa Ufaransa Emmanuel Macron, katika mkutano wao kupanga mkakati mpya wa kukabiliana na ugaidi.

**Na Mwandishi Wetu**

UFARANSA na mataifa matano ya ukanda wa Sahel, inayojulikana kama G5 yametangaza kuimarisha ushirikiano katika vita dhidi ya ugaidi kwenye eneo hilo linalokabiliwa na mashambulizi ya mara kwa mara ya wanamgambo.

Katika mkutano wa kujadili mbinu na mikakati ya kuwatokomeza wanamgambo hao wanaosababisha mauaji katika nchi hizo, ujumbe ulikuwa ni wa wazi, nao ni kuhakikisha ukanda huo unakuwa salama.

Rais wa Burkina Faso na mwenyekiti wa mkakati wa mataifa hayo matano, Marc Christian Kabore, amesema kunahitajika matokeo ya haraka katika vita hiyo kwa sababu bado kuna kitisho cha kukosekana kwa imani miongoni mwao.

Amewaambia viongozi wenzake kuwa wanahitaji kudhihirisha uwezo wao wa kukabiliana na changamoto hiyo.

Rais Kabore ameonekana kuwa na umakini katika mkutano huo uliofanyika kwenye mji wa Pau kusini mwa Ufaransa, kutokana na nchi yake kupoteza idadi kubwa ya wananchi baada ya kuuawa na wanamgambo hao.

Mataifa yanayounda kundi la kimkakati la G5 ni Mali, Burkina Faso, Niger, Chad na Mauritania.

Hali ya usalama inazidi kuzorota kila uchwao kufuatia kuongezeka mashambulizi. Kati ya Januari na Novemba mwaka jana, zaidi ya raia 1,500 waliuawa na milioni moja waliyakimbia makazi yao.

Idadi hiyo ni mara mbili ya wale waliokimbia mwaka jana, kulingana na takwimu ya Umoja wa Mataifa.

Shambulizi la hivi karibuni Januari 9 katika Mji wa Chinegodar Kaskazini mwa Niger lilisababisha vifo vya wanajeshi 89.

Hata hivyo, Rais Emmanuel Macron wa Ufaransa ameamua kuwakutanisha viongozi hao baada ya kukabiliwa na ukosoaji mkali kuhusiana na utendaji kazi wa wanajeshi wake waliopo Sahel.

Ni kutokana na hali hiyo nchi hiyo na mataifa ya G5 yametangaza kuanzisha mfumo wa ushirikiano wa kijeshi utakaoratibu shughuli za Jeshi la Ufaransa lililopo kwenye ukanda huo tangu mwaka 2014.

Wanajeshi wa Ufaransa wanafikia 4,500 pamoja na muungano wa majeshi ya G5 yenye jumla ya wanajeshi 5,000. Nchi hiyo imeahidi kuongezea wanajeshi wengine 220 kufanikisha mkakati huo wa pamoja.

Kikosi kipya kinachoitwa Takuba kitaundwa ili kuviunganisha vikosi maalum kutoka nchi nyingine za Ulaya, ambazo ni Uingereza, Denmark na Ujerumani.

Mkuu wa zamani wa ujumbe wa kijeshi wa Ufaransa na mshauri wa masuala ya kijeshi Jenerali Dominique Trinquand, ameliambia shirika la habari la DW kwamba hiyo ni habari njema.

Trinquand anaamini kwamba ukanda wa Sahel unatakiwa kuangaliwa kwa jicho la kipekee katika mapambano dhidi ya ugaidi. Wasiwasi uliopo ni Sahel inaweza kuwa kama Syria hapo baadaye na huenda wapiganaji wake wakatumwa kwenye mataifa ya Ulaya kufanya mashambulizi ya kigaidi.



Askari wa kupambana na ugaidi wakilinda usalama katika maeneo ya jangwani.

**RAIA WANASEMAJE?**

Abdoulaye Adouwal aliyetokea mji mkuu Paris ameiambia DW kwamba anataka vikosi vya Ufaransa viondoke. Anadai kwamba viongozi wao wameleta wanajeshi wa nje wakidai watarejesha usalama, lakini bado mashambulizi yanaendelea.

Anasema ni bora wangewapa mafunzo ya kijeshi vijana wa nchi zao ili warejeshe amani za nchi zao wenyewe.

Mtafiti mwandamizi kwenye taasisi ya masomo ya usalama nchini Ivory Coast, William Assanvo, anaielewa ghadhabu hiyo, ingawa anaamini kwamba bila ya wanajeshi hao wa Ufaransa hali ingekuwa mbaya zaidi. Anasema, ni wazi G5 wanahitaji msaada.

Lakini pamoja na yote bila ya kuwapo mikakati mipya ya kupambana na ugaidi kwenye ukanda wa Sahel, kuna wasiwasi kwamba miito ya vikosi hivyo kuondoka itaongezeka.

MAREKANI YAKOSOA

Hivi karibuni Marekani imezikosoa nchi za ukanda wa Sahel kwa kushindwa kudhibiti na kurejesha utulivu wa eneo hilo.

Imewalaumu viongozi wake wameshindwa kuchukua hatua madhubuti za kuhakikisha utulivu, wakati mashambulizi ya wanamgambo yakiongezeka.

Naibu balozi wa Marekani katika Umoja wa Mataifa, Cherith Norman, ameliambia Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, kuwa kunahitajika uwajibikaji zaidi katika kukabiliana na machafuko ya kikanda kutoka kwa serikali za nchi hizo.

Aidha, anasema mara kadhaa jeshi linashindwa kushughulikia chanzo cha mizozo, na kuongeza kwamba Marekani imeidhinisha msaada wa zaidi ya dola bilioni 3.5 mwaka 2017 na 2018 ili kuunga mkono uthabiti na usalama wa eneo hilo la Afrika Magharibi.

***Kwa msaada wa mtandao***

MAKALA



Rais wa Urusi, Vladimir Putin (kushoto), akiwa na aliyekuwa Waziri Mkuu wa nchi hiyo, Dmitry Medvedev. **PICHA: MTANDAO**

# KARATA NYINGINE YA RAIS PUTIN

## • Kuongoza serikali hata akimaliza urais?
## • Katiba kubadilishwa kuongeza nguvu

WIKI hii dunia ilipatwa na mshtuko baada ya kiongozi wa Urusi, Vladimir Putin, kutangaza mabadiliko ya mwenendo wa kisiasa nchini humo na kusababisha Baraza la Mawaziri kujiuzulu.

Tukio hilo la kipekee limewashangaza hata mawaziri katika serikali ya Urusi, kwani hawakuona uwezekano wa wao kujiuzulu ndani ya serikali.

Hungeweza kubisha kwamba Vladimir Putin, 67, amebadili mawazo na mtazamo wake wa kisiasa ikiwa imesalia na miaka minne kabla ya kuondoka madarakani.

Akiwa amekalia kiti cha urais miaka 20, kila mmoja alitabiri kiongozi huyo anapanga namna ya kurudi tena madarakani kwa njia nyingine.

Serikali mpya inayoongozwa na Mikhail Mishustin, mwenye ujuzi wa mifumo ya kodi Urusi, aliweza kuibadilisha nchi hiyo na kuwa na mfumo ulipaji kodi ambao unaopendwa na wananchi kuliko ilivyokuwa awali.

Dmitry Medvedev, ambaye alijiuzulu kumpa nafasi Putin kuunda serikali mpya, aliwahi hata kuwa rais kwa miaka minne, kwa sababu kulingana na katiba ya Urusi isingewezekana Putin kuendelea.

Medvedev, kiongozi wa chama tawala cha Urusi asiye na ushawishi mkubwa, bado yupo lakini majukumu yake mapya kama naibu wa baraza la usalama la Urusi huwa hayaangaliwi sana na umma.

"Kwake ni kama kupata dhahabu. Hii inamaanisha kwamba kuwekwa katika Baraza la Usalama ni sawa na kuwa mtu wa karibu na Putin na serikali yake ndogo," amesema Alexander Baunov kutoka jopo la ushauri wa sera za ndani na nje ya nchi.

Putin anafikia pale alipokuwa baada ya kipindi chake cha pili madarakani, wakati ambapo Dmitry Medvedev alikuwa makamu wake.

Lakini wakati huu, rais huyo hatakuwa kimya tu akiangalia kama waziri mkuu. Kwa sasa inaonekana kana kwamba muhula wa nne wa Putin madarakani kama utakuwa wa mwisho.

Kwa hiyo nini anachotaka?

Kwa nje, inamaanisha kwamba bunge litakuwa na nguvu zaidi kwa kuchagua waziri mkuu na kuidhinisha Baraza la Mawaziri. Lakini hilo halitatokea sasa wakati Putin amemchagua mrithi wa Medvedev.

**"Putin anataka kusalia madarakani lakini swali ni je, hilo linawezekana vipi? Amehoji Goryashko. Kwa wakati huu tunakaribia kuwa na uhakika wa kwamba Putin hataendelea kuwa rais baada ya 2024, lakini majukumu atakayochukua baada ya hapo. Huenda hata ikawa jukumu alilonalo sasa hivi la kiongozi wa baraza la taifa.**

Kwa suala la bunge kuwa na nguvu zaidi, hilo bado halijajitokeza wazi. "Wabunge watakuwa walewale, siyo mengi yatakayobadilika," amesema Sergei Goryashko wa BBC nchini Urusi.

Wakati Rais Putin anapendekeza kuwa na kura maoni katika mabadiliko ya katiba, itakuwa kura ya kwanza ya aina hiyo tangu mwaka 1993.

Moja ya pendekezo linalopendwa na wengi ni kubadilisha Baraza la Taifa kuwa taasisi rasmi ya serikali itakayojumuishwa kwenye katiba.

Kwa wakati huu ni bodi ya ushauri yenye kujuisha magavana 85, maofisa wengine wakiwemo viongozi wa kidini. Bodi hiyo ni kubwa kiasi kwamba siku ya kufanya mikutano inabidi wakutane kwenye jumba la serikali lililopo Kremlin.

Bwana Putin ameweka hatima ya baraza hilo wazi. Moja ni kwamba anaweza kuwa kiongozi mpya mwenye nguvu.

"Ukweli wa kwamba ameanza mazungumzo kuhusiana na Baraza hilo la Taifa na huenda anajaribu kuunda nyadhifa nyengine itakayokuwa na nguvu zaidi, ambapo anaweza kuwa juu ya wadhifa wa rais," Baunov amesema.

"Putin anataka kusalia madarakani lakini swali ni je, hilo linawezekana vipi? Amehoji Goryashko. Kwa wakati huu tunakaribia kuwa na uhakika wa kwamba Putin hataendelea kuwa rais baada ya 2024, lakini majukumu atakayochukua baada ya hapo. Huenda hata ikawa jukumu alilonalo sasa hivi la kiongozi wa baraza la taifa.

Sam Greene, Mkuu wa Taasisi ya Urusi iliyopo King's College London, anaamini kwamba viongozi wanaotafakari hatima yao baada ya 2024, kwa sasa watahitajika kucheza karata zao vizuri macho yao kwa bunge, Baraza la Taifa na Putin mwenyewe.

Watu wamepokeaje hatua hii?

Kwa Alexei Navalny, mpinzani ambaye ni tishio kwa Putin, anaona mabadiliko ya sasa ni mwanzo wa kurejea kwa siasa za mfumo wa kisovieti na kura yoyote ya kupendekeza mabadiliko kwenye katiba itakuwa ulaghai.

Mwanaharakati Lyubov Sobol pia alikuwa anashtumu kwa kusmea "Kubadilisha wezi na wezi wengine hakuwezi kuwa mabadiliko wala mageuzi."

## MAKALA



Baadhi ya watoto wanaokimbia ukeketaji na kulelewa katika vituo vya nyumba salama za Butiama na Mugumu wakiwa na Mkurugenzi wa Shirika la Hope for Girls and Women Tanzania, Rhobi Samwelly. **PICHA: MTANDAO**

# WASICHANA 36 WAKIMBIA UKEKETAJI MARA

**Na Sabato Kasika**

JUMLA wasichana 36 kutoka wilayani Tarime mkoani Mara, wameepuka na vitendo vya ukeketaji baada ya kukimbilia katika Kituo cha Nyumba Salama.

Idadi hiyo ni ya wasichana waliopokelewa kuanzia mwezi Desemba mwaka jana hadi mwaka huu, kulingana na Mkurugenzi wa Shirika lisilo la Kiserikali la Hope for Girls and Women Tanzania, Rhobi Samuel.

Robi ambaye anamiliki kituo hicho cha Nyumba Salama, anasema miezi hiyo huwa ni kipindi cha ukeketaji kila mwaka.

"Kimsingi ukeketaji ni mila inayopigwa vita kwa sababu una athari kwa mtoto wa kike, ndiyo maana kumekuwapo na jitihada za kuitokomeza, lakini bado tatizo lipo kwenye baadhi ya makabila," anasema Rhobi.

Anasema, Hope for Girls and Women Tanzania, ambayo inamiliki vituo viwili katika wilaya za Butiama na Mugumu wilayani Serengeti, zimekuwa kimbilio kwa wasichana wanaokataa kukeketwa.

**WALIVYOOKOLEWA**

Rhobi anasema, kila ifikapo mwezi Desemba huwa ni kipindi cha ukeketaji, hivyo muda huo unapowadia wasichana wanaokuwa hatarini wanatafuta marafiki wa shirika hilo kuomba msaada wa kukimbiza.

"Ndivyo ilivyokuwa kwa mwaka jana mwanzoni, tulipokea hao wasichana ambao walifika Butiama kwa msaada wa marafiki wa Hope for Girls and Women Tanzania," anasema.

> **"Marafiki zetu wanajulikana, hivyo mabinti, ambao wameshapata elimu kuhusu madhara ya ukeketaji, inakuwa rahisi kuwafuata, na ndivyo ilivyotokea kwa hao wasichana 36 waliokimbia hadi Butiama," anasema.**

Anasema shirika hilo lina marafiki karibu kila kona ya mkoa wa mara, na ilikuwa ni rahisi wasichana hao kuwafuata na kuwezesha kuepukana na ukatili huo.

"Marafiki zetu wanajulikana, hivyo mabinti, ambao wameshapata elimu kuhusu madhara ya ukeketaji, inakuwa rahisi kuwafuata, na ndivyo ilivyotokea kwa hao wasichana 36 waliokimbia hadi Butiama," anasema.

Mkurugenzi huyo anafafanua kuwa marafiki hao wakawasiliana na viongozi wa Hope na kuelekezwa wawapeleke wasichana hao, katika kituo cha Nyumba Salama kilichopo Mugumu.

"Baada ya kuwapokea tulishirikisha ustawi wa jamii, dawati la jinsia na tukaweka mikakati ya kujenga urafiki na wazazi wao na kuwaelimisha kuhusu madhara ya ukeketaji," anasema.

Mkurugenzi huyo anasema, lengo la kufanya hivyo ilikuwa ni kutaka wazazi na walezi waelewe madhara ya ukeketaji na kuachana vitendo hivyo na hatimaye kuishi na watoto wao salama.

Anafafanua kuwa shirika hilo lina fomu maalum, ambazo anapewa mzazi kabla ya kukabidhiwa mtoto wake, akiapa kutojishughulisha na vitendo vya ukeketaji.

Rhobi anasema, fomu hizo pia zinasainiwa na viongozi wa serikali wakiwamo wa ustawi wa jamii na dawati za jinsia, hivyo mzazi anayekiuka anajiweka katika mazingira ya kukumbana na vyombo vya dola.

**27 WARUDISHWA KWAO**

Anasema, kutokana na utaratibu huo, wasichana 27 wamerudi nyumbani kwao, kuendelea na masomo, baada ya wazazi wao kuelimisha na kuelewa madhara ya ukeketaji na kuahidi kutowafanyia watoto wao vitendo hivyo vya kikatili.

"Kwa hiyo hadi sasa wasichana hao wako kwa wazazi wakiendelea na masomo baada ya kuwekeana makubaliano maalum, ambayo ni lazima mzazi ayatimize kwa ajili ya usalama wa mtoto wake," anasema.

Mkurugenzi huyo anasema, wakati wasichana hao wanarudi kwao, wengine tisa wataendelea kuwapo kituoni hapo baada ya wazazi wao kukataa kuwapokea, wakidai mabinti hao wamewadhalilisha kwa kukataa kukeketwa.

"Tutaendelea kuwa nao na tutawasomesha, mpaka wahitimu, watapata mafunzo maaluma ya kuwawezesha kujitegemea hapo baadaye," anaongeza kusema.

Anasema, wataendelea kujadiliana na wazazi wao, huku Hope ikiwapa mafunzo maalum kuwasaidia kujitegemea endapo watarudi kwa wazazi wao.

**MADHARA YA UKEKETAJI**

Wataalamu wa afya wanasema ukeketaji una madhara kiafya na huweza kusababisha kifo wakati akifanyiwa kutokana na kupoteza damu nyingi.

Aliyekeketwa anaweza kupata uharibifu mkubwa wa mfumo wa nje ya uzazi, matatizo wakati wa ujauzito na kujifungua.

Pia humsababishia maumivu wakati wa kujamiiana.

Hivyo ni wajibu wa wadau wote wanaopinga vitendo hivyo, kuendelea kutoa elimu kwa jamii kuhusu ubaya wa ukeketaji.

HABARI KIMATAIFA

## Wanajeshi Marekani wajeruhiwa shambulio la Iran

**WASHINGTON,** Marekani

UONGOZI wa juu wa Jeshi la Marekani umekiri kuwa wanajeshi kadhaa walijeruhiwa katika shambulio la makombora lililofanywa na Iran katika vituo viwili vya jeshi nchini Iraq mapema mwezi huu.

Msemaji wa uongozi wa Jeshi la Marekani, Kapteni Bill Urban, alisema hapo jana kwamba ingawa hakuna mwanajeshi hata mmoja aliyeuawa katika shambulio hilo la Januari 8 katika kituo cha jeshi la anga cha Al Assad, wako wengi waliopatiwa matibabu kutokana na matatizo ya kupumua na bado wanaendelea na tathmini ya afya zao.

Urban alifafanua kuwa, ni utaratibu wa kawaida kwamba wanajeshi wote waliokuwapo katika eneo la shambulio wanachunguzwa kwa ajili ya kujua iwapo wamepata athari katika ubongo wao. Kama itaonekana athari, lazima wanasafirishwa kwa matibabu zaidi ya juu.

Baada ya shambulio hilo baadhi ya wanajeshi walisafirishwa kutoka kituo cha Al Asad nchini Iraq, kwenda kituo cha matibabu cha Landstuhl nchini Ujerumani. Wengine walipelekwa kambi ya Arifja nchini Kuwait kwa ajili ya uchunguzi. **DW**

## Mwanamke apimwa ujauzito apande ndege

**HONGKONG,** China

SHIRIKA la Ndege la Hong Kong, limemwomba msamaha abiria wake baada ya kumlazimisha kufanya majaribio ya ujauzito ili aweze kusafiri kutoka Hong Kong hadi eneo moja la Marekani.

Midori Nishida, 25, alikuwa akisafiri kwa ndege ya Shirika la Hong Kong mwezi Novemba hadi visiwa vya Kaskazini vya Mariana.

Kumekuwa jambo la kawaida kwa wanawake raia wa kigeni kuzaa kwa sababu ya uhakika wa kupata uraia wa Marekani. Ndege hiyo ilikuwa inataka kuhakikisha sheria za uhamiaji za Marekani zinafuatwa.

Awali, shirika hilo lilisema kwamba ilikuwa ni sehemu ya kuhakikisha kuwa yuko katika hali nzuri kusafiri. Hata hivyo, limeomba msamaha kwa tukio hilo. **BBC**

# Kiongozi Mkuu wa dini Iran atetea udunguaji wa ndege

**TEHRAN,** Iran

KIONGOZI mkuu wa dini wa Iran Ayatollah Ali Khamenei ametetea majeshi ya nchi yake baada ya kukiri kuwa ilidungua ndege ya abiria ya Ukraine kimakosa.

Amesema kikosi maalum cha majeshi ya ulinzi ya Iran Revolutionary Guard kilichohusika na mkasa huo kilikuwa kinalinda usalama wa Iran.

Maandamano ya ndani ya nchi na ukosoaji kutoka mataifa ya kigeni yameiweka Iran mashakani kuhusiana na jinsi inavyoshughulikia tukio hilo.

Lakini Ayatollah alitoa tamko hilo wakati wa alipoongoza sala ya Ijumaa mjini Tehran kwa mara ya kwanza tangu mwaka 2012.

Ametoa wito kuwapo na umoja wa kitaifa na kusema kuwa maadui wa Iran akiashiria Marekani na washirika wake wanatumia ajali hiyo ya ndege kuzima mauaji ya Jenerali Qasem Soleimani.

**Tunawaonya washirika wote wa Marekani ambao wameruhusu vikosi vya Marekani kuwa katika ardhi yao, kwamba wakijaribu uchokozi wa aina yoyote dhidi ya Iran yatalengwa.**

"Mamilioni ya raia wa Iran na maelfu ya raia wa Iraq walimwomboleza Soleimani," alisema.

Ndege aina ya Boeing 737-800 ya Shirika la Kimataifa la Ndege la Ukraine ilikuwa inasafiri kuelekea Kyiv kutoka Tehran Januari 8, ilipoanguka muda mfupi baada ya kuanza safari. Abiria wote 176 waliokuwa ndani ya ndege hiyo wengi wao raia wa Iran na Canada, walifariki.

Utawala wao pia uko kwenye shinikizo kutokana na kuporomoka kwa uchumi hali iliyosababishwa na vikwazo vya Marekani.

Mara ya mwisho alifanya hivyo ilikuwa mwaka 2012 wakati wa kumbukizi ya miaka 33 ya mapinduzi ya kiislamu katika nchi hiyo.

Baadhi ya mambo aliyozungumza ni kukosoa na kuutaja utawala wa Rais wa Marekani Donald, kuwa una chuki na kwamba hatua ya Iran kushambulia kwa makombora vituo vya wanajeshi wa Marekani nchini Iraq ilikuwa sawa na kofi la usoni kuonyesha taifa hilo kuwa Mungu anaunga mkono Wairan.

Pia alielezea kikosi maalum cha Quds ambacho Marekani imetambua kama shirika la kigaidi – kuwa ni shirika la kibinadamu linalothamini utu. Alitaja mazishi ya Soleimani na hatua ya majeshi ya nchi yake kama mwanzo mpya wa kihistoria.

Siku ya Jumatano, Rais Hassan Rouhani aliomba kuwapo kwa mshikamano wa kitaifa.

Lakini katika ishara ambazo hujitokeza kwa nadra ndani ya utawala wa Iran, Rais Rouhani amelitaka jeshi kuwajibika kwa kutoa maelezo ni kwa vipi waliidungua ndege ya Ukraine.

Saa chache kabla, makombora ya Iran yalilenga kambi mbili za jeshi la anga nchini Iraq zilizokuwa na wanajeshi wa Marekani.

Shambulio la roketi lilikuwa kisasi baada ya ndege isiyokuwa na rubani ya Marekani kufanya shambulizi Baghdad na kusababisha kifo cha Jenerali Qasem Soleimani. **BBC**



Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wakiwasilisha mashtaka katika Bunge la Seneti kwa ajili ya kuanza kusikilizwa kwa mashtaka dhidi ya Rais Donald Trump, juzi. **PICHA: DW**

# Rais Trump ashtakiwa, ushahidi mpya waibuka

**WASHINGTON,** Marekani

BARAZA la Seneti la Marekani limefungua mashtaka ya kumwondoa madarakani Rais Donald Trump baada ya kushtakiwa kwa makosa ya matumizi mabaya ya madaraka pamoja na kulionesha dharau Bunge.

Kesi hiyo ilianza Alhamisi iliyopita, huku maseneta wakisimama na kula kiapo cha kusimamia haki bila upendeleo kama majaji, waendesha mashtaka wa baraza hilo wakisoma mashtaka, na mwanasheria mkuu John Roberts akiongoza kesi hiyo.

Maseneta wanne wanaosimamia kesi hiyo, wanachuana ili mmoja wao kuteuliwa kama mgombea urais kupitia tiketi ya chama cha Democtratic na kupambana na Trump katika uchaguzi ujao.

Trump anakabiliwa na mashtaka mawili baada ya Baraza la Wawakilishi kupiga kura ya kumshtaki mwezi uliopita, moja likiwa ni matumizi mabaya ya madaraka yake kwa kuishinikiza Ukraine kumchunguza hasimu wake wa chama cha Democratic Joe Biden. Trump pia anashtakiwa kuzuia uchunguzi dhidi yake uliofunguliwa baadaye na Bunge.

Rais huyo anaendelea kusisitiza kuwa hana makosa, kwa mara nyingine tena ameyatupilia mbali mashtaka hayo na kusema kuwa ni uwongo mtupu.

Trump hatarajiwi kupatikana na hatia katika baraza hilo linalohodhiwa na maseneta wa chama chake cha Republican. Hata hivyo kuna ushahidi mpya unaodhihirisha vitendo vya Trump dhidi ya Ukraine.

Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi imesema Alhamisi iliyopita kwamba serikali ya Trump ilikiuka sheria ya nchi kwa kuzuia msaada wa usalama kwa Ukraine, ambayo ina mpaka mmoja na Urusi yenye uadui nayo.

Wakati huo huo, mshirika wa wakili binafsi wa Trump, Lev Parnas, ambaye naye ameshtakiwa amewasilisha nyaraka za ushahidi mpya kwa waendesha mashtaka unaomhusisha kiongozi huyo na sera ya kigeni isiyo rasmi inayoendeshwa na Giuliani.

Ushahidi huo mpya umewashinikiza maseneta kuita mashahidi wapya katika kesi hiyo, hali iliyozua mabishamo ambayo bado hayakupatiwa suluhisho.

Spika wa Bunge Nancy Pelosi alisema ushahidi huo mpya kutoka kwa Parnas unahitaji kufanyiwa uchunguzi, ambao hautarajii kufanywa na Mwanasheria Mkuu wa Trump.

Baraza hilo la Seneti litatoa wito rasmi kwa Ikulu ya Rais kuhudhuria katika kikao hicho, na timu ya kisheria ya rais inatarajiwa kutoa jibu Jumamosi wakati mawakili wataanza kusikiliza.

Wiki ijayo, wakati Baraza la Seneti likisikiliza hoja za ufunguzi wa kesi hiyo, Trump atakuwa katika mji wa mapumziko wa Davos nchini Uswisi. **DW**

# HADITHI

WASWAHILI wana msemo wao unaosema kuwa ufukara ni jereha la ulimwengu. Wakiwa na maana, mtu fukara mara nyingi hukutana na mitihani mikubwa duniani, ambayo mingi husababishwa na baadhi ya binadamu wengine wenye vipato kwa kuwaona hawana thamani na hawahitajiki kuwa na kitu chochote cha thamani.

Kijana anayetoka kwenye familia duni Kadili, anatokea kupendwa na msichana mrembo anayetoka kwenye familia ya kitajiri, Edina. Lakini kitendo hicho kinamsababishia kijana huyo matatizo makubwa ambayo hajawahi kuyapata katika maisha yake, kiasi cha maisha yake kuwa hatarini. Fuatilia mkasa huu wa aina yake.

# JUMBA JEKUNDU- 36

**Mtunzi anapatikana (0716 350534)**

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya dakika tatu kupita, Kadili aliingia sebuleni akiongozana na wanawake wawili. Mmoja ni mama wa makamo na mwingine ni msichana ambaye umri wake haukutofautiana sana na Edina.

"Mama, napenda kukutambulisha kwa rafiki yangu, anaitwa Edina na Edina, huyu ni mama yangu mzazi." Kadili alinyamaza kidogo akiwatazama kwa zamu mama yake pamoja na Edina.

Edina alisimama na kupiga magoti kwa heshima zote.

"Shikamoo mama."

"Marahaba mwanangu, hujambo?"

"Sijambo mama, leo nimeamua kuja kuwatembelea."

"Karibu mwanangu, hapa ni kwako, karibu muda wote ule unakaribishwa."

Mama Kadili alishangazwa kwa uzuri na urembo wa mwanamke huyo. Hakuona kasoro yoyote kwenye mwili, nywele na nguo za mwanamama huyo.

Manukato yake yaliifanya nyumba zima mle ndani kunukia kana kwamba wote mle walikuwa wamejipulizia manukato hayo, au nyumna ndiyo imepuliziwa.

"Mhh, ndiyo maana mwanangu aliamua kujitoa muhanga kufa na kupona kwa msichana huyu. Amepata tabu sana. Amevumilia tabu sana na amekuwa mvumilivu kwa kila kitu. Alikuwa sahihi, huyu ni malkia wa uzuri," alijisemea moyoni.

"Eliza, kutana na rafiki yangu anaitwa Edina, bibie, huyu anaitwa Eliza ni dada yangu binamu, mtoto wa mjomba wangu aliyezaliwa tumbo moja na mama yangu."

Edina alisimama na kumkumbatia Eliza.

"Hujambo mrembo." Edina alimsabahi akiwa amemkumbatia.

"Sijambo mrembo." Alijibu.

Walitazamana kwa sekunde kadhaa. Eliza alikiri kuwa Edina ni mrembo wa warembo na hapo alipojua ni kwa nini Kadili alikuwa hakubali hata chembe suala la kumuoa yeye kama wazazi walivyotaka na akawa anapiga chenga au kuchelewesha mpaka aone imeshindikana kabisa.

Kwa Edina kufika pale, alijua kabisa kuwa biashara yake ya kuoana na kaka yake binamu Kadili imekufa rasmi.

****************************

Hali ilitulia kidogo. Kila mtu akarudi kwenye hali yake ya kawaida. Tayari ilishatimu saa 10:00 jioni. Mama Kadili na mtoto wa kaka yake Eliza walikuwa wameshatoka sebuleni kwenda kutayarisha chakula cha usiku.

Meze naye aliamua kuaga kwa makusudi ili kuwapa nafasi Kadili




**Alijiegemeza kwenye mapaja ya Kadili. Pamoja na kwamba ametoka kwenye familia ya kitajiri na anakaribia kurithi mali na kampuni zote za marehemu mama yake, lakini bado alibaki kuwa ni mwanadamu na mtoto wa kike mwenye hisia kama mwingine yoyote yule.**

na Edina waendelee na maongezi binafsi kwa utulivu.

"Nitarudi baadaye kidogo." Aliaga Meze.

Zilipita dakika mbili za ukimya. Kila mmoja akiwaza nini cha kuongea. Ulikuwa ni muda muhimu kwa kila mmoja kuweka lengo lake.

Tangu kifo cha mama Pauline mama mzazi wa Edina, walikuwa wamekutana mara moja tu kwenye hoteli ya Safari Beach maeneo ya Kunduchi jijini Dar es Salaam, ingawa walikuwa wakiwasiliana kwenye simu.

Waliongea mengi, lakini hakuna yoyote aliyemfunulia mwenzake la rohoni. Kadili aliona leo hii ndiyo siku ya kueleza kila kitu.

Kwanza kabisa alikuwa anajiamini kwa sababu yuko nyumbani kwao, hivyo hata kama Edina alimkatalia, atakataa kistaarabu.

Pili hakutaka kumwambia jambo kama hilo sehemu nyingine yoyote ile kwa sababu ya kumpenda na kumuheshimu.

Mtu mwenye heshima na anayependwa anatakiwa aambiwe kitu kama hicho sehemu maalum na wakati maalum.

"Leo ndiyo mwisho. Leo ndiyo siku ya kuweka kila kitu mezani." Alijiambia mwenyewe.

Alivaa ujasiri na kuangalia kwa makini Edina aliyekuwa kama mtu anayefikiria jambo.

"Karibu Edina hapa ndiyo nyumbani."

"Nashukuru Kadili, nimeshakaribia."

"Umetustukiza lakini."

"Nilikwambia leo nilitaka kukufanyia 'sapraizi.'

"Sasa kwa hizo 'sapraizi' zako utakula ugali na maharage."

"Poa tu, si chakula? Chakula hata kikiwa cha kawaida, lakini ukila na rafiki zako kinakuwa kitamu, lakini hata chakula kikiwa kizuri vipi, ukila tu huku una mambo mengi kichwani au na watu ambao wanaokuumiza kichwa, hakinogi." Alisema huku akimtazama Kadili kwa kumuibia jicho.

"Sikiliza Edina." Alisema Kadili huku akimsogelea karibu kabisa na miili yao ikawa imegusana.

Ni ujasiri ambao hakuwahi kuufanya Kadili, kiasi cha kumshangaza hata Edina mwenyewe.

"Leo unefika nyumbani kwangu. Ni fahari kubwa sana kwangu na kwa familia yangu. Jinsi mimi na familia yangu tulivyo, maisha yetu na nyumba yetu, huwezi kabisa kulinganisha na wewe ulivyo, maisha yako na mali ulizonazo ulizoachiwa na mama yako. Watu hapa mtaani saa hizi kila mmoja yupo nje ya nyumba wakiulizana na kutaka kujua nini kinafanyika na nini kitatokea na yule aliyekuja ni nani.

Edina wewe ni rafiki yangu, tumepita kwenye mambo kadhaa mazuri na mengi magumu ya kutisha na ya kukatisha tamaa, lakini leo kwa mastaajabu uko nyumbani kwangu.

Leo kwa heshima na taadhima, naomba kukutamkia rasmi kuwa mimi nakupenda. Nakupenda tutoka kwenye nafsi yangu. Na siyo kwamba nimekupenda leo. Nilianza kukupenda tangu siku ya kwanza 'blue star' uliponichagua tucheze muziki. Moyo ulianza kunyanyasika. Shahidi yangu alikuwa ni Meze. Maswahibu yote yaliyonipata ya kuchukuliwa na mabaunsa wa mama yako na kuteswa nusura kuuawa ilikuwa ni kwa sababu ya penzi langu kwako.Muda mrefu nilikuwa nataka kukwambia hili, lakini muda ulikuwa bado, lakini nilitaka nikumbie hili sehemu sahihi. Edina naomba pokea ombi langu." Maneno haya aliyasema kwa sauti ndogo karibu na sikio la Edina.

Hakutaka mama yake na binamu yake, au dada zake kama wamerejea wasikie.

Sauti ilipenya neno kwa neno kwenye sikio la Edina. Mrembo huyo alishusha pumzi kwa nguvu kana kwamba alikuwa ameutua mzigo mzito uliokuwa unamuelemea na kutembea umbali mrefu.

"Hatimaye umesema." Alinong'ona.

"Kadili nilitegemea hili. Najua ulitaka kulisema tangu zamani, lakini mazingira yalikuwa hayakuruhusu.

Wakati ule ulikuwa bado uko chuo, uliogopa pengo lililopo baina ya maisha yako na yangu ambao wanaume wengi wana matatizo hayo. Lakini pia vitisho vya mama na wafanyakazi wake wakati huo, pamoja na udhalilishaji wa hali ya juu, yalikufanya uwe au uonekane mnyonge mbele ya wanyonge. Kusema kweli hata mimi ilinitia simanzi na huruma.

Nadhani nilikueleza kuwa hata mimi nilisimama juu yako, walitaka kukuua mle ndani ya jumba letu, lakini niliwaambia kuwa chochote mnachotaka kumfanya fanyeni, lakini msimuue au kumtesa kiasi cha kusababisha ulemavu au kutetereka kwa afya yake, la sivyo na mimi nitajiua, kitu ambacho marehemu mama hakutaka kabisa kitokee. Taarifa ya siri nilipenyezewa kuwa kama nikikataa kuolewa basi watakutafuta wakuue kwa sababu walidhani kuwa wewe ndiyo unayesababisha mimi nikatae kuolewa, ndiyo iliyofanya mimi kuolewa bila kupenda kwa Dk.Kapilima ili kulinda uhai wako.

Tayari wao waliona kuwa mimi nakupenda na wewe nakupenda. Ni kweli Kadili hakukuwa na kitu kama hicho. Wala hakuna hata siku moja tuliopanga au kuambizana maneno ya mapenzi. Tuliogopana. Lakini siku zote mapenzi ni hisia na si maneno. Penzi linaonekana zaidi kuliko kusikika. Muonekano wetu tu bila kuambiana ilionekana tunapendana. Na hata waliotuona waliona kabisa tunapendana. Lakini leo ndiyo unaniambia maneno hayo.

Na mimi nakuambia kuwa yale yote waliokuwa wakiyaona na kuhisi yalikuwa ni kweli. Na mimi pia nakupenda." Alisema Edina naye akijibu mapigo kutoka kwa Kadili.

"Hatujapendana leo, sema tu leo tumeambizana ukweli ulio moyoni mwetu, lakini tulipendana tangu zamani. Vitendo vyako na vyangu vilionekana kuwa tunapendana. Na yote yaliyotokea ni kwa sababu tunapenada. Umetesema kwa sababu unanipenda. Nimeteseka kwa sababu nakupenda. Niko hapa leo kwa sababu nakupenda." Alinong'ona Edina na machozi yalianza kumtoka. Alilia kwa kwikwi, lakini bila sauti.

Alijiegemeza kwenye mapaja ya Kadili. Pamoja na kwamba ametoka kwenye familia ya kitajiri na anakaribia kurithi mali na kampuni zote za marehemu mama yake, lakini bado alibaki kuwa ni mwanadamu na mtoto wa kike mwenye hisia kama mwingine yoyote yule.

Kwa muda mrefu alikuwa na funda moyoni mwake. Alimpenda Kadili licha ya umasikini wake. Alipambana bila kumwambia chochote. Lakini leo anamfunulia ukweli baada ya yeye kufunuliwa ya moyoni kutoka kwa mtu aliyempenda. Kilikuwa ni kilio cha furaha. Kilio cha kukaribia kupata ushindi ulioonekana mgumu na wenye vikwazo.

**Itaendelea Jumamosi**

# TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## MATANGAZO MCHANGANYIKO

**MKOPO WA HARAKA KUTOKA ENTERPRISE FINANCE LIMITD (EFL).** Kwa mahitaji kama kulipa ada ya shule, kodi, kuboresha biashara, kumalizia tenda etc. Kwa maelezo zaidi **piga 0758 112 332. Karibu EFL**.

**TANZANIA RESEARCH AND CAREER DEVELOPMENT INSITUTE:** Inatangaza mhula mpya wa masomo Certificate na Diploma za kilimo na maendeleo ya jamii.maelezo zaidi tembelea tovuti yetu www.tracdi.ac.tz Simu:**0714404491/0746995144**


**NIPASHE NI JIBU LAKO**

NJOO UTANGAZE NASI

BIDHAA YAKO

KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz,


## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**YUSUPH KASSIM KISWAMBA** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya SANLG yenye namba za usajili MC 500 BYP. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/CEN/RB/3754/2020.**

115589702

## PROSHARE CAPITAL LIMITED

*Kutangaza Magari Yanayouzwa;*

1. **PETER G. NDOKEJI** (SUZUKI MARUTI T826 CJK)
2. **JONES A. MWANG'ONDA** (TOYOTA IST T110 DPN)
3. **DANIEL R. MAKO** (HILUX T485 ABA)
4. **OCTAVIAN G. MKORONGWE** (NOAH T803 DHU)
5. **JOSEPHAT A. MANEMBE** (T/PROGRES T403 DHF)
6. **JAMILA M. KALLAGE** (T/NOAH T934 DLV)
7. **ALLY A. ALLY** (SUZUKI CARRY T870 CYT)
8. **JOSEPH J. MHERE** (SUBARU LEGACY T965 DPN)
9. **CHRISTOPHER MTIGA** (SUZUKI CARRY T327 BRZ)

115589202

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**

**MAHAKAMA YA MWANZO DODOMA MJINI**

**WILAYA YA DODOMA**

**MADAI NAMBARI 312/2019**

**MDAI AUGUSTINE J URASSA**

**DHIDI YA**

**MDAIWA SHEIKHAN MUSSA**

**KWA SHEIKHAN MUSSA**

kwa kuwa mdai ameleta madai yake kwamba madai ya **TSHS 716,500**

kwa hiyo unahitajika kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii siku ya Jumanne 28/1/2020 saa 2:00 asubuhi kwa kujibu madai haya na kwa kuwa siku hiyo ya kuitwa shauri hilo ni lazima kuleta mashahidi wako na hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo.

Angalia kama hukuhudhuria siku iliotajwa hapo juu Mahakama ikithibitisha kama umepokea kuitwa shaurini hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe 15/1/2020.

Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo

115589502

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF DODOMA**

**AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 98/2019**

**In the matter of the Estate of the Late OLIPA MATHAYO JOHN of Ihumwa area within Dodoma Region and**

**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTER OF ADMINISTRATION BY ELASTO ANDASON MNHAMBA**

**GENERAL CITATION**

**(RULE 75 PROBATE RULES GN 369 OF 163)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of administration is made to the above named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 27 Day of January, 2020.

**Date at Dodoma this 16th Day of October, 2019.**

**ERASTO MNHAMBA**

**PETITIONER**

**Presented for filing this 15 day of January, 2020.**

115589602

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo**
**CHAMWINO MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;5/2020**
**Ombi la OMARY ALLY SANAMBUYA**
**Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu**
**ABDU ALLY LUANDA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 30/01/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 17/01/2020.

Sahihi ya Hakimu.

115589802





TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Mustafi: Mashabiki Arsenal wamenitesa

**LONDON,** England

MCHEZAJI Shkodran Mustafi amebainisha kwamba alikuwa na wakati mgumu kudhibiti presha aliyokuwa akiipata kwa kufanya makosa kadhaa wakati akiichezea Arsenal.


Beki huyo wa kimataifa wa Ujerumani, Mustafi alijiunga na "Washika Bunduki" hao akitokea Valencia mwaka 2016, lakini kiwango chake kimekuwa kikishuka kwa misimu ya hivi karibuni.

Msimu huu mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, amekuwa akitumika zaidi kwenye mechi za Ligi ya Europa na Kombe la EFp, ingawa Calum Chambers amekuwa nje ya dimba na Konstantinos Mavropanos kujiunga kwake na Nurnberg kwa mkopo kunamaanisha kwamba anaweza kuwa na nafasi ya kucheza kwenye Ligi Kuu.

"Nimeamua kuinamisha kichwa changu chini kutokana na shutuma zinazokuja kwangu na nataka kufanya kazi kwa bidii.

"Niliamua kufumba macho yangu na kujikita zaidi kwenye kazi, na nafikiri mashabiki wataikubali kazi yangu," alisema Mustafi wakati wa mahojiano yake na tovuti ya klabu ya Arsenal.

"Nimeaamua kuvuta soksi zangu na kuzaliwa tena upya kwa uchezaji na kuisaidia timu yangu.






# MARTINEZ ANG'ANG'ANIA INTER MILAN AKIIKATAA BARCELONA

**MILAN,** Italia

LAUTARO Martinez ana "furaha kubwa" kuwa Inter Milan licha ya kiwango chake msimu huu kumfanya awaniwe na klabu nyingi barani Ulaya.

Mshambuliaji huyo wa kimataifa wa Argentina amefunga mabao 15 msimu huu likiwamo kwenye sare ya 1-1 na Atalanta wikendi iliyopita.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22, upatina wake na Romelu Lukaku umeifanya safu ya ushambuliaji ya 'Nerazzurri' hao kuwa ya kutisha zaidi huku wakikimbizana na Juventus katika mbio za ubingwa wa Ligi Kuu ya Italia, Serie A.

Kiwango chake pia kimeifanya klabu ya Barcelona kumtaka huku wakiwa wanakabiliwa na kumkosa Luis Suarez kwa miezi minne, huku pia Manchester City pia ikitajwa kumtaka Martinez ili kuwa mrithi wa mfungaji wao wa wakati wote, Sergio Aguero.

"Nina furaha kubwa kuwa hapa Inter, watu wananipenda mimi na nawapenda wao," Martinez alisema akiiambia TyC Sports.

"Kama unazungumza kuhusu mimi (kama natakiwa zaidi kwenye usajili) ni kwa sababu nafanya kazi yangu vizuri. Lazima niendelea na kazi hii kwa ufasaha zaidi.

"Nina utulivu mzuri, naishi hapa na kila siku najisikia mwenye furaha kubwa zaidi kuwa hapa."

# *Young akaribia kutua Inter*

**MILAN,** Italia

ASHLEY Young anajipanga kujiunga na Inter Milan baada ya Manchester United kukubali ada ya kumuuza beki huyo mzoefu wa kati.

Kwa mujibu wa mtandao wa Omnisport uhamisho huo utawagharimu miamba hao wa Ligi Kuu ya Italia, Serie A, kiasi cha euro milioni 1.5.


Young alijiunga na United akitokea Aston Villa mwaka 2011 na amecheza mechi 261 akifunga mabao 19.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 34, ameshinda mataji makubwa manne akiwa na 'Mashetani Wekundu' hao, likiwamo la Ligi Kuu msimu wa 2012-13, ingawa kuibuka kwa kijana Brandon Williams kumemfanya kukosa nafasi ya kucheza mara kwa mara msimu huu.

Wakati wake akiwa pale Old Trafford, Young alibadilishwa nafasi ya kucheza na kutoka winga na alikuwa chaguo la kwanza la kocha wa timu ya Taifa ya England, Gareth Southgate kama beki wa kushoto wakati timu hiyo ikifika nusu fainali ya Kombe la Dunia mwaka 2018.

Kipigo cha 2-1 kwenye muda wa ziada kutoka kwa Croatia mjini Moscow ndiyo mechi yake ya karibuni zaidi kati ya zile 39 alizoichezea timu hiyo ya taifa na kufunga mabao saba.

Uhamisho wa Young kutoka hapo Old Trafford kwenda San Siro, utamfanya kuungana na wachezaji wenzake wa zamani, Alexis Sanchez ambaye amesajiliwa kwa mkopo hapo Inter na Romelu Lukaku ambaye alisajiliwa kwa mkataba wa kudumu.



## Vieira: Uvumi Arsenal haukunisumbua

**PARIS,** Ufaransa

PATRICK Vieira amesisitiza hakukuwa na nafasi kwake kumrithi Unai Emery pale Arsenal kwa sababu ana majukumu na Nice kwa asilimia 100.

Nahodha huyo wa zamani wa Arsenal alikuwa akihusishwa na kupewa kazi pale kwa 'Washika Bunduki' wa London tangu kuondoka kwa Arsene Wenger mwaka 2018, lakini Mikel Arteta alichukua nafasi hiyo baada ya kufukuzwa kwa Emery Novemba mwaka jana.

Mfaransa huyo amesema hakukuwa na mazungumzo yoyote na Arsenal kuhusu nafasi hiyo, ingawa kocha huyo wa Nice alibainisha kwamba angeipiga chini ofa kutoka klabu yoyote.

"Hapana, lakini hakuna nafasi kwenye akili yangu kuwa na mazungumzo hayo," alisema Vieira akiiambia Daily Mail.

"Akili yangu na majukumu yangu yapo hapa Nice. Hapa ni sehemu nilipo kwa sasa na sina mpango wa kwenda popote.

"Uvumi kuhusu kwenda kuinoa Arsenal si kitu kilichonisumbua. Sijui nini kitatokea kesho, na ndio maana sitaki kuufanya ubongo wangu ufikirie sehemu ambayo haipo.

"Klabu inajua kwamba nataka kubakia hapa na najua kwamba wanataka mimi nibakie hapa kwa asilimia 100."

Hata hivyo, Vieira alisema alifanya majadiliano ya uwezekano wa kuchukua nafasi kutoka kwa Wenger kabla ya kuwa kocha wa Nice.





## JAMES AJIFUNGA MIAKA 5 CHELSEA

**LONDON,** England

NYOTA Reece James amesaini mkataba mpya na Chelsea ambao utamweka hapo Stamford Bridge hadi mwaka 2025, klabu hiyo ya Ligi Kuu ya England imethibitisha.

James amefurahia mafanikio msimu huu na klabu yake hiyo aliyokulia, baada ya kupata mafanikio msimu wa 2018-19 wakati akicheza kwa mkopo kule Wigan Athletic.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20, amecheza mechi 18 kwenye mashindano yote msimu huu kwa kikosi hicho kinachonolewa na kocha Frank Lampard akifunga katika mchezo wake wa kwanza dhidi ya Grimsby Town kwenye Kombe la EFL na sare ya kufungana 4-4 kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Ajax.

"Imekuwa ni ndoto yangu kuwa hapa Chelsea na kucheza kila wiki na kuwa na mkataba wa miaka mitano na nusu mingine ni ndoto iliyotimia," alisema akiiambia tovuti ya klabu hiyo.

"Mara zote nilitaka kuwa hapa na kupata miaka mingine mitano na nusu ni jambo kubwa sana kwangu na kwa familia yangu."

## *Utd yatajiwa dau la Fernandes*

**LISBON,** Ureno

KOCHA wa Sporting CP, Silas amesema Bruno Fernandes ana thamani ya fedha nyingi zaidi kuliko kiasi anachohusishwa nacho kwenda Manchester United.

Fernandes ameripotiwa kwamba anakaribia kujiunga na miamba wa Ligi Kuu ya England United, kwa ada inayotajwa kuwa ni pauni milioni 51, ingawa inaaminika kuwa Sporting inamzuia kwa kutaka fedha nyingi zaidi.

Baada ya kuthibitisha kwamba Fernandes atakuwapo kwenye mchezo wa 'dabi' ya Ureno dhidi ya Benfica jana Ijumaa, Silas alimsifia nahodha huyo wa Sporting.

"Ni mchezaji wa maajabu, bora na mwenye thamani kubwa kwenye ligi, kama alivyokuwa msimu uliopita," alisema Silas akiwaambia waandishi wa habari.

"Nimesikia mtu mmoja akisema kwamba hana thamani ya fedha inayotajwa na ni kweli ana thamani ya fedha nyingi zaidi.

"Kwa kuongezea amejitolea yeye mwenyewe. Bruno ni bora na mwenye thamani. Ukiwa na mchezaji kama yeye ni jambo la kawaida kila mmoja kumtaka."

Fernandes, ambaye amekuwa akihusishwa na kutakiwa United, Tottenham na Real Madrid kipindi cha madirisha yaliyopita ya usajili, amefunga mabao 15 kwenye mashindano yote aliyoichezea Sporting msimu huu.

Kiungo huyo mwenye umri wa miaka 25, alifunga mabao 31 msimu uliopita, yakiwamo 20 ya kwenye Ligi Kuu ya Ureno, Primeira Liga.



HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# GUARDIOLA: TUNAHITAJI MAOMBI KUISHIKA LIVER

Asema kujituma zaidi, kucheza vizuri sambamba na kuomba, ndiyo njia pekee ya kuweza...

**MANCHESTER,** England

PEP Guardiola amefunguka kuwa Manchester City lazima "ijitume sana, icheze vizuri na kufanya maombi" ili kuweza kuziba pengo dhidi ya Liverpool, lakini anaamini bado kikosi chake kipo fiti kabisa kuweza kutoa ushindani kwenye mbio za ubingwa.

**City imeshinda ubingwa wa Ligi Kuu katika kila msimu kati ya miwili iliyopita, lakini ipo pointi 14 nyuma kwenye mbio za ubingwa dhidi ya Liverpool, ambayo pia ina mechi mkononi.**

Wakati kikosi chake kikionekana kuwa chini ya kiwango msimu huu, Guardiola yupo tayari kusisitiza athari ya majeruhi muhimu katika timu yake - wakati Aymeric Laporte na Leroy Sane wakiwa nje kwa kipindi kirefu huku David Silva na Sergio Aguero pia wakiwa katika mkumbo huo.

Alipoulizwa ni kwa namna gani timu yake itakavyoweza kujizatiti ili kuishika Liverpool, kocha huyo wa City aliwaambia wanahabari: "Kujituma zaidi, kucheza vizuri na kuomba.

"Na kikosi chote, ndiyo, [City inaweza kushindana]. Kuna vitu vingine ambavyo huwezi kuzuia. Tunaweza kufanya ambavyo tunaweza.

"Lakini mambo mengine hatuwezi kuzuia, kama ilivyo timu nzuri kama Liverpool wamefanya hivi hadi sasa. Kama kila mmoja atakuwa fiti tunaweza kulifanya hilo."

Guardiola alikataa kukubali, hata hivyo, kwamba kushindwa kufanya usajili katika dirisha hili la usajili kumechangia matatizo hayo.

"Hapana, nadhani timu ni nzuri. Ninaipenda," alisema. "Tulikuwa na matatizo ya majeruhi - vitu hivi vinatokea, na kisha Liverpool ni ya kushangaza. "Ni mabingwa wa Ulaya na wamepoteza pointi mbili. Na baada ya hilo, tunawapongeza wao. Ninajua umbali tuliopo [nyuma] si tulipopaswa tuwe, lakini ndivyo ilivyo. "

Kama mwaka 2019 ulivyofikia mwisho, Guardiola pia anataka kumbushia kwa kutoa ofa ya mafanikio ya City ya mwaka 2019 - kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu, Kombe la FA, Kombe la EFL na Ngao ya Jamii kabla kuangukia nafasi ya tatu kwenye msimamo wa ligi.

"Ilikuwaje mwaka 2019? Sasa watu wanasema ilikuwa janga. Tulishinda mataji manne mwaka 2019," alisema. "Ulikuwa mwaka wa kushangaza kwetu, wakati tulifurahia sana.

"Katika baadhi ya mechi katika msimu uliopita, tulihaha kidogo. Lakini ulikuwa mwaka wa kushangaza kwetu."

## ZISIKUPITE

### CAVANI AZUIWA KUTUA UNITED

MANCHESTER United itapewa ofa ya kumsajili mshambuliaji wa Paris St-Germain, Edinson Cavani, 32, kwa uhamisho huru - lakini imeambiwa haiwezi kumpata mwezi huu. ***(Manchester Evening News)***

### WERNER AIFUNGULIA CHELSEA

CHELSEA inapewa nafasi zaidi ya kumsajili mshambuliaji wa RB Leipzig, Timo Werner baada ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23, anataka kujaribu mwenyewe soka la Ligi Kuu England. ***(Bild, via Mail)***

### SANE BADO LULU CITY

MANCHESTER City bado ipo tayari kumbakisha winga wa Ujerumani, Leroy Sane, 24, ambaye amekuwa akihusishwa na Bayern Munich, na haijanyosha mikono juu ya matumaini ya kumshawishi kusaini mkataba mpya. ***(Metro)***

### KANE HATIHATI EURO 2020

MSHAMBULIAJI wa Tottenham na England, Harry Kane, 26, amekuwa akielezwa na mmoja wa madaktari bingwa wa upasuaji Uingereza kuwa pengine anaweza kuikosa Euro 2020. ***(Press Association, via Sun)***

### MOURINHO AMTAKA CANCELO

KOCHA wa Tottenham, Jose Mourinho amezungumza na beki wa pembeni wa Manchester City na Ureno, Joao Cancelo, 25, kuhusu uwezekano wa kujiunga naye. ***(El Desmarque, via Mail)***

### SOUMARE NJIAPANDA EPL

KIUNGO wa Lille na Ufaransa U-21, Boubakary Soumare, 20, anajiandaa kuamua kati ya kusaini mkataba wa kuitumiakia Manchester United ama Chelsea kabla ya dirisha hili dogo kufungwa. ***(Sky Sports)***

### EMRE CAN AIGOMEA UNITED

KIUNGO wa Juventus na Ujerumani, Emre Can, 26, ametupilia mbali uwezekano wa kujiunga na Manchester United, kwa sababu ya uhusiano wake na klabu yake ya zamani ya Liverpool. ***(Tuttosport, via Mirror)***

### CITY, BARCA KWA MORANTE

MANCHESTER City inataka kuipiku Barcelona katika mbio za kumsajili kiungo wa Hispania U-19, Ivan Morante, 19, ambaye kwa sasa anaichezea Villarreal B. ***(Telegraph)***

### ASTON VILLA YAMTAKA NZONZI

ASTON Villa imekuwa ikihusishwa na kwenda kumsajili kiungo wa kimataifa wa Ufaransa, Steven Nzonzi, 31. Mchezaji huyo wa zamani wa Blackburn na Stoke kwa sasa anaichezea Galatasaray kwa mkopo akitokea Roma. ***(Telefoot, via Birmingham Mail)***

### ROBINSON AIVUTIA MILAN

AC Milan inapanga kumfuata beki wa kushoto wa Wigan na Marekani, Antonee Robinson, 22, beki kinda wa Hearts, Mscotland Aaron Hickey, 17. ***(Sky Sports)***

### BIELSA, LENNON KWA POVEDA

KOCHA wa Celtic, Neil Lennon anakabiliwa na vita kutoka kocha wa Leeds United, Marcelo Bielsa vya kumsajili winga wa Manchester City na England, Ian Poveda, 19, katika dirisha hili la usajili la Januari. ***(Express)***

HABARI MICHEZO

## Mghana wa Yanga atua na mbwembwe

**Na Mwandishi Wetu**

MGHANA wa Yanga, Bernard Marrison, ametua jana na kueleza kuwa amekuja Tanzania kufanya kazi katika klabu hiyo na Wanayanga watampenda tu.

Marrison (pichani) ambaye anacheza nafasi ya ushambuliaji, alitua jana nchini akitokea kwao Ghana kwa ajili ya kumalizia taratibu za awali za kuitumikia Yanga.




"Rasmi nimetua ndani ya Yanga kufanya kazi na ninaamini tutakuwa vizuri kutokana na ubora wa kikosi sambamba na sapoti ambayo tutaipata kutoka kwa mashabiki.

"Hakuna jambo lingine ambalo nimekuja kulifanya Yanga zaidi ya kazi, hivyo kikubwa ni sapoti kutoka kwa wachezaji na mashabiki," alisema.

DC Motemma Pembe, Orlando Pirates na AS Vita ni baadhi ya timu ambazo Marrison amewahi kuzitumikia kabla ya kutua Yanga.

## Boban, Chuji waipa jeuri Singida United

**Na Mwandishi Wetu**

PAMOJA na kushika nafasi ya pili kutoka mkiani ikiwa na alama 10 baada ya mechi 16, uongozi wa Singida United bado unaimani ya kupambana msimu huu ili kubaki Ligi Kuu kutokana na usajili walioufanya.

Singida United ilikuwa ikitisha vigogo vya Ligi Kuu, Simba na Yanga, lakini msimu huu wa 2019-2020 umekuwa mbaya kwao huku ikiwa imeambulia ushindi mara mbili tu, kutoka sare nne na kupoteza mechi 10.

Katika dirisha dogo lililofungwa Januari 15, Singida United imewasajili wa wachezaji wakongwe ambao wameanza kazi ikiwa ni pamoja na Haruna Moshi 'Boban' na Athuman Idd Chuji.

Akizungumza na mwandishi wetu, Ofisa Habari wa Singida United, Cales Katemana, alisema wachezaji walikuwa na masuala mengi yaliyokuwa yanawasumbua, lakini wamefanya kikao nao na wanaamini kitawasaidia kurejesha morali.

"Mambo hayakuwa mazuri mwanzoni ila tayari kwa sasa tumeanza kurejea kwenye ubora wetu, ushindi mbele ya Ruvu Shooting umetuongezea nguvu, wale wanaofikiria tutashuka daraja hilo litabaki kuwa stori," alisema.

# UBABE WA MTIBWA WAISHIA KWA KMC

**Na Adam Fungamwango**

MABINGWA wa Kombe la Mapinduzi Mtibwa Sugar, jana walikiona cha moto kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam, baada ya kukubali kichapo cha mabao 2-0 kutoka kwa KMC ya Kinondoni kwenye mfululizo wa mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara.

**KMC ilionekana kama imetumwa kuzilipia kisasi timu za Dar es Salaam, Simba na Yanga ambazo zilifungwa na Mtibwa kwenye Kombe la Mapinduzi lililomalizika Januari 13 mjini Zanzibar.**

Ikionekana kama bado ina kiwewe cha furaha cha kutwaa kombe hilo kwa kuichapa Simba bao 1-0 kwenye mechi ya fainali, Mtibwa ilijikuta ikifungwa bao la kwanza dakika ya 18 na Sadallah Lipangile kwa kisigino, baada ya kupokea pasi safi kutoka kwa Selemani Ndikumana, straika wa zamani wa Simba, aliyekuwa akicheza kwa mara ya kwanza kwenye kikosi hicho, akitokea Azam FC.

Dakika ya 41, Lipangile kwa mara nyingine tena, aliipatia KMC bao la pili, baada ya makosa ya kipa Shaaban Kado na mabeki wake kugongana na kumpa nafasi mfungaji kuudokoa mpira uliojaa wavuni.

Bao hilo linamfanya straika huyo kufikisha mabao manne, kwani Januari 5, pia alicheka na nyavu mara mbili kwenye Uwanja wa Liti mjini Singida, KMC ikiichapa Singida United mabao 2-0.

Mtibwa iliyotumia kikosi karibuni kile kile kilichoitoa kwa penalti Yanga kwenye hatua ya nusu fainali ya Kombe la Mapinduzi na kuifunga Simba kwenye fainali, lakini hakikufua dafu mbele ya KMC ambayo inaonekana kama imezinduka kutoka kwenye usingizi mzito kwa sasa.

Kwa matokeo hayo KMC sasa imekaa kwenye nafasi ya 17, ikiwa na pointi 17 na kucheza mechi 17, huku Mtibwa Sugar ikiwa kwenye nafasi ya 10, ikiwa baada ya kukusanya pointi 22 kwa michezo 16 ambayo tayari imecheza.




Wachezaji wa Simba wakimpongeza winga wa timu hiyo, Hassan Dilunga, baada ya kuifungia bao la kwanza wakati wakishinda 2-1 dhidi ya Mbao FC kwenye Uwanja wa CCM Kirumba juzi. **NA MPIGAPICHA WETU**

# *Mbao FC yajivunia wa dirisha dogo*

**Na Mwandishi Wetu**

LICHA ya juzi kukubali kipigo cha mabao 2-1 kutoka kwa mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Bara, Simba, uongozi wa Mbao FC unaamini kwa usajili wa dirisha dogo walioufanya kikosi chake kitaimarika zaidi.

Katika usajili huo wa dirisha dogo uliofungwa Januari 15, Mbao imesajili wachezaji sita.

Na juzi ikiwa katika uwanja wake wa nyumbani wa CCM Kirumba, ilikubali kipigo hicho kwa mabao ya Hassan Dilunga dakika ya 41 na Jonas Mkude dakika ya 46.

Mwenyekiti wa Mbao FC, Solly Njashi alisema wamejipanga kuhakikisha timu yao inafanya vema katika michezo ya Ligi Kuu iliyobakia.

Njashi aliwataja wachezaji waliowasajili katika dirisha dogo kuwa ni Hussein Iddi kutoka Mtibwa Sugar, Omary Wayne kutoka Friends Rangers, Wilson Wilson, wote wamesaini mkataba wa miaka miwili.

Wengine ni Mackyada Franco kutoka Coastal Union kwa mkataba wa miezi sita, Hamis Mwinshehe kutoka JKU ya Zanzibar kwa mkataba wa mwaka mmoja na Paul Maige kutoka timu ya vijana ya Azam FC ya vijana chini ya miaka 20 kwa mkataba wa miaka mitatu.

Kocha Mkuu wa timu hiyo, Hemed Morocco alisema ana imani na wachezaji hao kuwa watasaidia timu yao iweze kufanya vema katika michezo ya Ligi Kuu.

Michezo
Jumamosi Januari 18, 2020
Nipashe



Guardiola: Tunahitaji maombi kuishika Liver

HABARI UK.30

WALETENI HAO...



Majembe matatu ya Liverpool, Sadio Mane, Roberto Firmino na Mohamed Salah (kulia), yanayotarajiwa kuiongoza timu hiyo kesho, dhidi ya Manchester United kwenye mechi ya Ligi Kuu England itakayopigwa Uwanja wa Anfield. **PICHA: MTANDAO**

## Samatta achungulia 3 akimsubiri Mourinho

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI nahodha wa Taifa Stars na klabu ya KRC Genk ya Ubelgiji, Mbwana Samatta akikamilisha dili lake la kujiunga na Aston Villa inayochechemea kwenye msimamo wa Ligi Kuu England, Mtanzania huyo ana kazi kubwa ya kuanza kuipaisha katika mechi zake tatu za mwanzo kabla ya kumvaa Jose Mourinho.

Tayari Aston Villa imekubali kutoa pauni milioni 10 sawa na Sh. bilioni 29.7 za Tanzania kwa KRC Genk.

Jana Samatta alitarajiwa kukamilisha vipimo vya afya kwa klabu hiyo iliyopo nafasi ya 18 kwenye msimamo wa Ligi Kuu ikiwa na pointi 21 baada ya mechi 22, ikishinda sita, sare tatu, kupoteza 13, mabao 28 ya kufungwa na 43 ya kufungwa msimu huu.

Mechi za Aston Villa za Ligi Kuu zilizopo katika kalenda ya karibuni ni dhidi ya Brighton ugenini leo ambayo Samatta hawezi kucheza, lakini anapewa nafasi kubwa ya kuonekana dhidi ya Watford Januari 21 na kisha Leicester City Januari, 28.

Baada ya mechi hizo, wataifuata Bournemouth Februari Mosi, kisha Februari 16 kuikaribisha Tottenham inayonolewa na Mreno Mourinho mechi inayotarajiwa kuwa ngumu kwao.

Mchezo utakaofuata utakuwa ugenini dhidi ya Southampton hapo Februari 22.

# Mbelgiji Yanga hasira kwa Azam

**Na Somoe Ng'itu**

## ●●● Makocha watamba kuandaa kikosi kazi cha ushindi kila mmoja akipania kushusha...

HATUMWI mtoto sokoni! Ni kauli ambayo inaonekana kuwa wazi kuelekea mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara kati ya Yanga dhidi ya Azam FC utakaochezwa leo kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam majira saa moja usiku.

**Yanga inayonolewa na kocha Mbelgiji Luc Eymael, itashuka uwanjani kuwakabili Azam FC ikiwa na hasira ya kutaka kutibu mapema majeraha yake ya kipigo cha mabao 3-0 ilichopata kutoka kwa Kagera Sugar wakati wapinzani wao ambao ni mabingwa watetezi wa michuano ya Kombe la FA wakitaka kuendelea kuwatonesha baada ya kutoka kuwatia jeraha Lipuli FC kwa kuichapa 2-0.**

Akizungumza na gazeti hili jana, Meneja wa Yanga, Abeid Mziba, alisema kikosi chao kimejipanga vema kuwakabili Azam FC na makosa yaliyojitokeza katika mchezo uliopita yamerekebishwa na leo wanatarajia kupata matokeo mazuri.

Mziba alisema wachezaji wameahidi kupambana kuhakikisha wanarejea katika kasi ya ushindi ili kujiweka katika nafasi nzuri ya kulitwaa taji la Ligi Kuu Tanzania Bara ambalo linashikiliwa na wapinzani wao, Simba.

Meneja huyo aliongeza kila mchezaji anataka kuonyesha bado wanahitaji kutwaa taji hilo hivyo watapambana katika mechi ya leo na nyingine zitakazofuata za ligi hiyo.

"Kila mechi ina changamoto zake, tumeshaweka mambo sawa sawa, tunawakumbusha pia kuongeza umakini na kutumia vizuri nafasi tunazotengeneza, hakuna mechi rahisi katika ligi na ukimruhusu mpinzani wako kukukamata, ni vibaya, tuliona tulipokosea, hatutarudia makosa," Mziba alisema.

Kocha Msaidizi wa Azam FC, Iddi Cheche alisema kikosi chake kitaingia kuivaa Yanga kikiwa tofauti na hiyo inatokana na aina ya wachezaji waliopo kwa wapinzani wao hao.

"Mechi itakuwa ngumu, lakini kila mchezo tunaingia na mpango wake kutokana na kikosi cha wapinzani wetu kilivyo, tutaangalia eneo ambalo ni wazuri tutawadhibiti na tutaangalia mapungufu yao ili tutumie nafasi hiyo kuwamaliza," alisema Cheche. Aliongeza kuwa bado wanaamini wako katika mbio za kuwania ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, hivyo wanataka kuendeleza kasi ya ushindi ili malengo yao yatimie.

"Tumewaangalia katika mechi zao zilizopita, kila idara tumewasoma, kesho (leo), tutaingia tofauti ili dhamira yetu ya kuondoka na pointi tatu muhimu itimie," Cheche aliongeza.

Katika msimamo wa ligi hiyo inayoongozwa na Simba yenye pointi 38, Yanga wako katika nafasi ya nane wakiwa na pointi 25 baada ya kucheza mechi 13, wakati Azam FC yenye pointi 29 imeshuka uwanjani mara 14 na kwenye msimamo wa ligi iko katika nafasi ya tatu.

Ligi hiyo itaendelea kesho kwa mabingwa watetezi, Simba kuivaa Alliance FC kwenye Uwanja wa CCM Kirumba baada ya juzi kutoka kuibuka na pointi tatu dhidi ya Mbao FC katika dimba hilo lililopo jijini Mwanza.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >